Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 8 Februari, 2010**

## D U A

*Spika (Mhe. Samwel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza leo linaulizwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum Tabora.

Na. 115

**Fedha za Kukomboa Ng'ombe Waliokamatwa**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa kulikuwa na zoezi la kuhamisha mifugo kwenye meneo mbalimbali katika nchi hususani Ifufu na kadhalika; na kwa kuwa katika uzoefu hilo mfugaji mwenye mifugo yake alikuwa akitozwa kiasi cha shilingi 30,000/= kwa kila ng'ombe:-

(a) Je, fedha hizo zilikwenda wapi?

(b) Je, ni sheria ipi iliyohalalisha utozaji wa fedha hizo?

(c) Je, ni fedha kiasi gani kulikusanywa kutoka kwa wenye ng'ombe kama tozo kwa mifugo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kulikuwa na zoezi la kuhamisha mifugo kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Kilosa na huko Ihefu. Katika kutekeleza zoezi hilo kulikuwa na tozo la kiasi cha shilingi 30,000/- kwa kila ng'ombe katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Wakati wa ukusanyaji wa fedha hizi, stakabadhi halali za Serikali zilikuwa zikitumika, Fedha zilizokusanywa kwa Halmashauri ya Kilosa ziliwasilishwa katika Benki ya *NMB* Tawi la Kilosa akaunti ya Halmashauri Na 2181200019 *collection fund*.

Aidha katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali eneo la Ihefu kiasi cha fedha kilichokuwa kinakusanywa katika kila ng'ombe ni shilingi 10,000/-. Fedha hizo katika Halmashauri zote zilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo na operesheni iliyokuwa inaendelea.

(b)Mheshimiwa Spika, katika kuendesha zoezi hili Halmashauri ya Kilosa ilizingatia Sheria Ndogo ya udhibiti na uchungaji na njia ya kupitisha mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ya mwaka 2001 Tangazo la Serikali Na. 33.

Aidha, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali eneo la Ihefu zilitumika Sheria ndogo za vijiji vilivyopo katika eneo lililozunguka eneo la Ihefu. Mfano Sheria ya Kijiji cha Ubaruku, Mwanavala, Mkombwe, Madundansi na Luhanga. Hivyo, hakuna uvunjaji wa Sheria na Taratibu wala uporaji wa mifugo uliofanywa katika Wilaya ya Kilosa.

(c) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichokusanywa katika zoezi hilo ni shilingi milioni 577,884,500/- kwa upande wa Halmashauri ya Wilaa ta Kilosa. Kati ya fedha hizo shilingi 360,430,580/- zilitumika katika uendeshaji wa operesheni na shilingi 217,453,920 zilizotumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha katika Wilaya ya Mbarali eneo la Ihefu fedha iliyokusanywa ilikuwa shilingi 724,067,300/- kati ya fedha hizo shilingi 326,641,837/- zilitumika katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo na shilingi 397,425,463/- zilitumika katika operesheni iliyokuwa inaendelea.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kwenye majibu ya Waziri anasema hakuna sheria yeyote ambayo ilivunjwa na mambo yote yalikwenda shwari.

Je, Serikali ilipelekea nini kuunda Tume ya Ihefu ambayo mpaka leo taarifa haijaletwa hapa Bungeni? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, mimi *sensitivity* ya jambo hili naifahamu na ninajua kwamba ni jambo ambalo wafugaji wamekuja mpaka katika eneo hili nalifahamu.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba katika kufanya hili zoezi, hapa na pale palikuwa na malalamiko ambayo yalitokea kutoka kwa wananchi, na Serikali ili

ijiridhishe ijue kwamba ni nini kilichotokea ndipo ile Tume ikawa imeundwa ilikwenda mpaka Tabora na nimezungumza na Mkuu wa Mkoa kumwuulizia kwamba ilisema nini hakuna taarifa yeyeote ambayo ilikuwa imeshatolewa. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba Tume iliundwa katika maana kwamba kukiwa na jambo lolote linajitokeza hapa ambalo linaoonekana kwamba ni nyeti, basi ni jukumu la Serikali kuunda Kamati au Tume ili ione kwamba ni nini kilichotokea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kuongezea majibu ya Naibu Waziri kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ni kweli tume ya Ihefu iliundwa na ilitoa mapendekezo mbalimbali ambayo Serikali imeyafanyia kazi. Pia Tume nyingine iliundwa wakati wa zoezi mifugo la Kilosa na kule Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Tume hizi mbili Serikali imeanza kuzifanyia kazi, moja ni Serikali kukutana na wadau wa mifugo hapa Dodoma, tulikutana nao na tukaelezana namna bora ya kuboresha mifugo yetu katika nchi yetu.

Jambo la pili ambalo Serikali imefanya ni kuleta Miswada mbalimbali ambayo italetwa na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, moja ni kwa ajili ya Muswada wa malisho kwa ajili ya mifugo na Muswada mwingine wa usajili wa mifugo, zote hizi ni hatua za Serikali ili kuhakikisha kwamba zoezi la wafugaji kuchunga mifugo ovyo lisirudie tena.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kila njia kuhakikisha Miswada hii inakuja na hatua mbalimbali zinachukuliwa ili zoezi hili liwe linafanyika bila migogoro yeyote.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa upande wa Ihefu ameeleza kwamba zilipatikana shilingi milioni mia saba tu, lakini taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaonesha kulikuwa na shilingi bilioni tano zilizokusanywa kwa *HW5* ya Halmashauri ya Mbarari, na fedha hizo hazijarejeshwa wala kwa Halmashauri na hazijulikani zilitumika vipi, na Halmashauri ya Mbarali ilipokuja mbele ya Kamati yetu tuliwahoji na wao pia wanahoji kwamba hela hizo hazijarudi kwao.

Je, Serikali inatoa kauli gani na fedha hizo zitarejeshwa lini kwa Halmashauri ya Mbarali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mhehsimiwa Spika, mimi nafikiri hapa cha kufanya wala hakuna tatizo huyu Mbunge anatoa taarifa tu na Mbunge huyu ni Mwenyekiti wa *Local Authority Accounts Committee*, hasa huwezi kusema una-*doubt* anachokisema

hapa, mimi naomba atupe nafasi hili analolisema tulifuatilie ili tujue nini kilichotokea na baadaye tutamjibu. (*Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Willibrod Slaa na hasa kufuatia majibu mazuri sana yaliyotolewa na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kumthibitishia Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa ni suala la Mifugo linasimamiwa na sheria zake, kuna Sera ya mifugo ya mwaka 2006. Kuna sheria ya magonjwa ya mifugo Namba 17 ya mwaka 2006, kuna sheria ya *Veterinary* Namba 13 ya mwaka 2003, kuna sheria ya Ngozi na kuna sheria zingine mbalimbali.

Lakini nataka kumweleza pia kwamba kutokana na masuala haya yote yanayohusu mifugo kuwa na uzito wake, ndiyo maana paliundwa Tume ya Ihefu pamoja na Tume ingine iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kazi kubwa ya Tume hii ni pamoja na kuchunguza haya yote yakiwepo na matatizo hayo aliyoyazungumza ya fedha, baada ya ukamilisho na ripoti hiyo kukamilika kikamilifu haya masuala yote yataletwa hapa na kuweza kutolewa muafaka, ahsante sana.

**SPIKA**: Waheshimiwa tuwe na subira yatakuja baadaye, ingawa hizi ndiyo dakika za lala salama tena. (*Kicheko*)

Na. 116

**Mafao ya Madiwani Kulipwa na Serikali Kuu**

**MHE. CASTOR R. LIGALAMA:** Kwa kuwa, kuna habari kwamba mafao ya Madiwani baada ya Mabaraza yao kuvunjwa nchi nzima mwaka 2010 yatalipwa na Serikali Kuu.

(a) Je, kauli hiyo ni sahihi?

(b) Kama ni sahihi. Je, ni stahiil gani hizo ambazo kila Diwani ategemee kuzipata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kauli sahihi kuhusu kuwepo kwa mafao ya Madiwani baada ya Mabaraza yao kuvunjwa nchi nzima mwaka 2010 na mafao hayo yatalipwa na Serikali Kuu.

(b) Mheshimiwa Spika, kila Mheshimiwa Diwani ategemee kulipwa kiinua mgongo ambacho kittolewa kulingana na muda aliotumikia.

Waraka Kumb. Na. CHB:17/443/01 wa tarehe 26 Novemba, 2007 uliotolewa na Serikali kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote Tanzania Bara unaelekeza stahili za Madiwani wanapomaliza muda wao. Kiinua mgongo cha Waheshimiwa Madiwani baada ya kumaliza kipindi cha miaka mitano kisheria ni asilimia hamsini na tano (55%) ya posho ya Diwani kwa kipindi alichotumikia.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:**Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo hayana ubishi, nina swali mmoja la nyongeza.

Kwa kuwa Bunge hili linategemea kumaliza muda wake katika Bunge la Bajeti tarehe 23 Julai, 2010. Je, hayo Mabaraza ya Madiwani yatavunjwa lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hapa nadhani niende kwenye historia inaonesha nini kwa sababu anauliza kwamba ni lini na wewe nimekusikia hapa huenda ikawa kwenye tarehe 22 Julai, 2010 unategemea kwamba Bunge litakuwa limemaliza shughuli zake na kwamba lini Bunge linavunjwa hilo linategemeana na Rais mwenyewe atakapoamua, kwa sababu halivunjwi hapa linaweza likavunjwa tukiwa hukohuko tuliko.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha kwamba kuna uhusiano kati ya kuvunjwa kwa Bunge na kuvunjwa kwa Halmashauri na kwa sababu sina jibu kamili hapa mwezi wa saba mpaka wa nane katika kipindi hicho kwa kawaida unategemea na Halmashauri nazo zitakuwa zimeondoka kwa sababu na Mbunge kule ambaye ni Mjumbe katika Baraza la Madiwani hayupo tena wakati huo.

Mheshimiwa Spika nadhani kwenye kipindi hicho ndipo nategemea kwamba na mabaraza haya yatakuwa yamemaliza shughuli zake.

Na. 117

**Mpango wa TASAF Wilayani Ngara**

**MHE. PROF. FEETHAM FILIPO BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Ngara ilipata fedha kwa ajili ya Miradi ya vijijji chini ya mpango wa *TASAF* Awali ya kwanza (*TASAF* – 1,2002 – 2005) na kwa kuwa matumizi ya fedha hizo yalilalamikiwa sana na wananchi pamoja na Madiwani kutokubaliana na jinsi fedha hizo zilivyotumika.

(a) Je, ni vijiji vipi na kila kimoja kilipata kiasi gani cha fedha katika utekelezaji wa miradi ya *TASAF* Awamu ya kwanza 2002-2006?

(b) Je, baada ya Mradi wa *TASAF* kukamilika, ni miradi ipi haikukamilka kutokana na ufujaji wa fedha za mradi?

(c) Je, ni hatua gani za pamoja za *TASAF* na Wilaya ya Ngara zilizochukuliwa kukamilisha miradi hiyo na kuwawajibisha wahusika wa ubadhilifu wa fedha hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feetham Filipoi Banyikwa, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *TASAF* katika Awamu ya kwanza (kuanzia 2002 hadi 2005) ilifadhili jumla ya miradi 350 katika vijiji 31 vya wilaya ya Ngara. Miradi hiyo ilikuwa na thamani ya shilingi 686,844,352.00.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa Awamu ya kwanza ya *TASAF* katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, hakuna mradi ambao haukukamilika kutokana na ufujaji wa fedha. Miradi ambaya haikukamilika ilisababishwa na (i) Kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi ambayo ilimalizika Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mradi. (ii) Jamii kutotimiza mchango wake kama ilivyo katika mkataba wa kutekeleza mradi.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la kutokamilika kwa baadhi ya mradi ya *TASAF* katika Awamu ya kwanza, haikuwa tatizo la Halmashauri ya Wilaya ya Ngara pekee.

Tatizo hili lilizikumba Halmashauri nyingi za Tanzania. *TASAF* iliorodhesha miradi yote ambayo haikukamilika katika Awamu ya kwanza na kuwaandikia

Wakurugenzi wa Halmashauri hizo na kuwaomba kuchangia kwa kupitia vyanzo vyake vya mapato ili miradi hiyo ikamilike na jamii ziweze kupata huduma walizoomba. Pamoja na ombi hilo, kuna Halmashauri ambazo hazikuweza kutoa fedha za kukamilisha miradi hiyo.

Katika awamu ya pili ya *TASAF*, Halmashauri zilizokuwa na miradi ambayo haikukamilika katika awamu ya kwanza walishauriwa kuiingiza mradi hiyo katika maombi mapya ya miradi ya awamu ya pili ili kuikamilisha. Hayo yalifanyika na miradi ilipatiwa fedha za kuikamilisha. Hayo yalifanyika na miradi ilipatiwa fedha za kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu ilimpatia Mheshimiwa Mbunge taarifa za kina kuhusu miradi iliyofadhiliwa na *TASAF* katika Wilaya ya Ngara na jumla ya fedha zilizotolewa kwa kila mradi uliotekelezwa katika kipindi hicho kwa kila kijiji.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA**: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Waziri ameyatoa. Lakini naomba niseme kwamba kumetokea mabadiliko makubwa sana katika Halmashauri ya Ngara kutokana na matumizi mabovu ya pesa za *TASAF* awamu ya kwanza. Labda niishukuru Serikali kwa kuona hilo na kufanya mabadiliko makubwa. Mkurugenzi amebadilishwa, Wakuu wote wa Idara wamebadilishwa na hiyo ni kutokana na matumizi mabovu ya pesa za Serikali.

**SPIKA:** Kwa kuwa hakuna swali kuna taarifa tu. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo ni la Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi.

Na. 118

**Kuchelewa kwa Mishahara na Posho za Walimu**

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa mishahara na posho za walimu wakati mwingine huchelewa sana kuwafikia walengwa hadi kufikia miezi sita:-

Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo inawakatisha tamaa walimu hawa na inachukua hatua kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mishahara ya walimu imekuwa ikichelewa hii ilitokana na mchakato mrefu uliokuwepo wa kuwaingiza walimu wapya kwenye orodha ya walipwa mishahara na Serikali.

Aidha, tatizo hili limekuwa likijitokeza iwapo taarifa za mwajiriwa hazikujazwa kwa usahihi kwenye fomu ya kudhibiti ajira na kuwasilishwa mapema kwa mamlaka husika. Pia tatizo limekuwa likijitokeza pale ambao mwalimu anaomba kubadili kituo wakati mshahara wake umeshaelekezwa na unalipwa kwenye kituo chake cha awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaweka utaratibu mpya ambapo mishahara na posho za walimu hutumwa kwenye vituo kabla ya walimu walengwa kuripoti. Hivyo mwalimu anapata posho yake na mishahara wake mapema kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Aidha Serikali inatoa wito kwa walimu wote kuripoti kwenye vituo walivyopangwa ili kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa posho na mishahara yao.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Anasema kuwa tatizo hili la kuchelewesha mishahara linajitokeza pale ambapo taarifa za mwajiriwa hazikujazwa kwa usahihi. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuzijaza fomu hizi hukohuko chuoni, kabla ya mwanafunzi hajamaliza masomo yake ili kupata muda wa kufanya marekebisho pale ambapo mwajiriwa amekosea kujaza ndani ya fomu hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ninayofuraha kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba utratibu huo hufanyika vyuoni kila inapokaribia musimu wa wanafunzi wale kuhitimu. Maafisa utumishi kutoka Wizara ya Elimu na TAMISEMI husambazwa kwenye vyuo vyote kwa ajili ya kuwapa muelekezo wa kujaza zile fomu. Hata hivyo tatizo kubwa linalosababisha mishahara kuchelewa baadhi ya walimu waliopangwa huchelewa sana sana kuripoti kwenye vituo vyao na kwa wakati mwingine pale wanapokwenda kwenye vituo vya awali wanakuta mishahara imesharudishwa Hazina.

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la mishahara lipo hata kwa walimu walioajiriwa kwa njia ya mkataba; kwa kuwa walimu wa nane wa Singida Mjini mpaka sasa wanadai mishahara ya zaidi ya miezi 15 na kwa kuwa tatizo hilo nilishalifikisha mpaka hapa Bungeni na Serikali ikaahidi kushughulikia tatizo hilo. Lakini mpaka sasa hivi ni mwalimu mmoja tu kati ya walimu nane ambao wanadai wameshalipwa. Je, ni lini sasa hao walimu saba waliobaki watalipwa pesa zao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, tatizo la walimu wastaafu ambao hufanya kazi kwa mkataba tumelifanyia kazi kwa kadri tulivyoweza na Mheshimiwa Diana Chilolo ameshawasilisha kwangu mara kadhaa. Mishahara ya walimu wastaafu wanaofanya kazi kwa mkataba ipo kwenye Halmashauri wanazofanyia kazi. Kwa sababu walishamaliza muda wao wa utumishi wa umma na wanapokuwa kwa mkataba ni Mkurugenzi wa Halmashauri ndiyo anayepaswa kumlipa mshahara wake baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Naomba nitoe rai kwamba Wakurugenzi wote ambao wanao walimu wa aina hii tafadhali tunawaomba muwapatie mishahara yao endapo itathibitika kwamba wametimiza wajibu unaostahili.

Na. 119

### Waliomaliza Kidato nne 2006/2007 Kukosa nafasi za Ualimu

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wanafunzi wanaofuzu Kidato cha nne hupata alama nzuri zinazotolesheleza kujiunga na kozi mbalimbali ikiwemo ya ualimu daraja la IIIA; na kwa kuwa, baadhi yao hukosa nafasi hizo na hivyo kuomba miaka inayofuata ambapo wengi hufanikiwa kupata:-

Je, Serikali haioni kuwa imeleta kero kubwa kwa mwaka huu 2009 kuwaacha wale waliomaliza miaka iliyotangulia wakiweno wa mwaka 2006 na 2007?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA MUGOSI KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Spika, kimsingi utaratibu wa waombaji kuingia mafunzo ya ualimu ni wa ushindani. Vijana wenye sifa stahili ni wengi na inabidi kuweka utaratibu wa kupata wale wanaotimiza vigezo muhimu. Vigezo hivyo ni pamoja na:-

(a) Mwombaji awe amehitimu mwaka huo wa masomo ili kupata mapendekezo ya wakuu wa shule kupitia *selforms* kama anafaa kuwa mwalimu.

(b) Kipaumbele kwa sasa ni kwa masomo yenye uhaba wa walimu. Masomo hayo ni pamoja na hisabati, sayansi na kiingereza.

Mheshimiwa Spika, vijana wenye sifa na waliohitimu kidato cha Nne kati ya 2006 na 2008 jumla yao ni 41,860. Kati ya hawa, waombaji waliohitimu mwaka 2008 na wenye sifa ni 15,489. Idadi hii ni kubwa ukilinganishwa na nafasi za mafunzo ya

ualimu. Nafasi za mafunzo ya ualimu zilikuwa 5,000 na hivyo ilikuwa vigumu kuwapa nafasi waombaji wote hivyo kipaumbele kilitolewa kwa wahitimu wa mwaka 2008 ambao walijaza maombi ya ualimu kupitia *selforms*. Aidha, uzoefu unaonesha kwamba kuna baadhi ya waombaji wanaotumia vyeti vya watu wengine waliomaliza miaka ya nyuma ambao tayari wameshavitumia kwa mafunzo ya ualimu na wengine kutumia vyeti vya kugushi. Hivyo ili kuziba mianya ya kutumia vyeti vya namna hiyo kipaumbele kitaendelea kutolewa kwa waliomaliza kidato cha nne miaka ya hivi karibuni.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Utaratibu wa kujaza *Selforms* kwanza si wa zamani, umeanza nadhani mwaka 2007/2008. Kwa hali hiyo, wapo wengi waliomaliza miaka ya nyuma kabla ya utaratibu wa kujaza fomu hizi. Naishauri na kuiomba Serikali kwa maswali yafuatayo na kwa sababu mahitaji yetu ni makubwa mno kwa nini Serikali haifanyi yafuatayo:-

(i) Ikajenga mabweni ili wale wanafunzi wanaoonekana wanasifa lakini wanakosa nafasi wakasoma vyuoni kwa kutoka nje wakawa wanafunzi wa vyuo lakini wakiwa wanalala nje?

(ii) Kwa wale ambao wana sifa kwanini wasifikiriwe kwa mwaka mwingine kwa kucheki kuhakikisha kwamba hakuna hiyo tabia za kugushi na wanaogushi wote wakachukuliwa hatua ili kukomesha tabia ya kutumia vyetu vya watu wengine.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA MUGOSI KABAKA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tulishajaribu utaratibu huu wa wanachuo kulala majumbani na kuja kuhudhuria masomo baada ya kuona mahitaji ya walimu ni makubwa sana. Lakini utaratibu huu ulituletea matatizo kwa sababu tatizo si bweni lakini pia ni vyumba vya kusomea. Tukaona kwamba tunaongeza idadi mahali ambapo hatuna miundombinu ya kutosha katika vyuo. Lakini pia hatukuwa na wakufunzi wa kutosha kwa wanafunzi wote hawa waliokuwa wanahitaji ualimu. Kwa hiyo tukarudi kwenye utaratibu wetu ule wa kawaida kwamba wanachuo lazima waje wakae mabwenini. Kwa suala la kughushi ni kwamba Watanzania ni wajanja sana. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kuchukua vyeti kwa wale waliomaliza nyuma kwa sababu wanajaribu na wenyewe kutuzunguka kwa kutumia vyeti vya kughushi kwa namna yoyote ile na tumeshagundua tuna lundo la vyeti vya namna hii katika vyuo katika Wizara kwa hiyo kwa kweli tutaendelea kuchukua wale wanaomaliza kwa kipindi hicho na wale wanaojaza *selform*. Lakini bado tunamwanya wale wanaoleta maombi mmoja mmoja na tumewachukua wengi sana na nyie Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tumejaribu kuchukua vijana ambao wamemaliza baada ya kupeleka vyeti vyo Baraza la Mitihani na kuvihakiki kwamba kweli ni vyeti halisi.

Na. 120

**Matumizi ya Fedha za Uwezeshaji Mikoani**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

(a) Je, ni fedha kiasi gani za uwezeshaji Mikoani maarufu kama Mabilioni ya Rais Kikwete zimewafikia wananchi walioko vijijini katika Jimbo la Magu, ikitajwa idadi na kwa kila Kata?

(b) Je, kwa nini wakulimwa wasikopeshwe majembe ya kukokotwa na ng'ombe kutokana na fedha hizi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Magu imeishapata mikopo yenye thamani ya shilingi 309,979,662/= ikiwa ni zaidi ya kiwango kilichotengwa na Serikali cha shilingi milioni 200 kwa kila Wilaya. Jumla ya shilingi 58,567,776/= zimetolewa kwa wajasiriamali mmoja mmoja kupitia benki ya NMB na walionufaika ni wajasiriamali wapatao 63 wakiwemo wanaume 41 na wanawake 22. Kwa upande wa Benki ya *CRDB,* jumla ya shilingi 262,723,000/= zimetolewa kwa *SACCOS* mbili za Chawaki shilingi 251,363,000/= na Ntuzu shilingi 11,360,000/= ambazo zimewanufaisha wajasiriamali wapatao 131 (wanawake 19 na wanaume 112).

Kati ya fedha hizo za *CRDB,* Tsh. 27,885,000/= zilitolewa kwenye awamu ya pili. Hata hivyo, inawezekana wananchi wengi waishio vijijini katika Wilaya ya Magu walikosa mikopo hiyo kutokana na benki za *CRDB* na zilizoshiriki katika awamu ya kwanza kutokuwa na matawi ya kutoa huduma za mikopo vijijini sawa na maeneo mengine vijijini yaliyokosa mikopo hiyo Tanzania Bara.

Kwa bahati mbaya, kwa sasa mchanganuo wa mgao Kata kwa Kata hatujaweza kupata, lakini namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tutampatia mgawanyo huo mara uchambuzi ukikamilika.

Mheshimiwa wa Spika, kwa kuwa mpango huu ni endelevu, Serikali itahakikisha wananchi walioko vijijini wanafaidika na huduma za mikopo kupitia benki na asasi za fedha zilizo na mtandao wa kutoa huduma za kibenki vijijini kwa utaratibu unaoendelea kutumika kwenye awamu ya pili.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu uliotumika katika utekelezaji wa mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira nchini ilikuwa ni kutoa mikopo ya fedha kwa wananchi wa kawaida hasa wakulima ili kuwajengea uwezo na uzoefu wa kuweka akiba na kukopa kwa mtu mmoja mmoja kupitia vikundi na *SACCOS.*

Kwa kuwa utaratibu umekuwa wa benki au asasi kukopesha fedha kwa wajasiriamali mmoja mmoja au kupitia *SACCOS,* ni jukumu la mjasiriamali mwenyewe kuwa na nidhamu ya kununua majembe au pembejeo nyingine anazohitaji kwa kilimo

chake au *SACCOSS* kuweka utaratibu wa kununua vifaa hivyo na kukopesha wanachama wake badala ya kuzitaka benki zikopeshe pembejeo badala ya fedha kitu ambacho si kazi yao.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ulipoanzishwa na Serikali mkazo ulikuwa kwamba wananchi wajiunge ama waanzishe SACCOS, na wananchi wa Jimbo la Magu walihamasishwa, wakaanzisha, wakajiunga kwenye *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, sasa, napongeza sana Serikali kwa kupeleka hizi milioni 300, lakini zimetolewa katika Kata moja tu. Je, wananchi wa Tarafa zingine na Kata zingine wasubiri hadi lini na hivi sasa ni miaka mitano imepita?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wananchi wengi wa vijijini ni wakulimwa, kwa nini Serikali isitoe maelekezo kwamba sasa watakaokopeshwa huko vijini, wakopeshwe majembe ya kukokotwa na ng'ombe badala ya fedha taslimu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wenzetu wa benki ya *NMB* na *CRDB* ambao walitumika katika awamu ya kwanza katika taratibu zao za kukopesha hawakuzingatia sana *SACCOS* hii inatoka Kata gani katika Wilaya husika, badala yake waliangalia vile vigezo vinavyokidhi matakwa yao ya kuweza kukopesha *SACCOS* husika. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kwa kweli unakuta kwamba *SACCOS* zingine hazikukidhi vigezo au zilichelewa kupeleka maombi na kwa namna hiyo utakuta maeneo mengi, *SACCOS* ambazo ziko kwenye Kata moja au maeneo ya mjini tu ndiyo walifaidika, lakini tumesema kwamba baada ya kuona kasoro hizo ndiyo maana awamu ya pili tukaweka utaratibu wa kutumia asasi zingine za kifedha zenye mtandao wa kwenda vijijini ili na wengine waliokosa katika awamu ya kwanza waweze kufaidika.

Lakini, nakubali kwamba bado hata kwenye awamu hizi mbili haitowezekana kufikisha mikopo hiyo katika maeneo yote ya vijijini, kwanza kwa sababu fedha zile sasa zitakuwa zimekamilika na kwa maana ya Magu, wameishapata milioni 300 ambayo ni zaidi ya ile avarage ya milioni 200.

Tunachotaka kusema ni kwamba, kwa sababu hizi hela ni revolving, baadae tutakapoanza awamu nyingine, na kama nilivyosema hivi karibuni sasa hivi tunajaribu kutathmini jinsi ambavyo mikopo hii ilivyokwenda kwa wananchi mpaka chini, tuone kasoro zilizopo ili baadae, ikimfurahisha Mheshimiwa Rais, kutoa tena mabilioni mengine ya kwake, tuweze kuwa na utaratibu mzuri zaidi wa kufikisha fedha hizi kwa wajasiriamali na zile *SACCOS* ambazo ziko maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, nadhani Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kwamba utaratibu ambao unatumika kukopesha vifaa kama hivyo, benki hizi za kawaida hazifanyi. Ingekuwa tumetumia zile *banking* zinazokopesha vifaa au *Leasing companies*, ingekuwa na ni sahihi.

Lakini, hizi benki tulizozitumia kwa kweli zimetumia utaratibu wao wa kutoa fedha. Sasa, kwa kweli ni nidhamu ya mkulima mwenyewe kuangalia kwamba nikishapata ile fedha, ninunue pembejeo ninayohitaji, na kwa kweli ndiyo nia ya Serikali wanunulie pembejeo, wanunulie vifaa waweze kufanya kilimo chao. Lakini, ombi lake ni zuri, tutaangalia katika awamu zijazo, tutumie njia gani ili wakulima ambao tunadhani wanaweza kuwa na nidhamu, tuwakopeshe kabisa vifaa hivyo ama kwa kutumia benki hizo hizo au kwa utaratibu mwingine tutakaouona unafaa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na sintofahamu kubwa sana kuhusu mabilioni haya ya JK; na kwa kuwa inaoenekana dhahiri kwamba fedha hizi inaonekana zimetolewa kwa upendeleo. Kwa kuwa majimbo mengi eneo la Pemba pesa hizi hazijaonekana hasa katika Jimbo langu la Mkanyageni.

Je, Waziri yuko tayari sasa kuonyesha kila Jimbo limepata fedha gani na tukaweza kupata kabla ya Mkutano wa Bunge hili kumalizika ili tujue kila Jimbo limepata kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme hakuna sintofahamu kubwa. Kilichotokea kwa kweli sana sana ni kwamba wajasiriamali wengi walioko vijijini walikosa kutokana na sababu nilizozieleza mwanzoni. Lakini, ombi lake kwamba kila Jimbo tuone mchanganuo, inaweza ikapatikana.

Lakini kwa haraka tunachoweza kufanya ni kwa kila Wilaya, kila Wilaya ilipata kiasi gani, hilo tunaweza tukafanya, lakini Wabunge watusaidie waende huko Wilayani kwao waangalie sasa hizo fedha tulizotaja kwamba ni kwa ajili ya Chakechake kwa mfano, zimekwenda kwenye majimbo yapi.

Hiyo inawezekana kwa kufanya sasa utaratibu wa kule kule kwenye Wilaya husika. Ila kama tukipewa muda mrefu, tunaweza tukawataka wakaleta na haitakuwa Bunge hili. Lakini kwa maana ya Bunge hili, tunaweza Wilaya kwa Wilaya.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya viongozi ambao wanasimamia fedha hizi, huwapatia kwa upendeleo watu wao wa karibu kama ndugu, rafiki, wapenzi ambao hawana sifa ya kupewa fedha hizi na kuwaacha wanawake ama vijana au watu ambao wana sifa za kupata fedha hizi ambao wanafanya biashara.

Je, Serikali inalijua hilo? Na kama inalijua inalichukulia hatua gani ili kukomesha tatbia hii mbaya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuruhusu umeuliza mawili; kulijua na hatua zipi! Lakini, nadhani yanaungana. Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwamba kulikuwa na upendeleo wa benki kutoa fedha, hatuna taarifa hiyo kwa sababu ninachoamini ni kwamba benki wanafuata taratibu zao, nani ana vigezo vile vinavyowezesha wao kama ni *SACCOS* ama ni mmoja mmoja kupewa fedha zile. Lakini, kasoro kama nilivyosema sina sababu za kuzirudia, zilikuwepo kwa maana kwamba kwa utaratibu ule wengi hawakufikiwa.

Lakini kwamba kuna upendeleo sina hakika. Lakini kama anao ushahidi fulani ambao unaonyesha kwamba benki hizi zilitoa fedha hizi kwa upendeleo, basi tunaweza tukafuatilia tukachukua hatua zinazostahili.

**SPIKA:** Kwa hiyo, una maana akufuate kukupa hizo tarifa? Basi, ungemalizia Mheshimiwa! *(Kicheko)*

Na. 121

**Serikali Kuajiri Mhandisi wa Maji Mji Mdogo wa Shelui**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji Mdogo wa Shelui unayo maji ya kutosha ambayo yanasambazwa kwa njia ya mabomba; na kwa kuwa hakuna kitengo cha Uhandisi wa Maji kwa ajili ya kutoa huduma ya kuunganisha mabomba ya maji kwenye nyumba za wakazi wa Shelui?

Je, ni lini Serikali itaajiri Mhandisi wa Maji atakayetoa huduma endelevu katika Mji Mdogo wa Shelui ili wakazi wake waondokane na adha ya kusubiri Mhandisi wa Maji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ambaye hufika mara chache sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Shelui (Nselembwe) ni kijiji kati ya vijiji tisa vilivyojengewa miradi ya maji katika awamu ya kwanza ya programu ya maji vijijini. Mradi huu ulianza

kujengwa mwaka 2005/2006 na kukamilika katika mwaka wa 2007/2008 ukiwa na visima viwili vyenye uwezo wa kuzalisha lita 30,000 kwa saa na mtandao wa mabomba wa mita 19,345. Aidha, jumla ya vituo 26 na malambo mawili yalijengwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria Na. 12 ya Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009, kifungu cha 31 inatoa madaraka ya kuanzishwa kwa vyombo vya kuendesha miradi ya maji. Aidha, majukumu ya vyombo hivyo yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 32 cha sheria hiyo ni pamoja na kumiliki mali za mradi, kusimamia, kuendesha, kutunza miundombinu ya maji, kufanya matengenezo, kutunga sheria ndogo za uendeshaji pamoja na kutoza ada ya matumizi ya maji. Jukumu la Halmashauri za Wilaya ni kujenga uwezo wa kumudu matengenezo ya miradi inayojengwa.

Mheshimiwa Spika, maradi wa maji wa Shelui una Jumuiya ya watumiaji wa maji yenye vikundi 26 vya watumiaji maji ambavyo vilipewa mafunzo na taratibu zote za kuendesha mradi wa maji. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba imebaki na jukumu la kuratibu, kutoa ushauri, kusimamia na kutoa mwongozo kuhusu shughuli za uendeshaji wa mradi wa mradi.

Aidha, inapotokea tatizo linalohitaji utalaam, Ofisi ya Mhandisi wa Maji wa Wilaya ina jukumu la kutoa utalaam huo na imekuwa ikifanya hivyo mara kwa mara. Wizara yangu itaendelea kutoa ushauri wa kitalaam kila utakapohitajika.

Mheshimiwa Spika, suala la kuajiri Mhandisi Maji wa Mradi wa Shelui kwa sasa halijafanyika na uwezo wa kulitekeleza katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya bado ni mdogo kwa vile hata kwenye ngazi ya ya Wilaya bado kuna mahitaji ya Mhandisi ambaye pamoja na kibali cha kumwajiri kutolewa hajapatikana na uhaba wa Wahandisi wa fani hizi nchini. Wakati Serikali inafanya juhudi za kuajiri, tayari utaratibu umekwishaandaliwa wa kuwapanga Fundi Sanifu walioko Wilayani kulea miradi yote iliyojengwa ukiwemo ule wa Shelui, Mradi huo una Fundi Sanifu Mlezi mwenye uwezo wa kutoa ushauri wa kitalaam na kiufundi pale inapojitokeza.

Wizara inatambua umuhimu wa kuwa na Wahandisi wa Maji wa kutosha kwa kuzingatia Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na umuhimu wa kuwa na Wahandisi katika ngazi ya kijiji na mji na juhudi zinaendelea kufanywa ili hatimaye kila Halmashauri ipate Wahandisi wa Maji.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa ni kweli wananchi wa Mji Mdogo wa Shelui bado wanatumia maji kupitia vituo ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameviainisha; na kwa kuwa Mji Mdogo wa Shelui unakua kila siku, wananchi wengi wamejenga nyumba za kisasa ambao zinatumia maji katia vyoo vya kuvuta ndani ya nyumba zao; na kwa kuwa kuna Fundi Sanifu ambaye ni Mlezi wa Mji huo Mdogo wa Shelui. Je, ni huyu Fundi Sanifu ataruhusiwa kuwaingizia maji wananchi wa Shelui ambao wanataka sasa kuingiza maji kwenye nyumba zao ili waweze kwenda na wakati? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, suala analoliuliza la kuingiza maji katika nyumba zao ni suala zuri na ninaamini ni kwa sababu Mheshimiwa Chilolo mwenyewe alishiriki sana wakati wa kuanzisha Mradi huu hasa tulipoanza Mradi ule wa Miradi 14 iliyoanzisha mradi uliopelekea Mradi huu mkubwa wa vijiji kumi. Kwa hiyo, naamini analifahamu na ndio maana anafuatilia sana. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Chilolo kwamba taratibu hizi sasa, Sheria za Maji Na.11 na Na. 12 ambazo tumezipitisha mwaka uliopita zinazipa mamlaka Halmashauri katika ngazi ile kusimamia taratibu kama nilivyosoma katika majibu yangu ya msingi. Kwa hiyo, ninachoweza kumshauri na kumhakikishia Mheshimiwa Chilolo ni kama alivyofanya awali wakati akitetea mradi huu ukianzishwa, tutafanya hivyo hivyo, tutaangalia, tutashirikiana na Halmashauri kuona ni vipi tunaweza kuhakikisha kwamba wananchi nao wanaunganisha maji kutoka kwenye maeneo ya machoteo hata wale wanaoweza wakaingiza katika nyumba zao. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mradi huu wa Selembwe – Shelui ni mkubwa sana na kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri una uwezo wa kutoa lita 30,000 kwa sasa; na kwa kuwa kuna kijiji cha jirani cha Kizonzo ambacho kina shida sana ya maji, hususan kitongoji cha Msansao. Je, Wizara iko tayari kuweza kusogeza Mradi wa Selembwe ili usogee Msansao kama walivyofanya Kibigili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu ya swali la msingi, basi tutashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuangalia uwezekano wa kusogezo maji hayo kutoka kijiji hicho cha Selembwe kwenda Msansao, ni utaratibu tu. Namwomba Mheshimiwa Killimbah kama anavyofanya siku zote na mwenzake Mheshimiwa Diana Chilolo, tushirikiane kuhakikisha maji hayo yanakwenda. *(Makofi)*

Na. 122

**Maji ya Chemchem, Mito na Mifereji kutumika kwenye Mabomba-Rombo**

**MHE. BASIL B. MRAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, huko Wilayani Rombo maji ya chemchem, Mito na Mifereji yamekwishatumika kwa kuingizwa kwenye mabomba yaliyopo na hivyo kuilazimisha Serikali kuchunguza vyanzo vipya:-

(a) Je, Utafiti huo umefikia wapi na ni lini maji hayo yataanza kutumika?

(b) Kama utafiti umeonesha kukosa maji ya kutosha. Je, Serikali iko tayari kuomba Serikali ya Kenya ituruhusu kutumia maji yaliyopo mpakani upande wao ambayo chanzo chake ni Mlima Kilimanjaro?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Basil Mramba, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rombo inapata sehemu kubwa ya maji kwa matumizi ya nyumbani kutoka katika chemchem zilizoko Marangu katika Wilaya ya Moshi. Wilaya ya Rombo ina wakazi takribani 240,000 ambao mahitaji yao ya maji ni meta za ujazo 20,000 kwa siku zikilinganishwa na uzalishaji wa meta za ujazo 15,000 tu kwa siku. Ni kweli kwamba, vyanzo vya maji ikiwemo mito na chemchem zilizopo katika Wilaya ya Rombo zimekwishatumika lakini vyanzo hivyo peke yake havitoshi kukidhi mahitaji ya watu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Basil Mramba, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kutafuta vyanzo vingine vitakavyoweza kuongeza wingi wa maji. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, ambaye naye ametoa ushirikiano mkubwa sana kwa Serikali kwa kumtoa Katibu wake ashirikiane na Wataalam kutoka Ofisi ya Bonde la Mto Pangani, kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi. Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji (WSDP) imefanya uchunguzi wa Kihaidrolojia na kijiofizikia ili kubaini maeneo yanayofaa kuchimba visima virefu vya maji. Kati ya maeneo 27 yaliyochunguzwa maeneo 15 yamebainika kuwa na maji chini ya ardhi.

Maeneo hayo yapo katika Vijiji vya Kidondoni, Marangu, Shoshoro, Kiarema, Kibaoni Mkwini, Keramfua na Najarareru, mchakato wa kumpata Mkandarasi wa kuchimba visima hivyo 15 umeanza na matarajio yetu ni kukamilisha uchimbaji ifikapo mwezi Septemba, 2010.

(b) Mheshimiwa Spika, nasita kukubaliana moja kwa moja na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iombe maji kutoka upande wa nchi ya Kenya kwa sababu bado tutaendelea kufanya uchunguzi wa vyanzo vingine ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunachofanya ni kuangalia uwezekano wa kuwa na usimamizi wa pamoja na nchi jirani ya Kenya katika matumizi na usimamizi wa maji shirikishi ya Maziwa Chala na Jipe na Mto Umba. Jambo hili linawezekana ukizingatia kwamba, tukikubaliana tunaweza kuunda chombo cha usimamizi wa maji shirikishi chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kenya tayari wanao mpango wa kutumia maji ya Ziwa Chala kupitia *Capital Development Authority (CDA)* lakini ni ya kule Kenya, lakini hawawezi kutumia maji hayo shirikishi mpaka tukubaliane. Kwa upande wa Tanzania, mpango kama huo wa Kenya utakamilika baadaye mwaka huu baada ya kukamilisha tathmini ya kina, ya wingi, ubora na mahitaji ya maji katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro, Ziwa Chala na Ziwa Jipe. Aidha, tathmini hiyo itawahusisha pia majirani zetu wa Kenya

*(CDA) Athi River Authority* na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ya Kenya. Hatua itakayofuata baada ya tathmini hiyo ni kufanya majadiliano na Kenya juu ya ushirkiano katika matumizi ya Ziwa Chala.

**MHE. BASIL B. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika**,** kwanza nitoe shukrani za dhati kwa Serikali ya Tanzania, Serikali ya Ujerumani, *Kili Water,* Halmashauri ya Rombo na *NGOs* mbalimbali ambazo kwa miaka thelathini (30) sasa zimekuwa zikishughulikia matatizo ya maji kule Rombo.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza; kwa kuwa maji ni siasa na kwa kuwa eneo ninalozungumzia ni kubwa takribani kilomita 50 zenye watu ambao wanahaha mara kwa mara kutafuta maji hasa wakati wa kiangazi; na kwa kuwa mazungumzo haya na Kenya yamechukua muda mrefu, zaidi ya miaka mitano (5).

Je, Serikali haioni kwamba, kwenye eneo hili sera ya kasi mpya ndiyo ingetuletea jawabu mapema na kumaliza tatizo hili, na kuondoa siasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mramba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mazungumzo na Serikali ya Kenya na wenzetu hususani katika ushirikiano wa maji yamechukua muda mrefu, lakini kama nilivyowaeleza hata ushirikiano wa Afrika Mashariki wenyewe unachukua muda mrefu mpaka tunapofikia maandalizi kamili.

Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na tayari nimemweleza kwamba, tumeishafanya utafiti sisi wenyewe na yeye mwenyewe ametoa Katibu wake na katika visima 27, visima 15 tayari vimethibitika kwamba, vitatoa maji na sisi wenyewe kama Serikali nakumbuka mwaka 1989 tulifanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi kule Rombo katika mradi ulioitwa *Lower Rombo, Lower* Hai na taarifa zile tunazo, na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutatumia taarifa hizo tulizonazo na uchunguzi wetu chini ya *WSDP* kuendelea kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata maji wakati hizi taratibu nyingine za mashirikiano zinaendelea.

Na. 123

**Mfumo wa Vocha kwa Matumizi ya Ruzuku ya Mbolea na Mbegu**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mfumo mpya wa vocha kwa matumizi ya ruzuku ya pembejeo ya mbolea na mbegu unaonekana kwa namna fulani kuwa ukisimamiwa vizuri unaweza kusaidia kuboresha kilimo; na kwa kuwa, mfumo huu ulichelewa sana kuanza katika msimu huu na kusababisha wakulima wengi kutopata mahitaji hayo muhimu kwa wakati:-

(a) Je, Serikali imebaini kasoro ngapi za mfumo huo toka uanze kufanyiwa majaribio ya utekelezaji?

(b) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza?

(c) Je, Serikali iko tayari kufuata agizo la MLALE Mkoa wa Ruvuma ili kufanikisha mfumo mzima wa pembejeo na kilimo Mkoa wa Ruvuma?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a), (b) na ( c ) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mfumo huu wa vocha Serikali ilibaini kasoro nyingi zikiwemo zifuatazo; vocha kuchelewa, bei ya mbolea kuendelea kuwa juu,kutokubalika kwa mbolea ya Minjingu, kutoeleweka vyema kwa utaratibu wa vocha, uchache wa maafisa ugani na usimamizi duni hususani katika ngazi ya Wilaya na Vijiji.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hizo Wizara imefanya yafuatayo; Vocha zimesambazwa mapema kulingana na msimu wa kilimo, elimu ya vocha na faida ya mbolea ya Minjingu kwa wadau mbalimbali imetolewa, na kigezo cha mkulima atakayenufaika kuwa ni mwenye uwezo wa kuchangia tofauti ya bei.

Pia Serikali imepeleka vijana 1,998 wa cheti na *diploma* kutoka vyuo mbalimbali vya kilimo kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo kusimamia na kutoa maelekezo ya kitaalam kwa wakulima.

(c) Mheshimiwa Spika, agizo la MLALE la Mkoa wa Ruvuma toleo la mwaka 1987 liliweka mkazo wa kuwasaidia wakulima wadogo kwa kutambua kwamba, asilimia 97 ya wakulima wa Mkoa wa Ruvuma ni wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, msisitizo mkubwa uko katika kuhakikisha mambo yafuatayo yanafanyika; pembejeo na zana za kilimo ziwepo karibu na mkulima kwa wakati na za kutosha, kutengeneza na kuimarisha barabara za vijijini (*feeder roads*), kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, kuwa na watumishi wa kutosha wa ugani, kuwepo na uhakika wa masoko ya mazao wanayozalisha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mpango wake wa kuendeleza sekta ya kilimo (ASDP) imeweka utaratibu wa kuanisha shughuli zote za kilimo katika Halmashauri na mipango yote inaingizwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)*.

Pamoja na hayo, Serikali Kuu inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kuhakikisha kwamba, mipango iliyopangwa inatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia Kilimo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo kwa kuwa; zoezi hili la vocha kwa kweli limeonesha mafanikio makubwa lakini pamoja na mafanikio hayo yote msimu huu wa kilimo zoezi hilo limeingiliwa na kasoro nyingine kubwa ya mbolea ya kukuzia ya *Urea* kugawiwa kwa wakulima mfuko mmoja badala ya mifuko miwili kwa ile ekari ya kitaalam.

Je, ni nini tamko la Serikali katika kurekebisha kasoro hiyo ambayo inaweza kupunguza tija ya uzalishaji badala ya kuifanya tija hiyo iwe njema kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, suala hili la vocha linahusu kabisa pembejeo kwa maana ya mbegu, mbolea na masuala mengine ya madawa na kadhalika na kwa kuwa mwaka huu wakulima wamepata tatizo kubwa sana la mbegu na hivyo pia kuongeza kasoro nyingine kubwa ya uzalishaji katika suala zima la mfumo wa vocha.

Je, Serikali sasa ipo tayari kutoa kipaumbele katika maeneo yale ambayo yamejipanga kuzalisha mbegu kama kule Mlale JKT katika jimbo la Peramiho na maeneo mengine ambayo yako tayari kuzalisha mbegu nchini badala ya kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI , KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza kwamba mbolea ya *Urea* ilitolewa kiasi kidogo. Labda nimueleweshe kwamba kitaalamu mfuko mmoja umeshafanyiwa utafiti na ikaonekana kwamba kitaalamu kuwa unatosha kwa eneo hilo la ekari moja kwasababu kwa kuweka mifuko miwili gharama inakuwa ni kubwa lakini mazao atatakayopata yanakaribia na yale ya mifuko miwili, kwa hiyo katika uchumi wa Kilimo kuna kitu kinaitwa *law of diminishing returns* unavyozidi kuweka mblolea ndivyo unavyozidi kupata mavuno lakini ukiweka mbolea zaidi inafikia point ambayo ile mbolea inakuwa ni sumu lakini vilevile mkulima anatumia fedha nyingi kununua mbolea wakati uzalishaji unakuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kwamba mbolea ambayo inatutolewa kwa mfuko mmoja inatosha kutokana na vigezo vya kitaalamu na imefanyiwa utafiti. Swali lako la pili kuhusu mbegu ni kwamba matatizo yaliyotokea kule Mbeya na Songea ni kwamba mbegu waliyokuwa wameizoea ilikuwa inatokea Kenya, sasa mbegu iliyozalishwa Tanzania ilivyokwenda kwa wakulima wakaona kwamba kwasababu hawakuizoea wakaona kuwa haifai lakini ukweli ni kuwa mbegu hiyo inafaa, na mbegu iliyokuwa inatoka Kenya kule Kenya kulikuwa na matatizo ya mbegu kwa hiyo walizuiwa kuleta Tanzania kwa hiyo tunaomba kuwasahauri wakulima kwamba waweze kukubali mbegu ambazo zinazalishwa nchini.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Suala la kutumia JKT ni kweli kabisa kuwa mpaka sasa hivi tunatumia JKT pamoja na magereza katika uzalishaji wa mbegu wakisaidiaa na ASA ili tuweze kuhakikisha kwamba tunakuwa na uzalishaji wa mbegu wa kutosha hapa nchini.

**SPIKA:** Nashawishika niruhusu wawili kama maswali ni mafupi Mheshimiwa Arfi na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la kutoa pembejeo kwa vocha lilikuwa lisaidie kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula kadhalika pia na mazao ya biashara. Lakini kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa pembejeo za tumbaku katika maeneo yote yanayolima tumbaku nchini je, dosari hii Wizara imeifahamu na iko tayari sasa kuwalipa fidia wakulima wale ambao wamepata hasara kwa kuchelewa kupata pembejeo za tumbaku?

**NAIBU WAZIRI, KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kilimo cha tumbaku kinalimwa kwa mikataba na kina taratibu zake. Kwanza kuna miezi ambayo wanapanga mipango kwamba makisio ya mwaka huu yatakuwa ni haya nay a pembejeo yanahitajika kiasi hiki sasa makisio yale yanapangwa mwezi wa nne, ununuzi wa mbolea una nunuliwa labda miezi miwili ijayo.

Kwa hiyo kilichofanyika ni kwamba bei ya tumbaku mwaka jana ilikuwa ni nzuri sana kwa hiyo wananchi wakashawishika kulima tumbaku nyingi zaidi. Na wakati huohuo mipango na uagizaji wa mbolea ulikuwa umekwisha fanyika mbolea ikawa ni

chache kulingana na makisio ya msimu uliopita lakini kilimo kikawa ni kikubwa kwasababu ya bei nzuri waliyokuwa wapeta. Kwa hiyo hii ni habari nzuri kwamba wameongeza uzalishaji sasa mipango inayofuata ni kwamba mbolea hizo ziongezwe kwasababu wakulima wameshawishika kulima zaidi na zaidi.

**SPIKA:** La mwisho Dr. Mzindakaya.

**MHE.CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo bora ni mbegu bora je, Tanzania tutaanza kujitegemea lini kwa kuwa na mbegu yetu hapahapa nchini.

**SPIKA:**Jibu Mheshimiwa Naibu waziri, hilo ndilo swali sahihi la Kibunge fupi na linalenga kitu kinaeleweka.

**NAIBU WAZIRI, KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA:**Mheshimiwa Spika, Taasisi zetu na maeneo yetu ya utafiti yanaendelea kugundua mbalimbali na mpaka sasa hivi tunatumia mbegu mbalimbali za mahindi, za maharagwe, za mtama na alizeti zinazozalishwa humuhumu nchini. Kwa hiyo nchi yetu imeshaanza kujitegemea lakini uwezo wa uzalishaji kwa wingi ndiyo hatujaipata na tunaendelea kuongeza mwaka hadi mwaka na ndiyo maana nilisema kwamba tunasaidiana na magereza pamoja na taasisi yetu ta ASA kuzalisha mbegu zaidi hapa nchini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea na swali linalofuata linaelekezwa katika Wizara hiyo hiyo ya Kilimo safari hii linaulizwa na Mheshimiwa Mgana Msindai wa Iramba Mashariki.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, sasa swali langu lijibiwe kwa makini.

Na. 124

### Mikopo kwa Wananchi Kununulia Mashine za Kilimo

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Singida ndio unaozalisha alizeti nyingi hapa nchini; na kwamba wananchi wa Iramba Mashariki wanataka sana kuomba mikopo kwa ajili ya kununulia mashine za kukamua mbegu za zao hilo ili kupata mafuta na mashudu:-

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao kupata mikopo kupitia Hazina?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hutenga fedha kupitia mfumo wa matumizi ya muda wa kati *(Medium Term Expenditure Framework (MTEF)* kwa ajili ya kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo kupitia Muko wa Pembejeo za Kilimio *(AGITF).* Mfuko wa Pembejeo unatoa mikopo ya mbolea, mbegu bora, madawa ya mimea na mifugo, matreekta makubwa, matrekta madogo *(power tiller),* zana za kukokotwa na wanyamakazi, zana za umwagiliaji na mashine za kusindika na kuongeza thamani ya mazao kwa masharti nafuu.

Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kutoa mikopo ya pembejeo na zana mbali mbali za kilimo kupitia Mfuko wa Pembejeo. Aidha, Serikali imefungua dirisha la mikopo kwa ajili ya kilimo kupitia Benki ya Taifa ya Rasilimali (*Tanzania Investment Bank* – TIB) na kutenga kiasi cha shilingi bilioni 22 kwa ajili hiyo katika mwaka wa 2009/2010. Dirisha hilo limeanza kufanya kazi tangu mwezi Januari, 2010. Huduma inayotolewa inahusu mikopo kwa ajili ya shughuli yoyote ya uwekezaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshaurri Mheshimiwa Mgana I. Msindai ashirikiane na Serikali kwa kuwahimiza wananchi wa Iramba Mashariki wanaotaka kuomba mkopo kwa ajili ya kununulia mashine za kukamua mbegu za alizeti watumie fursa ya Dirisha la Mikopo ya Kilimo katika Benki ya Taifa ya Rasilimali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mshindai swali la nyongeza.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:**Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa fedha alizosema Serikali inatenga yaani bilioni 3 ni fedha ndogo sana ukilinganisha na ukubwa wan chi yetu. Je, Bajeti inayokuja Serikali ipo tayari kuongeza fedha?

(b) kwa kuwa tunaimani na Benki ya *TIB* lakini ina tawi Dar es salaam, Arusha na Mwanza tu na Serikali imepeleka fedha nyingi pale Serikali iko tayari kuishauri Benki hii ili iongeze matawi ili ifike mpaka kwa wananchi wa chini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Maswali ya Mheshimiwa Mbunge ni kama ushauri. Na ninakubaliana na yeye kabisa kwamba kusema kweli kwasababu tumeingia kwenye zana ya KILIMO KWANZA kuna haja ya kuongeza fedha hizi na kwa kadri tutakapokuwa tumewezeshwa kwenye bajeti basi tutaweza kuongeza fedha hizi ili ziweze kufikia wananchi wengi zaidi.

Vilevile katika kuongeza matawi ninakubaliana na yeye kabisa kwasababu kilimo hiki ni cha Tanzania nzima ni vema pale kunapokuwa na uwezo kwa maana ya wafanyakazi na miundombinu ya benki basi yaweze kufika matawi mengi iwezekanavyo.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, sasa ni zamu ya Wizara ya mambo ya ndani ya nchi swali linaulizwa na Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba.

Na. 125

**Kituo chya Polisi Hungumalwa Kushindwa Kuzuia Uhalifu**

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, moja ya majukumu ya Serikali nu kulinda usalama wa raia na mali zao;na kwa kuwa jukumu jukumu hilo hutekelezwa na vyombo vya usalama ikiwa ni pamoja na jeshi la polisi amabalo linatakiwa kuwa na uhusiano na raia linalowahudumia; na kwa kuwa katika kituo cha biashara kilichopo katika kijiji cha Hungumalwa kipo kituo cha polisi ambacho kinashindwa kuzuai uhalifu majambazi katika *SACCOS* ya Hungumalwa na nyumba za kulala wageni katika kijiji hicho:-

(a) Je, ni kitu gani kimepungua katika kituo hicho na kufanya kishindwe kuzuai uhalifu?

(b) Kama zipo sababu zinazojulikana Serikalini ; je ni lini Serikali itakisaidia kituo hicho kiweze kutekeleza majukumu yake vizuri?

(c) Je, Serikali inaridhishwa namahusiano yaliyopo kati ya askari wa kituo hicho na wananchi katika tarafa za Nyamilama na Mwasimba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa MAmbo ya ndani ya nchi naomba kujibu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila Mbunge wa Kwimba lenye sehemu (a) , (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimikiwa Spika, askari katika kituo cha polisi kilichopo katika Kijiji cha Hungumalwa wamekuwa wakijitahidi kuzuia na kupambana na uhalifu kwa kushirikiana na wadau wa usalama wakiwemo wananchi.Hivyo jeshi la polisi halijashindwa kuzuia uhalifu kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge shughuli za Kiuchumi kama vile *SACCOS* Na biashara za nyumba za kulala wageni katika kijiji zinaendelea kufanyika pasipo tishio lolote.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na askari katika kupamabana na kuzuia uhalifu, Kituo cha polisi cha Hungumalwa kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa vitendea kazi na hasa vyombo vya usafiri. Hata hivyo jeshi la polisi litaendelea kudhibiti vitendo vya uhalifu ili kuwawezesha wananchi kuendela kufanya shughuli za kujipatia maendeleo pasipo kubughudhiwa na wahalifu.

(c)Mheshimiwa Spika, mahusiano kati ya askari wa kituo hicho na wananchi katika Tarafa za Namilama na mwamashimba pia ni nzuri. Jeshi la polisi kupitia mpango wa polisi jamii linaendelea kuhamasisha wananchi kuimarisha uhusiano huo waweze kushiriki katika vita dhidi ya uhalifu, Aidha tutaendelea kutumia polisi katika kata kujenga uhusiano na kupata taarifa za uhalifu pamoja na kubaini maeneo dhaifu kiusalama ili hatua zichukuliwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sakila swali la nyongeza.

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA:** Mheshimiwa Spika, sibishani sana na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini inavyoeekea tunatofautiana sana katika tafsiri ya neno kuzuia uhalifu. Mimi nasema *SACCOS* ya Hungumalwa ambayo iko kama mita 30,000 au 40,000 kwenda kituo cha polisi ilivamiwa tena kwa baruti wakavunja na kasiki na kuchukua fedha zote mimi nasema kituo hicho kilishindwa kuzuia yeye anasema kiliweza. Nyumba za wageni walivamiwa wageni mali zao zikachukuliwa ninasema kuwa kituo hicho hakikuweza lakini Waziri anasema kuwa waliweza kuzuia, lakini maelezo ya askari katika kituo kituo kile pamoja na wananchi wanasema kwamba mambo haya yanatokana na upungufu wa Askari pamoja na vitendea kazi.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ilishaahidi kuongeza maaskari pamoja na vitendea kazi pamoja na usafiri ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo hilo ni kubwa sana na kwasababu Waziri amesema mahusiano ni mazuri sana. Na mimi naamini naami kuwa maelezo haya yanatokana na mawasiliano ya kawaida ndani ya Wizara je ni lini Waziri atakuja katika kata ya Mwamashimba na Nyamilama awasiliane na wananchi ili apate taarifa kwa upande wa pili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI**: Mheshimiwa Spika, matukio yanaweza kuwa yalitokea hiyo hatutakanusha lakini ni matukio ambayo yanatokea kila mahala.

Jitihada zimefanyika na ripoti tulizokuwa nazo na siyo kuwa zimetoka katika vyombo vya polisi lakini vimetoka hata katika taasisi ambazo si za kipolisi kwamba mahusiano na hali ya usalama katika Jimbo lake na katika maeneo anayoyazungumza ni ya kuridhisha kwa kweli, lakini naungana na Mheshimiwa Mbunge kuwa tutakuwa pamoja kuhakikisha kwamba hali ya usalama inakuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuja nakuahidi tunazo harakati nyingi nitajitahidi na nitazungumza na wewe tuone kama kutakuwa na uwezekano wa kuja. Maana siyo busara tuanze mimi na wewe kubishana hapa lakini kwa yote hayo nimeyachukua na nikuahidi kwamba tutapanga na tutaweza kuja kuwasilikiza wananchi wanasenaje.

**SPIKA:** tunaendelea Waheshimiwa Sasa ni zamu ya Wizara ya Miundombinu. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Dr Raphaeli Chegeni kwa niaba yake Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Chegeni naomba swali lake namba 126 lijibiwe.

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Na. 126

**Kuweka matuta Barabara ya Nyanguge- Musoma**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI (K.n.y. MHE. DR RAPHAEL M. CHEGENI)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa barabara ya Nyanguge – Musoma imekuwa ikisababisha ajali nyingi na kuwepo vizuizi mwendo barabarani yaani matuta, hivyo kupelekea vifo na uharibifu wa mali za wananchi; na kwa kuwa, kupitia Bunge hili kumekuwa na ahadi za mara kwa mara za kuweka matuta lakini hazijatekelezwa:-

Je, ni lini Serikali itaweka matuta katika maeneo ya Masanza Kona, Mwamanyili, Nyakaboja, Nyamikoma na Kalemela?

**WAZIRI WA MIUNDO MBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* tayari imeanza kazi ya kuweka matuta katika barabara ya Nyanguge – Musoma ili kupunguza ajali zinazosababishwa na mwendo kasi. Hivi sasa mkandarasi anaendelea na ujenzi wa matuta maeneo ya Nyamikoma na Nyakaboja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi swali la nyongeza halafu Mheshimiwa Esther Nyawazwa atamalizia.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, katika hii barabara ya mwanza – Musoma ajali nyingi vilevile zinasababishwa na ufinyu wa barabara hasa ukitambua kuwa barabara ule ina watumiaji wengi wanaoitumia. Napenda kufahamu Serikali ina mpango gani wa kuipanua barabara hii ili wale watumiaji wote wanaoitumia waweze kuitumia pasipo kupata ajali za mara kwa mara.

Moja wapo ya sababu inayosababisha ajali za barabarani ni pamoja na mwendo kasi wa magari. Kama tunavyofahamu siku za nyuma Serikali iliweka mpango wa *speed*

*governor* napenda kufahamu mpango huo Serikali iliweza kufikia wapi kwa ajili ya kupunguza ajali barabarani?

**WAZIRI WA MIUNDO MBINU:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwanza hadi Musoma ni barabara kuu na kufuatana na Sheria ya barabara amabayo tumepitisha 2007. Vipimo vya barabara kuu kwa sasa ni hifadhi ya mita 60 na barabara hiyo tuliijenga kwa upana wa mita 10 pamoja na shoulders hatujawa na mpango thabiti wa kuipanua hivi sasa lakini tutaendelea kuidhibiti kwa kadri inavyowezekana katika maeneo yote yale ambayo ama yana historia ya ajali nyingi ama maeneo ambayo ni hatarishi ili kuhakikisha kuwa tunapunguza ajali katika barabra hiyo.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu *speed governor* ni kweli tulianzisha utaratibu huu lakini kwasababu mbalimbali na nyingine za kiufundi vifaa hivi havikuweza kufanya kazi kwa mafanikio kama tulivyotarajia. Kwa hivi sasa tutaendelea na taratibu za kuhakikisha kwamba tunadhibiti mwendo kwa taratibu mbalimbali pamoja na kutumia wenzetu askari polisi ili kuhakikisha kwamba tunapunguza ajali hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nyawazwa swali fupi la nyongeza.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ina zoezi la kuwekewa matuta maeneo hayo lakini kutoka Kalemela kwenda Lamadi na Bunda mashimo yamekuwa ni mengi sana, Je, zoezi hili haliwezi kwenda sambamba unapoweka matuta na mashimo haya yakazibwa?

**WAZIRI WA MIUNDO MBINU:** Mheshimiwa Spika, nimepokea ushari na tutalifanyia kazi.

Na. 127

**Kukwama kwa Ujenzi wa Barabara ya Mbeya – Chunya Makongolosi**

**MHE. DR. HARRISON MWAKYEMBE (K.n.y. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano aliweka jiwe la Msingi la Ujenzi wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi mwaka jana akiwa ziarani Mkoani Mbeya; na kwa kuwa sasa hakuna hata mita moja iliyowekwa lami kwenye barabara hiyo:-

Je, ni kitu gani kimekwamisha ujenzi huo?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu sawali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi yenye urefu a kilomita 112 cha lami kama ifutavyo:-

(i) Sehemu ya kutoka Mbeya – Lwanjilo (km36):-

Serikali ilianza ujenzi wa sehemu hii ya barabara tarehe 7/ 09/ 2007 kwa gharama ya shilingi bilioni 27 na bilioni na kazi zilipangwa kukamilika mwezi machi 2010.

Lakini kwa bahati mbaya mkandarasi Kundan Singh aliyekuwa najenga sehemu hii ya barabara alishindwa kazi na kuilazimu Serikali kusitisha makataba. Baada ya kusitisha mkataba, mkandarasi huyu alikwenda Mahakamani na kuweka zuio la kusitisha makataba huu.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria tutajitahidi kuhakikisha kesi hii inatolewa uamuzi mapema ili taratibu za kumpata makandarasi mwingine zianze.

(ii) Sehemu ya Lwanjilo- Chunya (km 36):-

Mkataba wa ujenzi wa sehemu hii ulitiwa saini tarehe 15 Juni, 2009 kwa gharama ya shilingi bilioni 40.28 na muda wa kazi ni miezi 27. Kwa sasa mkandarasi yuko kwenye maandalizi ya kuanza kazi na inatarajiwa mnamo mwezi Agosti 2011 kazi zitakuwa zimekamilika.

(iii) Sehemu ya Chunya- Makongolosi (km 40).

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani na nje ili kumaliza sehemu iliyobaki ya Chunya – Makongolosi yenye urefu wa kilomita 40.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa si rahisi kujua muda amabao kesi kati ya Serikali na Mkandarasi Kundan Singh inaweza kuchukua miaka mingi huku ujenzi wa kipande caha kwanza cha barabara hiyo kutoka Mbeya hadi Lwanjilo ukiwa umesimama, Je, Serikali inalionaje wazo la kuhamishia nguvu zake zote za kifedha na utaalamu sasa ilizotenga kwa kipande hicho cha barabara ambacho ujenzi wake umesimama ziende kwenye kipande cha mwisho cha barabara hiyo cha Chunya hadi Makongolosi?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika,mategemeo yetu ni kwamba kwa ushirikiano kama alivyosema kwenye jibu la msingi. Ushrikiano kati yetu

na Wizara ya Katiba na Sheria itawezesha hii kesi kumalizika mapema iwezekenavyo hatujakata tamaa lakini kama itatokea ucheleweshaji mkubwa basi wazo hili la Mheshimiwa Mbunge tutalipokea na tutalifanyia kazi.

**MHE. FLORENCE E . KIENDESYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kiutaratibu jiwe lolote la msingi la mradi wowote. Linapowekwa na Kiongozi yoyote huwa linabaki palepale mpaka mradi husika ukamilike, kwa jiwe hili la msingi lililowekwa na Mheshimiwa Rais ili ujenzi wa barabara kutoka Mbeya, Chunya, Makongolosi na Uwanzu, limekwisha ng'olewa na halipo. Je, Serikali inafahamu hili na nini hatima yake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu namna ya kulipata hili jiwe lililo n'golewa hili.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii kwangu mimi ni mpya. Nilikuwa Mbeya mwezi wa 12 mwanzoni na nilifika eneo ambalo jiwe la msingi liliwekwa jiwe lilikuwepo na hapakuwa na tattizo lolote kwa hiyo inaelekea ni baada ya mimi kuondoka kule na hivi sasa taarifa hizo sikuwa na habari nazo nitazifanyia kazi kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Ahsante sana naomba Mheshimiwa Kiendesya awasaidie polisi. Tunamalizia Wizara ya Nishati na Madini. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Lukas Selelii, Mbunge wa Nzega.

**MHE. LUCAS L . SELELII:** Mheshimiwa Spika sasa swali langu lijibiwe.

Na. 128

**Kuvipatia Umeme Vijiji Vilivyopatiwa Gridi ya Taifa**

**MHE. LUCAS LUMAMBO SELELII** aliuliza**:-**

Kwa kuwa vijiji vya Puge na Ndala, Nkiniziwa na Itilo vimepitiwa na *Grid* ya Taifa tangu miaka ya 1980 ingawa havijapatiwa umeme na kwa kuwa kumekuwa na ahadi ya mara kwa mara ya muda mrefu ya kulipatia umeme vijiji hivyo.

(a) Je, lini (kwa uhakika) vijiji hivyo vimepangwa kupatiwa umeme?

(b) Je, ni gharama kiasi gani kuwa na *substation Puge* na kuleta umeme huo toka Nzega – Puge- Ndala?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu;

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa umeme katika vijiji vya Puge na Ndala, Nkiniziwa na Itilo umeshaanza ambapo shilingi milioni 400 zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 kwa ajili ya upelekaji wa umeme katika vijiji vya Ndala na Shabela Wilayani Nzega. Tenda imeshatangazwa, zabuni imefunguliwa ipoti imewasilishwa wakala wa Nishati vijijini ( REA) kwa ajili ya kupata ridhaa.

Tarehe 29 Januari, 2010 *REA* walitoa ridhaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Taratibu za kusainisha mkataba husika kati ya *TANESCO* na mkandarasi aliyeshinda Zabunu zitakamilika kabla ya mwisho wa mwezi februari 2010, baada ya hapo kazi itaanza mara moja. Vijiji vilivyosalia vimeombewa fedha kutoka kwa Wakala wa Nishati Vijijini *( REA)* na punde fedha zitakapopatikana mchakacho wa kumtafuta mkandarasi wa kutekeleza mradi utaanza kulingana na Sheria za manunuzi.

(b) Mheshimiwa Spika, vijiji vya Puge na Ndala, Nkiniziwa na Itilo vimeshafanyiwa tathimini ya kuvipelekea umeme na *TANESCO* ambapo gharama ya mradi ni shilingi milioni 900.

**MHE. LUCAS LUMAMBO SELELII:** Mheshimiwa Spika, wakati wa kikao cha bajeti Wizara hihi ilituambia kwamba kupeleka mradi Ndala, Puge na Nkiniziwa ni kiasi cha bilioni 3. Lakini kwa majibu ya leo Mheshimiwa Waziri anasema ni shilingi milioni 900 sasa ukweli ni upi? Bilioni 3 au milioni 900?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme ndala mpaka Puge ni mradi wa kama kilomita 100 hivi kwa ujumla wake. Na humu ndani kuna kazi za kupeleka line, transfoma, substation na kadhalika sasa kazi hiyo kwa makadirio ya kitaalamu kwa kilomita moja ni kama milioni 28- 30 unapata kama bilioni 3 kwa kutambua kwamba miradi ya umeme ni mingi na huenda hatutopata utekelezaji wake kama vile tunavyotarajia kupanga.

Mheshimiwa Spika, tumeielekeza REA na T*ANESCO* hasa *TANESCO* watupe tathimini ya utekelezaji wa awamu kwa hiyo milioni 900 ni utelezaji wa awamu ya mradi huo kwa makadirio kwamba mradi huo wa Nzega, Puge, Ndala na hapo karibu kuna mradi wa Bukene, Uyui, na pia mradi wa Urambo – Kaliua wa kuongeza *single phase* kwenda 3 *three phase* kwa hiyo miradi ya pale ni mingi.

Mheshimiwa Spika, kwa pesa iliyopatikana tulisema tupate tathimini za awamu. Awamu ya kwanza itakuwa milioni 900 lakini kazi itaendelea mpaka tufikishe umeme Ndala – Puge- Ndala.

Na. 129

**Kituo cha Umeme Tosamaganga**

**MHE. LEDIANA M. MNG’ONGO (K.N.Y.) MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kituo cha umeme cha Tosamaganga – Iringa, kiliacha kutoa umeme kwa kutumia maporomoko ya maji miaka mingi iliyopita baada ya umeme wa Gridi ya Taifa kuunganishwa Iringa lakini miundombinu yake bado ni imara:-

(a) Je, Serikali itafufua lini kituo hicho na kuunganisha na Gridi ya Taifa hasa ikitiliwa maanani upungufu mkubwa uliopo wa nishati nchini?

(b) Je, kama hilo haliwezekani, kwa nini kituo hicho kisitumike kama kituo cha kusambaza umeme vijijini kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mhehsimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo cha kuzalisha umeme cha Tosamaganga kilichoko karibu na Iringa Mjini, kilikuwa kinatumia maji ya Mto Ruaha kuzalisha umeme. Kituo kilijengwa na Serikali mwaka 1952 na kupanuliwa mwaka 1958. Kituo kilianza na mashine moja yenye uwezo wa kuzalisha umeme *KW400* na mashine iliyoongezwa ilikuwa na uwezo wa kuzalisha *KW800*. Mashine yenye uwezo wa kuzalisha *KW 400* iliharibika mwaka 1990 na mashine ya uwezo wa kuzalisha *KW800* iliharibika mwaka 1995 na baada ya ya mashine zote kuharibika, kituo kikafungwa mwaka 1995. Kuharibika kwa mashine hizo, kulitokana na uchakavu wa mitambo na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kufufua kituo cha umeme cha Tosamaganga ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Hivyo, Serikali kwa kupitia *TANESCO,* inatafuta mwekezaji atakayekifufua na kukiendesha kituo hicho kwa kipindi maalum ili aweze kuuza umeme katika kipindi hicho. Baada ya kwisha kwa kipindi hicho kitakachokubaliwa baina ya *TANESCO* na mwekezaji, kituo kitaendelea kuwa mali ya Serikali. Tenda kwa ajili ya kumpata mwekezaji katika kituo hicho, ilitangazwa mwezi Juni 2009 na kampuni tisa zimejitokeza. Hatua iliyofikiwa sasa ni kufunguliwa kwa zabuni za wawekezaji walioonyesha nia ya kushiriki yaani *expression of interest.*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Galinoma kwa ufuatiliaji wake wa karibu na wa muda mrefu ili kupata kupata ufumbuzi wa kufufua kituo cha Tosamaganga.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini ningependa kufahamu yafuatayo:-

(a) Kwa vile zabuni imeshatangazwa, ni lini Mwekezaji ataanza kazi na umeme kuzalishwa ambapo unaweza kutumika katika eneo la Jimbo la Kalenga?

(b) Kwa vile Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Rugemba, ni chuo cha muda mrefu na kinatumia jenereta, je, Waziri atakubaliana nami kwamba kwa vile kiko barabarani ambako zinapita nyaya za umeme, Serikali itakuwa tayari kuweka umeme wa Gridi ili wanafunzi wapate umeme wa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la lini, kama nilivyosema, kwa sasa hivi, *TANESCO* walitoa matangazo, wakapata *experession of interest* kutoka kwa makampuni kama tisa hivi. Kwa sasa hivi, ufahamu wangu ni kwamba ule utaratibu wa kuyafanyia makampuni yale tathmini na kuingia nao makubaliano, ndiyo unaoendelea. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria, tunataka tuwaruhusu hawa wawekezaji binafsi waendeshe vituo hivi wao wenyewe. Nadhani tukubaliane tu kwamba kipindi hiki ni kipindi cha kuafikiana baina yao na tumetangaza pia kwa vituo vya Kukiletwa na Mbalizi kule Mbeya, tumeomba pia kule Mgeta kwa Mheshimiwa Ligallama, kwa hiyo, tunatarajia kwamba hivi vituo vidogo vitaendeshwa na wawekezaji binafsi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, itakapokamilika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Galinoma kwamba, tutawafahamisha maendeleo ya makubaliano haya baina ya *TANESCO* na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, nadhani Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rugemba kinastahili kupata umeme kama ambavyo utaratibu wa kupata umeme hasa kwenye vyuo vya elimu na vituo vingine vya jamii ulivyo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba tutalifanyia kazi na kwa sababu umeme wa Gridi unapita hapo karibu na chuo, sidhani kama hili litakuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, tutalifanyia kazi na nitamtaarifu matokeo ya kazi hii. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, nina swali dogo la nyongeza, kwa kuwa, swali la msingi lililoulizwa linafanana na maporomoko ya *Stigler's Gorge*, je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuyatumia maporomoko hayo baada ya utafiti uliofanywa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nifafanue kwamba mradi wa *Stigler's Gorge* na miradi kama ya Kikuletwa na Tosamaganga na Mbalizi, ni tofauti kidogo, kwa sababu mradi wa *Stigler's Gorge,* ni mradi ambao *potential* ya *hydrology* inayopita pale, mradi ule unaweza ukazalisha zaidi ya *megawatt* 2000. Lakini huu ni mradi mkubwa na gharama yake ni kubwa sana na unaweza ukatekelezwa ama kwa kuzalisha *megawatt* 2000 au kwa awamu, kwa maana upate labda *megawatt* 800 halafu uongeze mitambo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *Stigler's Gorge,* ni mradi wa siku nyingi, umefanyiwa utafiti kwa zaidi ya miaka thelathini, kwa ufahamu wangu na tuko kwenye utaratibu wa kupata wawekezaji ambao wanaweza kuuendeleza mradi ule kwa manufaa ya Taifa. Lakini pia

ni lazima tuzingatie na tufahamu kwamba mradi ule umekaa kwenye maeneo ambayo kuna athari za kimazingira ambazo zinaweza kutokea, kwa hivyo, ni lazima *environmental* na *social impact assessment* ya ukamilifu ifanyike ili kujua utekelezaji wake kwa kulinganisha na athari zingine za kimazingira.

Mheshimiwa Spika, tathmini inafanywa na tukikamilisha kufanya tathmini hiyo, naamini tutakuja kutoa maelezo kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu mazuri na majibu yaliyotosheleza kabisa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni matangazo, nitaanza na Tanzia ya Mtumishi. Nasikitika kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mtumishi Marco Wanyange Ngwebesa, aliyekuwa *Head Driver,* amefariki jana tarehe 7/2/2010. Maiti itasafirishwa leo tarehe 8/2/2010, kuanzia saa saba kwenda Nyang'wale, Geita, Mwanza, baada ya kuagwa nyumbani kwake Nkhungu. Kwa hiyo, wale Waheshimiwa Wabunge ambao watapenda kufika na kutoa rambirambi pale Nkhungu, utaratibu utafanywa na Utawala ili hilo liwezekane, kumuaga Mtumishi huyu ambaye ametumikia Ofisi ya Bunge kwa muda mrefu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, kwa rehema zake, ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, leo tuna wageni wengi kidogo, nitaanza na wale ambao wanatokea maeneo ya nje kabisa lakini wapo Dar es Salaam kwa shughuli maalum, nao ni wageni kutoka Jumuiya ya Ulaya ambao ni Mheshimiwa Tim Clarke, Balozi wa Jumuiya ya Ulaya, *as I call your name your excellencies, please rise so that Members of Parliament can acknowledge you. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mheshimiwa Jacques Champagne de Labriolle, Balozi wa Ufaransa, Mheshimiwa Francesco Catania, Balozi wa Italia, Ndugu Rene Van Nes, Afisa kutoka Jumuiya ya Ulaya, yupo Bi. Pia Weurlander, kutoka Jumuiya ya Ulaya, Bi. Monique Korzelius, Mshauri wa Masuala ya Kisiasa na Utamaduni, Ubalozi wa Uholanzi na Bi. Agnes Hanti, Mshauri Masuala ya Sera na Utawala Bora, Ubalozi wa Uholanzi. *It is always a pleasure for us here in Parliament to receive visitors from important development partners, you are warmly welcome and please try to enhance our relationships, be healthy to Tanzania as much as you can, we are trying very much to get ride of poverty, so lets work together. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina furaha kubwa sana kuwatambulisha wageni kumi na saba wa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dr., jamani mnapomwita Mheshimiwa Magufuli, msisahau siku hizi ni Dokta, tena kwenye masuala ya Kemia. Alinileteа ile *Thesis* yake, kwa mtu kama mimi ambaye Sayansi kidogo ipo pembeni, toka ukurasa wa kwanza sikuelewa chochote lakini nimeitunza pale nyumbani kama rekodi ya Mbunge aliyefanikiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Dokta Magufuli, anao wageni wake kumi na saba ambao ni kama ifuatavyo, kadri nitakavyowataja, msimame mmoja mmoja tuwatambue. Amekuja na

Mheshimiwa Mwalimu Hadija Nyembo, Mkuu wa Wilaya ya Chato, usisahau kuwa unakwenda likizo nyumbani Tabora. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Ibrahimu Bagura, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Ndugu Jumanne Simba, Katibu wa CCM Wilaya, Ndugu Peter Mashenji, Mweka Hazina wa CCM Wilaya, Ndugu Barnabas Nyirembe, Katibu Mwenezi wa CCM wa Wilaya, Ndugu Magesa Kichwele, Mwenyekiti wa Halmashauri, Ndugu George Magezi, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, Ndugu Ramadhan Ndaki, Katibu Msaidizi wa CCM Wilaya, Ndugu Batholomeo Manunga, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Wilaya, Ndugu Elias Ntale, Mjumbe wa Kamati ya Siasa, Ndugu Eramu Lubagora, Mjumbe Kamati ya Siasa, Ndugu Sirilo Stephan, Katibu Ofisi ya Mbunge Chato, Bibi Diana Busimilo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana, Bibi Helena Basumilo, Mjumbe, Bibi Anastazia Basomi, Mjumbe, Bibi Pili Katemi, Mjumbe Kamati ya Siasa na Bibi Beatrice Kasanda, Mwenyekiti wa UWT wa Wilaya. Karibuni sana wageni wetu kutoka Chato, napenda mfahamu kwamba, tunamthamini sana Waziri Magufuli, ni mmoja wa watendaji wazuri sana katika Serikali ya Awamu ya Nne na Waheshimiwa Wabunge huwa wananinong'oneza kwamba wanachokipenda zaidi ni kwamba huyu ni mkweli, hana ubabaishaji, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Sevelina Mwijage, ni Ndugu Amir Abdallah ambaye ni Mkurugenzi wa *Blue Guard*, yupo wapi? Ndiyo yule bwana mwenye baraghashia? Ooh, karibu sana, haya maneno kama *Blue Guard* wengine hatujazoea lakini hata hivyo karibu hili ni Bunge lako. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene ambao ni wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* wakiongozwa na Mbijima Leopold, kiongozi wa msafara, wasimame, karibuni sana, tunawatakia mema katika masomo yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni saba wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro wa Vunjo, wanaongozwa na Mchungaji Elias Silayo kutoka KKKT, Usharika wa Kirimeni Mwika. Baba Mchungaji na wageni karibuni sana na mtusalimie mtakaporejea huko na tuzidi kuombeana kwa sababu mwaka huu ni mgumu kidogo. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja, kwanza ni Ndugu Cecilia Charles Keenja ambaye ni mkewe Mheshimiwa Mbunge, karibu sana. Ndugu John Mmari na mkewe Bi. Romana Mmari, marafiki wakubwa wa familia. Kwa maelezo, hawa wawili ni wajasiriamali, mke wa Mbunge si mjasiriamali. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo; hawa Wabunge wa Kanda ya Ziwa, wanajitahidi kweli. Mheshimiwa Diallo alikwenda Australia kuchukua Shahada yake hiyo, kwa hiyo, naye ni Doctor sasa hivi. Wageni wake ni 40 kutoka Wilaya ya Ilemela wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Ndugu Kamese, Katibu wa CCM wa Wilaya, Ndugu Shimba, Wajumbe wa Kamati ya Siasa wa Wilaya, Wanezi wa Kata tisa na wakereketwa wa CCM Ilemela. Wale pale karibuni sana. Inaelekea mnafanya kazi nzuri ya kumlea Mheshimiwa Mbunge, sasa nadhani wale

wanaonyemelea Jimbo la Ilemela, mna majibu ya kuwapa kwa sababu Mheshimiwa Diallo, ni madhubuti na anafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara, wameniomba nitangaze kuwepo kwa mgeni wao Ndugu Mshamu Nayopa, yeye ni Katibu wa Siasa na Uenezi Mkoa wa Mtwara. Karibu sana. Huu ndiyo mwisho wa wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Viwanda na Biashara, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati hiyo, mkutane leo saa saba, Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, nimetoa ridhaa Kamati hii ikutane saa tano kwa sababu inapitia Muswada ule wa Gharama za Uchaguzi, huu ni Muswada muhimu na waupitie kwa uangalifu. Wale Wabunge ambao wana mawasilisho maalum ambayo wanataka yaingizwe katika mapendekezo ya mabadiliko, nao pia wakatoe machango wao na kurejea Bungeni kwa sababu Muswada huu ni muhimu na unahitaji ushirikiano wa sisi sote kuupitisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunazo chaguzi za kupata uwakilishi katika taasisi zifuatazo:- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nafasi mbili, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, nafasi moja, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara, nafasi moja na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, nafasi moja. Inaelekea kuna kusitasita kuchukua hizi fomu. Sasa hii ni dalili ya mtu kutokujiamini tu; ingawa kipindi cha kuhudumia kinakwisha Oktoba 2010; lakini kwa nini mtu usijiamini kwamba utaendelea kuwa Mbunge. Nawaomba, imani hujenga imani, nendeni mchukue fomu, tuwachague na haya ni mazuri, unapopiga kampeni unawaambia, mimi nimechaguliwa na Wabunge kuwa mwakilishi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inasaidia. *(Kicheko)*

Uchaguzi huu, utafanyika Jumatano tarehe 10/2/2010 mara baada ya kipindi cha maswali. Kwa hiyo, *Returning Officer* atapokea maombi kesho. Naomba sana tujitahidi.

Mheshimiwa George Simbachawene, ameniomba nisahihishe wageni wake wanatoka *St. John University* na si *Dodoma University*.

Leo shughuli zitakazoendelea zitahusu Maazimio matatu na kuna uwezekano mkubwa pengine shughuli zikasitishwa saa saba. Kwa hiyo, Naibu Spika, amenikumbusha kwamba ikitokezea hivyo, basi vile Vikao vya Vyama mkutane saa kumi na moja jioni isipokuwa hivyo, basi itakuwa tena baada ya Maazimio yale kupitishwa lakini tunaamini kwamba haitachukua muda wote huo. Kwa hiyo, saa kumi na moja jioni inawezekana *party caucus* zikafanyika.

Waheshimiwa Wabunge, ahsante kwa kunivumilia, matangazo siku nyingine yanakuwa mengi lakini si kila siku. Kwa hiyo, kwa kuwa nina wageni, nimemwomba Mheshimiwa Jenista Mhagama, aje ashike Kiti.

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa nimwite Katibu aendelee kutuongoza kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge la Kutidhia Mapendekezo ya Mabadiliko katika baadhi ya vipengele vya Mkataba ulioanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa maelekezo ya Mheshimiwa Spika, sasa tutaingia katika ajenda ya maazimio na Azimio letu la kwanza linawasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali Kuridhia Mapendekezo ya Marekebisho ya Makubaliano ya Kimataifa *(Articles of Agreement)* yaliyoanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa *(International Monetary Fund – IMF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar M. Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili hapo siku ya Jumamosi, tarehe 6 Februari, 2010. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba michango yao tunaithamini na pia tunaifanyia kazi katika kuboresha sera na mageuzi ya kiuchumi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu marekebisho yanayokusudiwa ambayo tunaliomba Bunge kuridhia. Lengo la marekebisho kwanza; kuongeza kauli na ushiriki wa nchi za Kiafrika katika uendeshaji wa *IMF*; na pili ni kuiongezea mamlaka *IMF* katika kufanya maamuzi ya kuwekeza rasilimali za nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Fedha la Kimataifa lilianzishwa mwezi Julai mwaka 1944 katika Mkutano wa Kimataifa uliofanyika mjini Bretton Woods, New Hampshire, nchini Marekani, likiwa na jumla ya nchi wanachama 45. Hadi kufikia tarehe 29 Juni 2009, Shirika hili lilikuwa na jumla ya wanachama 186.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa la *IMF*, ni kusimamia mfumo wa fedha Duniani kwa kufuatilia Sera za Uchumi mpana wa nchi wanachama, hasa zile zinazoathiri viwango vya ubadilishaji wa fedha *(exchange rate)* na urari wa malipo *(balance of payment). IMF* hutekeleza jukumu hili kwa kutoa ushauri wa kisera na inapobidi, misaada ya kifedha ya muda mfupi na muda wa kati kwa nchi zinazokabiliwa na matatizo makubwa ya kifedha na kiuchumi kwa kutumia michango ya nchi

wanachama. Aidha, nchi wanachama zenye matatizo ya urari wa malipo, ambao hutokana na matatizo ya kifedha na kiuchumi zinaweza kuomba mikopo itakayosaidia kutatua tatizo hili. Baada ya kupata mkopo, nchi wanachama zinatakiwa kufanya mageuzi ya kisera, kimuundo na kisheria ili kurekebisha matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu ilipojiunga na *IMF* mwaka 1962, Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo imeendelea kupata misaada mbalimbali ya kifedha chini ya mipango mbalimbali ya Shirika hilo. Kuanzia mwaka 1996 hadi 2003, Tanzania ilinufaika na mpango wa *IMF* wa kupunguza umaskini na kukuza uchumi, ambapo chini ya mpango huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata mkopo wa riba nafuu unaokaribia dola za Kimarekani milioni 500. Mnamo mwezi Mei 2009, Shirika la *IMF* pia lilitoa mkopo wa riba nafuu wa kusaidia urari wa malipo kutoka Mfuko Maalum wa *Exogenous Shock Facility*, unaokaribia dola za Kimarekani milioni 328. Mkopo huu umeiwezesha Tanzania kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizotokana na mtikisiko wa uchumi ulioikumba Dunia hivi karibuni. Nchi yetu pia imenufaika na inaendelea kunufaika na ushauri wa kisera unaotolewa na *IMF* katika maeneo mbalimbali ya fedha na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Makubaliano ya Kimataifa, maamuzi yoyote makubwa yanayofanywa na *IMF* huhitaji asilimia 85 ya kura za wanachama, ili maamuzi hayo yaweze kupitishwa. Uwezo wa kupiga kura unaambatana na kiasi cha hisa za kila nchi mwanachama kinachofahamika kama "*quota*". Nchi zilizoendelea zimekuwa zinachangia kiasi kikubwa cha fedha katika mtaji na kuwa na hisa na kura nyingi katika *IMF*. Wingi wa kura unafanya nchi husika kuwa na nguvu na kauli kubwa katika kupiga kura, wakati wa kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu sera na programu za *IMF*. Kwa upande mwingine, nchi zinazoendelea ambazo ni asilimia 85 ya wanachama wote wa *IMF*, zina hisa na nguvu ya asilimia 27 tu, ambayo ni kidogo na ndiyo hutumika katika kupiga kura wakati wa kufanya maamuzi mbalimbali ndani ya *IMF*. Hali hii inatokana na udogo wa michango yao katika Shirika hili la *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwakilishi na ushiriki katika *IMF*, wa nchi za Afrika zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, ni kupitia katika Majimbo mawili (*Constituencies*). Jimbo la kwanza linaundwa na nchi zinazozungumza Kiingereza (*Anglophone*), Tanzania ikiwa katika Jimbo hili. Jimbo la pili ni la nchi zinazozungumza Kifaransa (*Francophone*). Kila Jimbo linaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji (*Executive Director*) akisaidiwa na Mkurugenzi Mtendaji Mwenza (*Alternate Executive Director*). Aidha, jumla ya kura za kila Jimbo zinatokana na jumla ya kura za nchi wanachama zinazounda Jimbo hilo. Jimbo la (*Anglophone*) lenye nchi 20 lina asilimia 3.01 ya kura zote ikilinganishwa na Marekani yenye asilimia 16.77. Kwa upande mwingine, Jimbo la nchi 23 zinazozungumza Kifaransa lina asilimia 1.35 tu. Hivyo, kuongezeka kwa kura za nchi moja moja kutaongeza pia kura za Majimbo haya. Jimbo la (*Anglophone*) linajumuisha nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Zimbabwe, Zambia, Botswana, Lesotho, Swaziland, Msumbiji, Sierra Leone, Liberia, Malawi, Eritrea, Nigeria, Namibia, Angola, Sudan, Ethiopia pamoja na Gambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya marekebisho yanayopendekezwa katika kipindi cha miaka 65, tangu kuanzishwa kwa Shirika la IMF, nchi zilizoendelea, zimeendelea kuwa wakopeshaji wakubwa wa *IMF* wakati nchi zinazoendelea zimebaki kuwa wakopaji wakubwa kutoka katika Shirika hili. Mpangilio huu umezifanya nchi zinazoendelea mara nyingi kuwa wahanga wa Sera za *IMF*. Kutokana na upungufu huo, nchi zinazoendelea kwa kipindi kirefu zimekuwa zikipigania kuongezewa kauli na ushiriki katika uendeshaji wa *IMF*, ili ziweze kuwa na ushiriki wa manufaa wakati wa majadiliano yanayohusu mahitaji ya nchi za Afrika katika mikutano ya Shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano wa *IMF* na Benki ya Dunia uliofanyika mwezi Oktoba, mwaka 2009 mjini Istanbul nchini Uturuki, Magavana wa *IMF* ambao ni Mawaziri wa Fedha au Magavana wa Benki Kuu wa nchi wanachama, waliafiki ombi la nchi za Kiafrika kuongezewa kauli katika uendeshaji wa *IMF*. Kufuatia makubaliano hayo, Magavana hao pia waliafiki hoja ya kufanyia marekebisho baadhi ya vifungu vya Mkataba wa Makubaliano wa Kimataifa ulioanzisha *IMF* yanayolenga kuongeza kauli na ushiriki wa nchi za Afrika katika uendeshaji wa *IMF* pamoja na kuongeza uwezo wa *IMF* katika kufanya maamuzi kuhusu uwekezaji wa rasilimali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha marekebisho yanayo pendekezwa kufanyika, ni budi kila nchi mwanachama kuridhia kufanyika kwa marekebisho hayo ya Mkataba wa Makubaliano ulioanzisha *IMF*, kupitia utaratibu wa kisheria unaokubalika katika kila nchi mwanachama. Marekebisho haya yalipaswa kuridhiwa hadi kufikia mwezi Desemba, mwaka 2009. Hata hivyo, hadi kufikia mwisho wa mwezi Desemba mwaka 2009, nchi wanachama arobaini na tano zilikuwa zimeridhia marekebisho yanayopendekezwa. Kati ya nchi hizo nne ni kutoka katika Jimbo la *Anglophone*, zikiwemo Kenya, Eritrea, Malawi na Lesotho. Juhudi za kuhamasisha nchi nyingine wanachama kuridhia marekebisho haya zinaendelea kupitia Ofisi za Wakurugenzi Watendaji wa Majimbo mawili ya Afrika na kupitia Ofisi za Wizara za nchi wanachama zinazoshughulika na mahusiano na *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yanayopendekezwa. Kwanza kuongeza Kauli na Ushiriki wa nchi za Afrika katika uendeshaji wa IMF katika Ibara ya 12 ya Mkataba huo ni kama ifuatavyo:-

Ibara ya 12(3)(e), inapendekeza kila Mkurugenzi Mtendaji katika Majimbo mawili yanayowakilisha nchi za Afrika katika *IMF*, kuteua Wakurugenzi Wenza wawili badala ya utaratibu wa sasa ambapo huteua Mkurugenzi mwenza mmoja. Kutokana na Majimbo mawili tuliyonayo, marekebisho hayo yatatuwezesha kuwa na Wakurugenzi wenza wawili zaidi katika Bodi ya *IMF*. Endapo mapendekezo haya yataridhiwa na idadi inayokubalika ya nchi wanachama, yataziwezesha nchi za Kiafrika kuwa na kauli na ushawishi zaidi katika masuala ya kisera na fedha wakati wa majadiliano na *IMF*, kwa faida na manufaa ya nchi za Afrika. Marekebisho hayo pia yataongeza uwezo wa ofisi za Wakurugenzi wetu Watendaji katika *IMF* katika kuhudumia nchi wanazoziwakilisha kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine yanahusu, Ibara ya 12(5)(a) kinachohusu ongezeko la kura za kawaida (*Basic Votes).* Tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo kila mwanachama ana kura 250 za kawaida, sawa na asilimia 2 ya kura zote. Kulingana na marekebisho haya, kura za kawaida zitakuwa asilimia 5.502 ya jumla kuu ya kura zote za wanachama wote. Jumla ya kura za kila mwanachama zitaendelea kujumuisha kura za kawaida na kura zinazotokana na hisa (*quota-based).* Marekebisho haya yanatarajiwa kuongeza idadi ya kura za kawaida na hivyo kuongeza kauli ya nchi wanachama, hususan nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho mengine yanahusu Aya namba 2 ya "Jedwali L" kuhusu matumizi ya kura za mwanachama ambaye haki ya kupiga kura imesitishwa kwa muda. Marekebisho haya yana lengo la kuweka masharti juu ya matumizi ya kura alizonazo mwanachama wa aina hii na pia kulinda haki stahiki. Uwezo wa kupiga kura wa mwanachama wa aina hii hautatumika kwenye chombo kingine chochote cha *IMF* isipokuwa kwa madhumuni yafuatayo:-

(i) kupiga kura kukubali mapendekezo ya marekebisho yanayohusu Idara ya "*Special Drawing Rights*"; na

(II) kukokotoa kura za kawaida za mwanachama wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni kuongeza uwezo wa *IMF* katika uwekezaji. Ibara ya 12(6)(f)(iii), inapendekeza marekebisho yatakayowezesha *IMF* kutumia sarafu ya nchi mwanachama iliyoko katika akaunti ya uwekezaji, kama itakavyoona inafaa, iwapo maamuzi hayo yataungwa mkono kwa asilimia 70 ya kura za wanachama wote. Tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo *IMF* haiwezi kutumia sarafu hii bila ridhaa ya nchi husika. Marekibisho haya yanaipa *IMF* mamlaka ya kuweza kutumia fedha zitokanazo na michango ya nchi wanachama na hasa nchi zilizoendelea kuwekeza na kusaidia katika nchi zinazoendelea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12(6) (f)(vi), inapendekeza utaratibu utakaotumika katika kusitisha akaunti ya uwekezaji wa *IMF*, endapo *IMF* itafilisika au kiwango cha uwekezaji kitakapopungua kabla ya kufilisika. Utaratibu utazingatia wingi wa kura wa asilimia sabini ya kura zote zitakazopigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5(12)(h), inapendekeza marekebisho yatakayoiwezesha *IMF* kutumia fedha za mwanachama zilizoko katika Akaunti Maalum **(***Special Disbursement Account)* kuwekeza, kadiri itakavyoona inafaa, kulingana na Kanuni na Taratibu zilizopitishwa na *IMF*. Marekebisho haya yanakusudia kuipa *IMF* uwezo wa kutoa misaada zaidi kwa nchi zinazoendelea bila kulazimika kupata ridhaa ya wanachama wenye hisa nyingi katika *IMF* kama vile Marekani, Uingereza na nchi nyingine zilizoendelea. Aidha, pato na riba itokanayo na uwekezaji huu itawekwa katika akaunti maalum na hivyo kuifanya akaunti hiyo iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mengine yanahusu kuongeza sehemu mpya katika Ibara ya 12 kwa kuongeza Ibara mpya ya 12(k), inayopendekeza marekebisho yatakayoiwezesha *IMF* kuweka mapato yatokanayo na mauzo ya dhahabu

kwa kiasi kinacholingana na bei ya kununulia, katika Akaunti ya Kawaida ya Rasilimali *(General Resources Account).*

Aidha, kwa mauzo yatokanayo na manunuzi yaliyofanyika baada ya tarehe ya marekebisho ya pili ya Mkataba wa Kimataifa (*Articles of Agreement*) za *IMF* na mauzo yaliyofanyika baada ya tarehe 7 Aprili 2008 au tarehe yoyote kabla ya kuanza kutumika kwa marekebisho haya, kiasi chochote cha ziada (tofauti kati ya mapato na bei ya kununulia) kitahamishwa kutoka katika Akaunti ya Kawaida za *IMF* na mauzo yaliyofanyika baada ya tarehe 7 April mwaka 2008 au tarehe yeyote kabla ya kuanza kutumika kwa marekebisho hayo kiasi chochote cha ziada kitahamishiwa katika akaunti ya kawaida na kuwekwa katika akaunti ya uwekezaji. Marekebisho haya yana lengo la kutunisha akaunti ya uwekezaji na ile maalum na kuifanya akaunti hii maalum iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, marekebisho yanayopendekezwa yanatokana na hoja ya nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Endapo yatapitishwa na nchi wanachama, marekebisho haya yatazisaidia nchi za Kiafrika kuongeza ushiriki na kauli katika kutafuta maslahi ya nchi za Kiafrika ndani ya *IMF*. Ninaamini kwamba, nchi za Kiafrika ikiwemo nchi yetu Tanzania, zitakuwa mstari wa mbele katika kuridhia marekebisho yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, marekebisho ya Mikataba ya Kimataifa ya aina hii yanapaswa kuridhiwa na Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* lililoanzishwa mwezi Julai, 1944;

**NA KWA KUWA** malengo makuu ya Shirika la Fedha la Kimataifa ni pamoja na kusimamia mfumo wa fedha duniani, kufuatilia Sera za Uchumi wa nchi na kutoa ushauri wa kisera na misaada ya kifedha kwa nchi wanachama;

**NA KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Shirika la Fedha la Kimataifa wanaonufaika na misaada mbalimbali ya kifedha na ushauri wa kisera ambao umeiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukabiliana na changamoto mbalimbali za mabadiliko ya kiuchumi;

**NA KWA KUWA** nchi za Kiafrika ambazo ni wanachama wa Shirika la Fedha la Kimataifa zinatambua umuhimu wa nchi za Kiafrika kuwa na kauli katika uendeshaji wa Shirika hilo kwa kushiriki kikamilifu katika majadiliano yanayohusu mahitaji ya nchi hizo;

**NA KWA KUWA** katika Mkutano wa mwaka uliofanyika mwezi Oktoba, 2009 huko Istanbul, Uturuki, nchi wanachama wa Shirika la Fedha la Kimataifa ziliafiki

mapendekezo ya nchi za Kiafrika kufanya marekebisho katika Mkataba ulioanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa ili kuzipatia nchi za Afrika kauli na kuongeza ushiriki wa nchi hizo katika uendeshaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa pamoja na kuongeza uwezo wa Shirika hilo katika kufanya uamuzi kuhusu uwekezaji wa rasilimali zake;

**NA KWA KUWA** Ibara ya ishirini na Saba ya Makubaliano ya Kimataifa (*Articles of Agreement*) yaliyoanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa inaelekeza kwamba marekebisho ya Mkataba yanayopendekezwa yatakubalika na kuanza kufanya kazi baada ya theluthi mbili ya nchi wanachama kuridhia;

**HIVYO BASI** kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhiwa kwa marekebisho ya mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura ya Pili, linaazimia kuridhia marekebisho ya Mkataba ulioanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa ili kuwezesha nchi za Kiafrika, ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na kauli na ushiriki katika uendeshaji wa Shirika la Fedha Duniani, ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa Shirika hilo kufanya uamuzi kuhusu uwekezaji wa rasilimali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa sasa, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Azimio hili ama mwakilishi, Mheshimiwa Mwenyekiti Dokta Abadallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007, niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Azimio la Kuridhia mapendekezo ya Marekebisho ya Makubaliano ya Kimataifa yaliyoanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Waziri wa Fedha kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati, Wajumbe wamelichambua na kulielewa na hivyo kukubaliana kwa kauli moja kuliomba Bunge hili Tukufu kukubali na kuridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Azimio hili, limetokana na Nchi 43 za Afrika kati yake ni zile 20 zinazozungumza Kiingereza *(Anglophone)* na 23

zinazozungumza Kifaransa *(Francophone),* zote zikiwa ni nchi wanachama wa Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF).* Sababu ya chimbuko hili ni kwa nchi hizi za Afrika kuona kwamba hazina haki na kauli ya kutosha ya kujiamulia mambo yao na badala yake kuamuliwa na nchi nyingine hususan zile zilizoendelea. Azimio hili ni kwa faida yetu na tumelianzisha na kulipeleka wenyewe *IMF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, mapendekezo yaliyotolewa ya marekebisho ya makubaliano ya Kimataifa *(Articles of Agreement)* yaliyoanzisha *IMF,* yamejielekeza katika maeneo ya jumla mawili.

(a) Kuongeza kauli na Ushiriki wa Nchi za Afrika katika uendeshaji wa *IMF*; na

(b) Kuongeza uwezo wa *IMF* katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitaka kupata ufafanuzi ni kwa kiwango gani kauli na ushiriki wa nchi hizi utaongezeka na ni kwa utaratibu gani marekebisho haya yatasaidia na kuongeza uwekezaji wa *IMF* katika Nchi za Afrika. Aidha, Kamati imeuliza kwa vile wenye maamuzi makubwa *IMF* ni zile nchi kubwa zenye kura nyingi *(basic votes)* na wanaochangia fedha nyingi, kama vile Marekani, Uingereza n.k, ni kweli kwamba kauli ya Nchi za Afrika itakuwa na nguvu, hasa ikieleweka kwamba sisi ni wakopaji tu *(recipients).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeeleweshwa kuwa uchache wetu hivi sasa kwenye Bodi ya *IMF* umetugharimu katika kutoa maamuzi, hasa ikieleweka Bodi ya *IMF* ndio inayotoa maamuzi yote. Marekani kama nchi, ina mjumbe mmoja katika Bodi, pamoja na Uingereza, wakati Nchi 20 zinazozungumza Kiingereza, Tanzania ikiwemo tuna mjumbe wa Bodi mmoja na msaidizi, wakati zile Nchi 23 zinazozungumza Kifaransa, nazo zinawakilishwa na mjumbe mmoja na msaidizi. Marekebisho haya yatawezesha badala ya kuwa na wawakilishi wanne, lengo ni kuwaongeza wafikie sita kwenye Bodi ya *IMF* na hapo hapo tukiendelea na juhudi zetu za kukuza uchumi wa nchi zetu ili kuwa na sauti kubwa zaidi. Hivi sasa ni nchi mbili tu Afrika, yaani Afrika ya Kusini na Nigeria ndizo zenye sauti kubwa binafsi katika *IMF*. Tija ya Wajumbe wanne kutembelea nchi 43 za Afrika kwa ukweli ni ndogo, tukizingatia mabadiliko ya uchumi yanayoendelea hivi sasa. Hadi hivi sasa katika nchi Wanachama 186; Nchi 45 zimekwisharidhia Azimio hili, wakati katika Nchi 20 zinazozungumza Kiingereza Nchi nne hadi sasa zimeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuongeza uwezo wa *IMF* katika uwekezaji, Kamati ilitaka ipate maelezo kwenye eneo la matumizi ya fedha za nchi mwanachama wa *IMF* zilizoko katika Akaunti Maalum *(Special Disbursement Account)* ya kuwekeza; Kuruhusu *IMF* kuwekeza fedha au hisa za nchi bila ya ridhaa ya nchi husika; masuala ya riba na mapato yatasaidiaje nchi husika endapo fedha hizo zitawekezwa katika miradi au maeneo yasiyolipa na nani atabeba mzigo huu. Kamati imearifiwa kuwa fedha zinazolengwa ni zile za Nchi tajiri ambazo mara nyingi

zinapelekwa kwenye uwekezaji salama na wenye tija na baada ya kuzingatia vigezo vya kuwekeza vinavyoamuliwa na Bodi ya *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rekebisho hili linaloongeza uwezo wa *IMF* kuwekeza lina lengo la kuondoa urasimu na ucheleweshaji wa kutoa maamuzi mara fedha za *IMF* zinapohitaji kutumika na Nchi za Afrika. Inapotokea haja ya kutumia fedha za uwekezaji za *IMF* kwa Nchi za Afrika inabidi Nchi zote Wanachama 186, zote ziulizwe na zitoe kauli ya kukubali au kukataa. Marekebisho yanayolengwa yanaipa uwezo Bodi ya *IMF* kuamua fedha hizo zitumike au la badala ya kusubiri maamuzi ya Nchi zote 186. Aidha, marekebisho haya yanatoa uwezo kwa Bodi ya *IMF* kutumia fedha za Kigeni au fedha za Nchi husika kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile ilitaka kujua uteuzi wa Wasaidizi hawa kutoka Nchi za Afrika unafuata misingi gani ili kuepuka uteuzi usio sahihi. Kamati imearifiwa kuwa Bodi ya *IMF* huwa inatoa vigezo vya kitaalam na kuziachia Nchi za Afrika *(constituencies*) zenyewe zichague na zifanye uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata wasiwasi kuwa marekebisho haya yasiwe chachu ya *IMF* kuongeza masharti yasiyofuata mazingira ya Nchi za Afrika kama ilivyozoeleka. Kamati ilibaini kuwa awali masharti ya *IMF* yalikuwa ni muhimu kutokana na mikopo iliyokuwa inatoa. Marekebisho ya Uchumi wetu *(Economic Reforms)* yalikuwa ni lazima ingawaje yalihitaji yafanyike hatua kwa hatua. Hivi sasa *IMF* haitoi fedha za bajeti bali zinasaidia katika kuboresha urari wa malipo (*balance of payment*) na kufuatilia Sera za Uchumi jumla *(Macro Economic Policies)* zinazoathiri viwango vya ubadilishaji wa fedha (*exchange rates).* Utaratibu uliopo sasa ni kuwa hakuna Nchi yoyote ya Afrika inayoweza kupata mikopo au misaada kutoka Benki ya Dunia au Wahisani wengine bila ya *IMF* kusema. *IMF* inabakia kuwa chombo muhimu cha kuunganisha Nchi Wanachama na vyanzo vya misaada na mikopo; kwa kuzingatia kura asilimia 3.01 ya Nchi 20 (*Anglophone*) za kura zote na asilimia 1.35 (*Francophone*) ya Nchi zile nyingine 23 watakaotafuta ridhaa ya nchi zetu kusaidiwa mathalani kutoka Marekani yenye asilimia 16.77 ya kura zote. Ndio maana hata Tanzania inayotekeleza mipango ya *Policy Support Instrument* bado tunategemea *IMF* kupeleka mbele hoja zetu, baada ya kuthathmini maendeleo ya Sera zetu za Uchumi na Kijamii. Hakuna Nchi Duniani inayotekeleza mipango yake ya Uchumi au Kijamii bila kuihusisha kwa njia moja au nyingine *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashawishika kuona kuwa marekebisho haya ni mlolongo wa kubadili na kurekebisha vyombo hivi vya Kimataifa Duniani. Hivi sasa Nchi zetu hususan Tanzania, tunaposhirikiana na *IMF* lazima tuwe na '*Letter of Intent'* ambayo inaonyesha yale tutakayokubaliana nayo tunayaidhinisha wenyewe na kuacha mapendekezo tusiyokubaliana nayo. Nchi za Afrika mara nyingi huwa na vikao na *IMF* na Benki ya Dunia ili kutoa kauli za Majimbo hayo mawili *(Anglophone na Fracophone).* Hapo awali, Nchi tajiri hususan Marekani haikukubali hata kidogo kuchunguzwa mwenendo wake wa Sekta ya Kifedha; baada uchumi wake kuathirika kutokana na mtikisiko wa uchumi Duniani, hivi sasa wamekubali kuchunguzwa chini ya Mpango wa

*Financial Sector Assessment Programme (FSAP*) inayohusisha kuangalia ufanisi wa Mabenki, Taasisi za Bima, Pensheni na Soko la Mitaji katika Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya fundisho tulilolipata kutokana na msukosuko wa Sekta ya Fedha uliotokea duniani pamoja na kudorora kwa Uchumi, ni ushirikishwaji dhaifu katika utekelezaji na utoaji maamuzi katika taasisi za kifedha Duniani pamoja na mashirika makubwa Duniani. Sote tunakubali kwamba imetambulika Dunia nzima kuwa msukosuko wa fedha duniani umeanzia kwenye nchi zilizoendelea ambao ni wanachama na washiriki wakamilifu katika taasisi husika za Kidunia pamoja na *IMF*. Ushiriki wa Tanzania na nchi zinazoendelea katika taasisi hizi, ungewezesha kabisa kujenga Kundi la Shinikizo *(Pressure Group)* la kuepukana na athari zilizojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunashuhudia Mataifa yaliyoendelea na yenye ushiriki mkubwa katika taasisi hizi, yamefikia hatua hata ya kuunda makundi kama vile G.8, G.20, pamoja na kulinda mafanikio yao ya kawaida, yanapata nguvu vile vile ya kulinda maslahi kwenye taasisi hizi za Kimataifa kama *IMF* kutokana na ushiriki wao kikamilifu. Baada ya msukosuko huo wa kifedha Duniani, hoja kubwa kati ya nyingi zilizojitokeza ni lile la kufanya marekebisho makubwa katika usimamizi wa taasisi hizi. Hoja hii, inatuhamasisha Tanzania nasi turidhie marekebisho yaliyoletwa mbele yetu juu ya *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuridhia kipengele cha marekebisho haya, kina athari zake kama ifuatavyo:-

- Kwa vile Tanzania ni mwanachama halali wa *IMF* kutokuhusishwa kwenye ushiriki na utekelezaji, kunaweza kuleta tatizo la kuwa mhanga wa maamuzi ya mwisho *(victim of residual decision making process)*;

- Inawezekana tukawa Taifa la kupokea tu maelekezo ya *IMF* na hili linatishia Utaifa wetu;

- Kwa vile moja ya tatizo letu kubwa ni uhaba wa mtaji, fedha kutoka *IMF* zinaweza zikatumika au kwa kutekeleza programmu/ mipango ambayo haitokani na utashi na mapendekezo yetu ya Kitaifa; na

- Inawezekana hata mipango yetu ya Nchi yote ya; Kiuchumi, Jamii, Kisiasa na Utamaduni ikabuniwa na vyombo hivi badala ya nchi yenyewe *(home grown vis a vis external grown ideas).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho baada ya uchambuzi wa kina wa hapo juu, Kamati inaliomba Bunge hili Tukufu liridhie Azimio hili. Utaratibu ulioelezewa katika Azimio hili utakubalika ikiwa asilimia 80 ya Nchi Wanachama wa *IMF* wakiridhia. Kamati inaipongeza Serikali kwa dhati kwa kushughulikia Azimio hili haraka; na hii ndio faida ya kutoa maamuzi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la Nchi za Kiafrika kuongezwa kauli katika uendeshaji wa *IMF* lilifikiwa mwezi Oktoba, 2009 pamoja na hoja ya mapendekezo yaliyowasilishwa. Serikali ya Tanzania kuwasilisha Azimio hili baada ya kuridhiwa na Bunge lako Tukufu itatuwezesha kukamilisha utaratibu huu kabla *”beat deadline”* ya mwisho wa mwezi Februari 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Maoni na Ushauri wa Azimio hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti na Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Dr. Anthony M. Diallo, Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Monica Ngenzi Mbega, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Damas Pachal Nakei, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Dkt. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi, Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Charles Kajege na Mheshimiwa Andrew J. Chenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Makatibu wa Kamati, Ndugu Lawrence Makigi na Michael Kadebe kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo(Mb), Manaibu Waziri, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari (Mb), Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, (Mb) na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Shija kwa utendaji wao mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na Kamati inaunga mkono Bunge hili Tukufu liliridhie Azimio hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio lililoko mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Jecha.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia siku ya leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Marekebisho ya Makubaliano ya Kimataifa (*Articles of Agreement*) yaliyoanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ili niweze kutekeleza lile ambalo Mwenyezi Mungu amenijalia nilitekeleze katika wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)*, lilianzishwa 1944 kwa malengo maalum. Lengo Kuu lilikuwa ni kusimamia mfumo wa fedha Duniani kwa utaratibu wa kufuatilia Sera za Uchumi Mpana za nchi wanachama hususan zile zinazoathiri viwango vya ubadilishaji wa fedha *(exchange rate*) na urari wa malipo *(balance of payment*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili, hulazimika kutoa ushauri wa kisera na tabaan/yumkini kwa nchi ambazo zinakabiliwa na matatizo makubwa ya kifedha, huzipatia misaada ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilijiunga na *IMF* mwaka 1962 na tangu wakati huo nchi yetu imekuwa ikipata misaada mbalimbali ya kifedha kugharamia mipango yake ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubali kwamba sera zinazotungwa na kutekelezwa na *IMF* zimekuwa ni mzigo mkubwa kwa maendeleo ya nchi hususan za ulimwengu wa tatu (zinazoendelea). Daima nchi hizi zimekuwa wahanga kutokana na utekelezaji wa sera na mipango ambayo hulazimika kuitekeleza na *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafakuri ya Azimio, katika hali ya uchumi wa kilimwengu, nchi zilizoendelea, zimekuwa ni wakopeshaji wakubwa wa viwango vikubwa vya fedha kwa nchi zinazoendelea. Kutokana na nchi zinazoendelea kujiingiza katika madeni makubwa ilhali uchumi wa nchi hizo bado haujapiga hatua nzuri, zinakuwa zimetumbukia katika dimbwi la madeni yasiyotabirika utekelezaji wa malipo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili, linatupa wasiwasi Kambi ya Upinzani pale nchi zinazoendelea zinapodhani kwamba kupigania kuongezewa kauli na ushiriki katika uendeshaji wa Shirika la *IMF* kunaweza kuwapa fursa ya kuweza kuwa na ushiriki wenye manufaa wakati wa majadiliano yanayohusu mahitaji ya nchi hizo. Ni jambo linaloeleweka wazi kwamba nchi zilizoendelea ambazo huchangia kwa kiasi kikubwa cha fedha kwenye Shirika hili ndizo zenye kura nyingi. Maana yake ni kwamba nchi zilizoendelea zina nguvu na kauli kubwa katika kupiga kura wakati wa kufanya maamuzi

mbalimbali yanayohusu Sera na Mipango ya Shirika hilo. Huu ni mgawanyo usio sawia katika kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mchango mdogo wa nchi zinazoendelea katika kupiga kura wakati wa kufanya maamuzi, ni dhahiri kwamba nchi hizo zinakuwa ni wasindikizaji tu katika maamuzi yanayofanywa na *IMF*. Kambi ya Upinzani inaona kwamba suala la msingi la kuweza kukuza nguvu ya maamuzi kwa nchi zinazoendelea, ni nchi hizo (ikiwemo Tanzania yenyewe) kukuza uchumi imara wa nchi zao ili kuepukana na mzigo wa madeni makubwa yasiyolipika. Kukua na kuimarika kwa uchumi wa nchi zinazoendelea ndio njia pekee ya kujiongezea kauli na ushiriki wenye kuleta manufaa wakati wa majadiliano yahusuyo mahitaji ya nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kuzingatia ni kujua na kukubaliana na vigezo au kanuni zinazotumika katika kupima uzito wa kura nchi mwanachama inayokuwanao. Kwa sababu ni ukweli ulio wazi kwamba madhali Tanzania tumekubaliana na Kanuni za mchezo, hatuna sababu za msingi za kukataa matokeo ya mchezo wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa nchi zilizoendelea, zitaendelea kuwa na sauti kubwa katika mchakato wa utunzi wa Sera za *IMF* na kadhalika katika upigaji kura zenye kutoa maamuzi. Kutokana na kadhia hiyo, wakati mwingine baadhi ya nchi zinazoendelea hulazimika kujitutumua na kutokubali kulazimika kufuata Sera za *IMF* pale inapoona mazingira ya nchi yao hayaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Nchi ya Malaysia, kwa mfano kwenye miaka ya 1997 – 2000 ilipokuwa katika kipindi kigumu cha uchumi, ilikataa katakata kukubaliana na Sera za *IMF* za kurekebisha uchumi wa nchi yao, badala yake walitumia sera zao za ndani kulingana na mazingira yanayowakabili. Hatimaye walifanikiwa, jambo lililoipelekea *IMF* kukiri baadaye kwamba ilitoa ufumbuzi ambao usingeleta suluhu kwa uchumi wa Malaysia wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha wa Malaysia wakati huo Mohamed Yakcop, katika tambo zake alisema na ninanukuu:-

*"In a situation where there are many complex trade – offs, it is useful to think outside the box and seek new or extra policy tools"* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema kwamba mazingira ya nchi zinazoendelea kwa sasa sio sawa na mazingira ya nchi hizo wakati zinajiunga na *IMF*. Hivyo basi, ni muhimu kwa nchi hizo kuwa na mtazamo wa kisera tofauti na ule uliowekwa miaka iliyopita wakati wa uanzishwaji wa Shirika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio, Ibara ya 5(12)(h), kinachopendekeza marekebisho yatakayoiwezesha *IMF* kutumia fedha za wanachama zilizoko Akaunti Maalum *(Special Disbursement Account)* kuwekeza kwa kadri itavyoona inafaa kulingana na Kanuni na taratibu zilizopitishwa na *IMF*.

Tumeelezwa kwamba riba itokanayo na uwekezaji huu itawekwa katika Akaunti Maalum na hivyo kuifanya akaunti hiyo kuwa endelevu. Nchi zinazoendelea zinapaswa kuwa macho katika utekelezaji wa marekebisho haya kwani isiwe ni janja ya nchi tajiri wanachama kutaka kuchukua fursa hii kuitumia *IMF* kuwafanyia biashara zaidi na nchi maskini kwa kisingizio cha uwekezaji na hivyo kunyonya rasilimali za nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yanayofanywa katika Ibara ya 12(3)(e), ni kwamba kila Mkurugenzi Mtendaji katika Majimbo mawili ya Bara la Afrika ya *(Anglophone na Francophone),* atateua Wakurugenzi wenza ambao watakuwa na mamlaka kamili ya kumwakilisha Mkurugenzi katika kazi mbalimbali. Lakini kifungu hicho hicho kinaweka bayana kwamba Wakurugenzi wenza hawatahusika katika Upigaji kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kusaidia nchi wanachama katika Bara letu la Afrika kuongeza ushiriki na kauli tu na sio kuongeza nafasi katika upigaji kura. Kwa maana nyingine ni kuongeza nafasi ya ushawishi. Kambi ya Upinzani, inaona kwamba njia pekee kwa nchi za Kiafrika kujinasua na mikiki ya *IMF,* ni kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi hizo kwa kuandaa na kufuata sera kwa mujibu wa mazingira ya nchi zao. Uchumi unapoimarika na sauti ya nchi nayo huimarika. Kimsingi Kambi ya Upinzani haina pingamizi kwa Bunge lako Tukufu kupitisha Azimio hili, hasa pale inapoonekana maslahi ya nchi yanalindwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jecha kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu azimio hili.

Waheshimiwa Wabunge, hapa Mezani kwangu sijapata jina la mchangiaji hata mmoja kuhusu Azimio hili.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Manaibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari na timu yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni muhimu sana hasa kwa maendeleo ya Afrika. *IMF* hujenga maamuzi mazito na yanayosaidia au kuathiri nchi za Afrika endapo maamuzi hayo siyo makini. Pamoja na kutokuonekana moja kwa moja kwa utajiri wa Afrika kipesa, lakini ukweli ni kwamba nchi hizo ndizo zinazochangia rasilimali nyingi mfano madini na maliasili nyingine kama pembe za ndovu na mafuta katika uchumi wa dunia. Hali kadhalika, kutokana na nchi hizo kuishi kwa kutegemea mikopo toka nje na misaada, zimebaki kuwa mchangiaji mkuu wa riba na wakati mwingine kuchelewa katika kuamua vipaumbele vyake kutokana na masharti magumu yanayowekewa na *IMF*.

Ongezeko la kura au ushiriki wa wadau, utaisaidia kuongeza sauti na uwakilishi katika Jumuiya hiyo na hivyo tunatarajia ongezeko la tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Bunge letu Tukufu Kuridhia Mapendekezo ya Mabadiliko katika baadhi ya Vipengele vya Mkataba ulioanzisha Shirika la Fedha la Kitaifa *(IMF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania, ni miongoni mwa nchi zinazoendelea ambazo hazina kauli katika Shirika la *IMF*. Hata hivyo, tumekuwa tukipokea misaada/ mikopo toka *IMF* kusaidia kupunguza umaskini na kukuza uchumi, baada ya wakubwa wenye sauti kukubaliana. Hali ambayo imekuwa ikiifanya nchi yetu kuwa mhanga wa Sera za *IMF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa nchi za Kiafrika ikiwemo Tanzania zimepeleka maombi ili nchi zetu ziongezewe kauli na ushiriki wake kwa *IMF* hali inayotarajiwa kuboresha hali yetu kiuchumi. Nachukua nafasi hii, kuunga mkono kwa dhati kwamba tukubaliane na maombi haya ili tuongeze uwakilishi wetu katika chombo hicho ili tupate huduma nzuri zaidi. Nchi yetu bado ina mapambano makubwa ya kutokomeza umasikini walau kuupunguza, tukipitisha Azimio hili tunaweza kupata ahueni kwa hali bora ya Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Napendekeza utaratibu uangaliwe tena hapo baadaye kuona uwezekano wa kuzipa sarafu zetu thamani toka mwaka hadi mwaka badala ya kupungua kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Sasa ninaomba nimwite mtoa hoja ili aweze kusema machache na kuhitimisha hoja yake ili Bunge liweze sasa kuiamua, mtoa hoja!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana *subject* ilikuwa *tough*.

Kwanza nataka nianze kuwashukuru wale wote ambao wamechangia. Nikianza na wale ambao wamechangia kwa maandishi Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Pindi Chana. Lakini vile vile nataka niwashukuru kwa dhati wale ambao wamechangia kwa kuongea nikianza na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na vile vile ndugu yangu, *school mate* wangu Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha. Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme machache kwa sababu wote waliochangia, waliochangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa maandishi, wameunga mkono hoja. Sina haja ya kusema mengi. Nataka niseme machache tu. Azimio hili lina mambo mawili tu makubwa na mambo hayo mawili tumeyaomba sisi wenyewe Waafrika, ningeshangaa ningeona Bunge letu hili halijaridhia. La kwanza

tuliona kwamba Waafrika katika Bodi ya *IMF* hatuna kauli nzito kwa maana ya uwakilishi wetu ni mdogo. Waafrika kwa pamoja tukasema nchi 20 za *Anglofone* zinapeleka mwakilishi na msaidizi mmoja kwenye Bodi wakati Marekani nchi moja anapeleka mwalikishi mmoja. Tukataka nguvu zaidi tupeleke wawakilishi wengi zaidi lakini wenzetu baada ya kutafakari wameongeza nafasi mbili za ziada. Hili tumelipeleka wenyewe Waafrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nalishukuru sana Bunge lako Tukufu, kwa wote waliochangia na wasiochangia kuridhia Azimio hili. Lakini la pili ambalo nataka niliseme ni kwamba kulikuwa na utaratibu ndani ya *IMF* unapotaka kutumia fedha za Marekani kwa mfano katika kuwekeza nchi inayoendelea, sharti *IMF, the Board of Directors,* wapate ridhaa ya Marekani mwenye pesa zake. Tukaona jamani sisi huku tunasumbuka sana kama Waafrika ambao tunahitaji zile fedha tuweze kuwekeza katika nchi zetu. Tukasema sisi kama Waafrika, hakuna haja tuipe Bodi ya *IMF mandate* wakihisi kwamba ziko fedha hapa ziwekezwe katika nchi fulani basi wao waridhie waje wawekeze badala ya kwenda kuwaomba nchi yenye fedha zao. Hii tukaona kidogo itatusaidia sisi kama Waafrika ambao ndiyo tunahitajia fedha nyingi zaidi katika kuwekeza katika nchi zetu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu nakubaliana na mawazo ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Kigoda, nakubaliana na mawazo ambayo yamezungumzwa na ndugu yangu pale Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha ili tuweze kujizatiti kuondokana na sera za *IMF,* kuondokana na kutegemea zaidi ya *IMF,* tujidhatiti katika kuimarisha uchumi wetu. Nataka niseme mbele ya Bunge lako, Kilimo Kwanza kama kweli tutajidhatiti kwa kauli moja kwa maelekezo ambayo yanatolewa na Serikali, tutaondokana na huu utegemezi, inawezekana tusiondokane nao kesho, lakini kesho kutwa na mtondogoo, tutajikuta tumeondokana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kutumia vema rasilimali zetu, bado hatujatumia rasilimali tulizonazo katika bahari, mito na maziwa. Tukizitumia vema rasilimali hizi, tunaweza tukapata mapato mengi, tukainunua uchumi wetu, tukaondokana na utegemezi, tukaondokana na sera hizi ambazo sisi tunaona kama ni changamoto kwetu. Lakini nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, *IMF* iliyokuwa miaka ya 1970 na 1980 siyo *IMF* iliyoko sasa hivi miaka 2000. Sasa hivi *IMF* wanakuja, tunakaa nao, tunashauriana, tusilolitaka tunawaambili hatulitaki, tunalotaka, tunasema tunarekebisha, kwa kweli sasa hivi na wao wamekuwa wasikivu. Bila ya sisi hawana kazi, kwa hiyo, lazima watusikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nataka nitoe shukrani za dhati kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi na kwa niaba ya mwenzangu Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa wale Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuliunga mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa hoja na hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge naomba kuwatangazia kwamba Bunge lote limeafiki Azimio hili, sasa limepitishwa rasmi na Bunge na hivyo tuwaombe na kuwatakia kila la kheri Mawaziri wetu wakatusaidie kusimamia marekebisho haya kwa manufaa ya nchi yetu, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Azimio linalofuata, Katibu.

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya Mabadiliko katika baadhi ya Vipengele vya Mkataba ulioanzisha Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) liliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(The Agreement on the Establishment of Zambezi Water Course Commission – (ZAMCOM)***

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na hatimaye liridhie Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(The Agreement on the Establishment of the Zambezi Watercourse Commission).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba niungane na Watanzania wenzangu katika kutoa rambirambi zetu kwa Mheshimiwa Vita Kawawa na familia yote, kwa kifo cha Mwasisi wa Taifa letu, Simba wa Vita, Mzee wetu, Mzee Rashid Mfaume Kawawa. Kumuenzi Mzee wetu, ni vema tukasimama juu ya misingi aliyotuachia, tena kwa vitendo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Mzee wetu Mahali Pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, imelipitia kwa undani Azimio hili na imelikubali na kulipitisha. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala na Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** nchi nane (8) ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC)* zinachangia Bonde la Mto Zambezi lenye eneo la kilomita za mraba 1,351,365 ambalo lina jumla ya wakazi wapatao milioni 31. Eneo ambalo kila nchi inamiliki katika Bonde hilo, kwa asilimia, ni kama ifuatavyo: Angola asilimia (17.4), Botswana (asilimia 0.9), Namibia (asilimia 1.3), Zambia (asilimia 42.5),

Zimbabwe (asilimia 15.8), Malawi (asilimia 8), Tanzania (asilimia 2.1) na Msumbiji (asilimia 12).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania huchangia asilimia 53 ya maji yote yanayoingia kwenye Ziwa Nyasa kupitia Mito ya Kiwira, Ruhuhu, Songwe na Lufilyo, wakati Malawi huchangia asilimia 43 na Msumbiji asilimia 4 tu. Kupitia Mto Shire, Ziwa Nyasa huchangia maji kiasi cha mita za ujazo 20 bilioni kwa mwaka kwenye Mto Zambezi wenye jumla ya mita za ujazo 94 bilioni. Pamoja na kuwa na eneo dogo kwenye Bonde, Tanzania huchangia kiasi cha asilimia 11.3 ya maji yote ya Mto Zambezi. Hii inatokana na kwamba Tanzania kuwa na wastani wa mvua nyingi kwa mwaka kuliko nchi nyingine yoyote katika Bonde hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ili kuboresha uhusiano uliopo na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa baina ya nchi wanachama, nchi za Bonde zimeanzisha ushirikiano katika kuhifadhi, kuendeleza na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwenye mabonde ya mito na maziwa kwa kuunda Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(ZAMCOM).* Kuundwa kwa *ZAMCOM*, ni utekelezaji wa Itifaki ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Majishirikishi *(The Revised SADC Protocol on Shared Watercourses),* iliyosainiwa na Wakuu wa Nchi za *SADC* mwezi Agosti, 2000 huko Windhoek, Namibia na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 7 Agosti, 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ushirikiano katika matumizi ya majishirikishi baina ya nchi za Bonde la Mto Zambezi ulianza mwaka 1987 kupitia Mpango wa Zambezi wa Utekelezaji *(Zambezi Action Plan - ZACPLAN)* wenye miradi 19. Kati ya miradi hiyo, Mradi Na. 6 (*Zambezi Action Plan Project – ZACPRO 6)* wenye awamu mbili *(ZACPRO 6.1* na *ZACPRO 6.2)* ndio uliopewa kipaumbele. *ZACPRO 6.1*, ambao umekamilika, ulihusu ukusanyaji wa takwimu za rasilimali za maji na utayarishaji wa benki ya takwimu ya rasilimali hizo (*hydrometeorological databas*e) na pia kufanya uchunguzi katika sekta sehemu zinazohusiana na matumizi ya rasilimali za maji. Awamu ya pili ya mradi (*ZACPRO 6.2)* ambao nao pia umekamilika, ilianza kutekelezwa mwaka 2001 kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa maji na kuzuia athari zinazoletwa na mafuriko, ukame, uchafuzi wa vyanzo vya maji, na uharibifu wa mazingira katika Bonde la Mto Zambezi. Tanzania inashirikiana na nchi wanachama katika matumizi ya takwimu zilizokusanywa chini ya mradi kwa ajili ya usimamizi thabiti wa rasilimali za maji katika Bonde hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuandaliwa kwa Azimio la kuunda Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(ZAMCOM),* kunatokana na uamuzi wa nchi za Bonde hilo wa kuunda Kamisheni ya Maji yenye lengo la kuimarisha ushirikiano wa kuwa na rasilimali za maji endelevu, na zenye ubora unaokubalika na pia, kuwa na matumizi yenye uwiano kulingana na mahitaji ya kila nchi mwanachama. Kuanzisha *ZAMCOM* ni moja ya hatua muhimu za utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 ambayo inaitaka nchi yetu kukuza ushirikiano miongoni mwa nchi zinazotumia majishirikishi ili kuhifadhi, kuendeleza na kusimamia matumizi ya maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Mkataba wa kuunda *ZAMCOM* ulisainiwa na Mawaziri wa Maji wa nchi saba za Bonde la Mto Zambezi huko Kasane, Botswana tarehe 13 Julai, 2004. Nchi ya Zambia bado haijasaini Mkataba huo kwa sababu bado inaifanyia mapitio Sera yake ya Maji, pamoja na kutengeneza Mkakati wa kusimamia rasilimali za maji na kutunga Sheria ya usimamizi wa rasilimali za maji. Hata hivyo, Zambia tayari imeridhia Itifaki ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Majishirikishi. Itifaki hiyo ndiyo chimbuko la kuanzisha Kamisheni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu muhimu vya mkataba, Mkataba wa *ZAMCOM* una jumla ya vifungu ishirini na sita (26). Baadhi ya vifungu hivyo ni kama ifuatavyo:

(i) Madhumuni na majukumu ya Kamisheni (Kifungu Na. 5). Madhumuni ya *ZAMCOM* ni kusimamia na kuendeleza rasilimali za majishirikishi ya Bonde la Mto Zambezi na kuhakikisha kuwepo kwa matumizi endelevu na yenye uwiano.

Majukumu ya *ZAMCOM* ni pamoja na yafuatayo:-

- Kukusanya, kutathmini na kusambaza takwimu na taarifa kuhusu Bonde la Mto Zambezi;

- Kuzishauri nchi wanachama katika kupanga, kusimamia, kutumia, kuendeleza, kuhifadhi na kulinda rasilimali asilia za Bonde; na

- Kutoa ushauri kuhusu hatua za kuchukua katika kupata ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya maji.

(ii) Vyombo vya Kamisheni (Kifungu Na.6) *ZAMCOM* itakuwa na vyombo vya kitaasisi vifuatavyo:-

- Baraza la Mawaziri: Kila nchi itawakilishwa na Waziri mwenye dhamana ya maji;

- Kamati ya Ushauri wa Kitaalam: Kamati hii itakuwa na wajumbe watatu kutoka kila nchi mwanachama na idadi ya washauri kadri kila nchi mwanachama itakavyoona inafaa; na
- Sekretarieti: Itakuwa na Katibu Mtendaji, Wataalam na Maafisa Utawala (kwa idadi kama itakavyoamuliwa katika nyakati mbalimbali).

(iii) Matumizi yenye Uwiano ya Rasilimali za Maji (Kifungu Na. 13)**.** Kifungu hiki kinaweka taratibu zitakazohakikisha kuwepo kwa matumizi yenye uwiano ya rasilimali za maji.

(iv) Mipango ya Utekelezaji wa Miradi (Kifungu Na. 16). Nchi mwanachama itakayokuwa na mpango au kusudio lolote la kutekeleza mradi au shughuli yoyote itakayohusu majishirikishi ya Bonde itawajibika kutoa taarifa kwa Sekretarieti ya *SADC*

na kupeleka takwimu na taarifa husika kwenye Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi kuhusu mipango hiyo kabla ya kuanza utekelezaji.

(v) Kutotekeleza Makubaliano (Kifungu Na. 20). Kifungu hiki kitatumika kuwajibisha nchi mwanachama ambayo haitatekeleza makubaliano ya Mkataba wa *ZAMCOM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuridhia mkataba; matokeo ya utekelezaji wa makubaliano hayo kwa nchi yetu ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kupatikana kwa takwimu za kutosha na zilizo bora kuhusu rasilimali za maji katika Bonde;

(ii) Kuwepo kwa uratibu wa pamoja wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Bonde; na

(iii) Kuwa na mipango shirikishi ya matumizi, uendelezaji na hifadhi ya rasilimali za maji katika Bonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kujiunga; nchi zilizo kwenye Bonde la Mto Zambezi zinaweza kuwa wanachama kwa kuridhia Mkataba wa *ZAMCOM* kwa mujibu wa taratibu za kikatiba za nchi husika. Ili Tanzania iweze kujiunga, inabidi Mkataba huo ujadiliwe na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** gharama za kujiunga; gharama ambayo nchi yetu itatakiwa kulipia kwa kutenga fedha kila mwaka katika Bajeti ya Serikali ni kwa ajili ya mambo yafuatayo:-

(i) Mchango wa kila mwaka wa uanachama kwa kiwango kitakachopangwa na kukubalika katika vipindi tofauti na nchi wanachama baada ya kuridhia mkataba huo; na

(ii) Mchango wa Dola za Marekani elfu ishirini na tano ($25,000) kwa mwaka utakaotolewa na kila nchi mwanachama kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Sekretarieti ya mpito itakayosimamia utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni kabla ya nchi wanachama kuridhia Mkataba wa Ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishaji wa wadau; katika kuandaa Azimio hili, wadau walioshirikishwa ni pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara za Katiba na Sheria; Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Kilimo, Chakula na Ushirika; Viwanda, Biashara na Masoko; Nishati na Madini; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje. Wadau hao wanaafiki uridhiaji wa Mkataba wa *ZAMCOM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ratiba ya utekelezaji; hadi sasa nchi nne (4) kati ya nane (8) ambazo ni Angola, Botswana, Msumbiji, na Namibia zimeridhia Mkataba wa kuunda Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(ZAMCOM).* Tanzania ikiridhia mkataba huo itakuwa ni nchi ya tano na hivyo kuiwezesha *ZAMCOM* kuanza kufanya kazi. Katika kipindi cha mpito, nchi ya Botswana imekubali kuchukua jukumu la kuwa makao makuu ya muda ya Sekretarieti ya *ZAMCOM* pamoja na kugharamia wafanyakazi waliopo (*supporting staff*) wakati nchi wanachama zilizobaki zikiendelea na utaratibu wa kuridhia Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi - ZAMCOM, kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** nchi Nane (Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Tanzania na Msumbiji) ambazo zinachangia Bonde la Mto Zambezi, lenye eneo la kilomita za mraba takribani milioni moja na laki tatu na hamsini na moja elfu na jumla ya wakazi wapatao milioni thelathini na moja;

**KWA KUWA** Tanzania huchangia asilimia kumi na moja nukta tatu ya maji yote ya Mto Zambezi;

**KWA KUWA** kwa lengo la kuboresha uhusiano uliopo na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa baina ya nchi wanachama, nchi za Bonde hilo zimeanzisha ushirikiano katika kuhifadhi, kuendeleza na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji katika mabonde ya mito na maziwa kwa kuunda Kamisheni ya Maji ya Mto Zambezi (*The Zambezi Watercourse Commission – ZAMCOM)*;

**KWA KUWA** kuundwa kwa ZAMCOM ni utekelezaji wa Itifaki ya Majishirikishi ya SADC *(The Revised SADC Protocol on Shared Watercourses*) iliyosainiwa na Wakuu wa Nchi za SADC mwezi Agosti mwaka 2000 mjini Windhoek – Namibia na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Agosti mwaka 2003;

**KWA KUWA** nchi za *SADC* zinatumia maji ya Bonde la Mto Zambezi kwa shughuli mbalimbali zikiwemo kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na utalii, uzalishaji wa umeme na shughuli nyingine za viwanda;

**KWA KUWA** Ibara ya 5 ya Mkataba huu inaainisha majukumu ya Kamisheni kuwa ni:-

1. Kukusanya, kutathmini na kusambaza takwimu na taarifa kuhusu Bonde la Mto Zambezi;

2. Kukuza takwimu na kuratibu uendelezaji wa rasilimali za maji katika Bonde la Mto Zambezi;

3. Kuzishauri nchi wanachama katika kupanga, kusimamia, kutumia, kuendeleza, kuhifadhi na kulinda rasilimali asilia za Bonde la Mto Zambezi;

4. Kukuza ufahamu na ushirikishaji wa wananchi wa Bonde la Mto Zambezi katika usimamizi bora wa rasilimali za majishirikishi; na

5. Kutoa ushauri kuhusu hatua za kuchukua katika kupata ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya maji.

**KWA KUWA** *ZAMCOM* itasimamiwa na vyombo vya Kitaasisi ambavyo ni Baraza la Mawaziri, Kamati ya Ushauri wa Kitaalam na Sekretariati, vitakavyoundwa na Mawaziri na Wataalam toka Nchi Wanachama;

**NA KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafaidika na mambo yafuatayo:-

1. Kupatikana kwa takwimu za kutosha na zilizo bora kuhusu rasilimali za maji katika Bonde;

2. Kuwepo kwa uratibu wa pamoja wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Bonde;

3. Kuongezeka kwa kiwango cha elimu na ujuzi kwa wananchi hususan, wale watakaokuwa wanatekeleza miradi katika Bonde kwa kutumia teknolojia za kisasa;

4. Kuongezeka kwa ajira kutokana na kutekelezwa kwa miradi mbalimbali katika Bonde;

5. Kuongezeka kwa pato la Taifa kutokana na mauzo ya bidhaa au huduma zitakazotolewa katika Bonde hilo;

6. Kudhibitiwa kwa uchafuzi wa mazingira katika Bonde;

7. Kuwa na mipango shirikishi ya matumizi, uendelezaji na hifadhi ya rasilimali za maji katika Bonde; na

8. Kushiriki katika ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya rasilimali za maji ili kuimarisha ujirani mwema na amani kati ya nchi za *SADC*.

**KWA KUWA** ushirikiano baina ya nchi zilizomo katika Bonde la Mto Zambezi utaimarika zaidi iwapo nchi zote za eneo la Bonde hilo zitakuwa wanachama;

**NA KWA KUWA** kuridhiwa kwa Mkataba huo kutaiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na nguvu zaidi za kiushawishi katika kuleta ushirikiano wenye lengo la kuzipatia faida au manufaa Nchi Wanachama kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika Mkataba wa *ZAMCOM.*

Hivyo basi, kwa kuzingatia umuhimu wa Kamisheni hii na manufaa ambayo wananchi watapata, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kumi na Nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya 2, sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(The Agreement on the Establishment of the Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, naomba kutoa hoja *(Makofi).*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba nichukue nafasi hii kusoma ama kuwasilisha kwako maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi, ama *The Agreement on the Establishment of the Zambezi Watercourse Commission – ZAMCOM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(ZAMCOM)*, kama ilivyoainishwa na Kanuni ya 114 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa Kamati yangu imepata nafasi ya kutoa maoni ya Kamati kwa mara ya kwanza katika Mkutano huu wa kumi na nane wa Bunge, nachukua nafasi hii kukutakia wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti, Waheshimiwa Wabunge wote, Katibu wa Bunge na Watumishi wote kila kheri katika Mwaka huu wa 2010. Aidha, natoa pole za dhati kwa familia ya Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Vita R. Kawawa na Watanzania wote, kwa kuondokewa na Mzee wetu, Simba wa Vita, Hayati Rashid Mfaume Kawawa, Kiongozi aliyetumikia nchi yetu kwa uadilifu mkubwa. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi , Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata muda wa kutosha kupitia na kujadili hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa

Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi. Mkataba huu unazihusisha nchi nane (8) wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* ambazo ni Angola, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia, Zambia, Zimbabwe na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madhumuni na manufaa ya Kuridhia Mkataba. Tarehe 7 Oktoba, 2009 Kamati ilikutana Dar es Salaam na Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandosya na kupokea maelezo na ufafanuzi kuhusu Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa na Bunge. Kamati ilielezwa kuwa madhumuni ya kuanzishwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi ni kuimarisha ushirikiano wa kuwa na rasilimali za maji endelevu na zenye ubora unaokubalika na pia kuwa na matumizi yenye uwiano kulingana na mahitaji, kwa kuzingatia misingi ya haki, busara pamoja na usimamizi wenye kuzingatia tija kwa manufaa ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Maji na Umwagiliaji aliendelea kuieleza Kamati kuwa iwapo Bunge litaridhia Azimio hili, nchi yetu itapata manufaa yafuatayo:-

(i) Kuwa na mipango itakayowezesha kutunza na kutumia kwa kiwango cha juu rasilimali maji ya Bonde la Mto Zambezi kwa manufaa ya nchi wanachama;

(ii) Kuwa na uwezo wa pamoja wa kukusanya, kuweka na kubadilishana takwimu za mtiririko wa maji na kuzuia matukio ya mafuriko, ukame na majanga mengineyo;

(iii) Kupata ushauri kuhusu mipango ya kutumia, kuendeleza, na kulinda rasilimali za Bonde la Mto Zambezi kwa kushirikiana na taasisi za nchi za *SADC* na Mashirika ya Kimataifa; na

(iv) Kupata ushauri utakaowezesha kuepuka migogoro baina yetu na nchi nyingine wanachama kuhusu mipango ya kuendeleza matumizi bora ya rasilimali maji na kuwa na maendeleo endelevu ikiwemo ulinzi wa rasilimali za Bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo, wajumbe walitoa hoja mbalimbali ambazo zilijibiwa na Mheshimiwa Waziri akisaidiwa na wataalam wa Serikali. Hoja hizo zilihusu masuala ya kisheria, kidiplomasia, mahusiano ya Kimataifa, ulinzi na usalama iwapo Mkataba huu utaridhiwa. Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu kiambatisho cha ramani katika Mkataba kilichokuwa hakionyeshi mpaka baina ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiambatisho hicho hakionyeshi dhahiri mpaka wa Tanzania, Malawi na Msumbiji katika Ziwa Nyasa, jambo ambalo Kamati ilitaka kujua kama ni kutokana na kiambatisho hicho kuwa kivuli *(Photocopy)* au ni kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kijiridhisha kuhusu vipengele vya Mkataba kama havipingani na Katiba wala Sheria nyingine za nchi, Kamati ilitaka kuona kiambatisho halisi cha Mkataba na kwamba Mkataba huu wa *ZAMCOM* hautahalalisha madai ya Malawi kuwa mpaka wake na Tanzania katika Ziwa Nyasa uko ukingo wa Mashariki mwa Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 Novemba 2009, Kamati ilikutana tena Dodoma kupata maelezo kuhusu hoja zilizotolewa na wajumbe, kikao ambacho Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema alihudhuria. Baada ya kusikiliza hoja za Wajumbe wa Kamati, Mwanasheria Mkuu wa Serikali naye aliomba akajiridhishe juu ya uhalisia wa Mkataba husika na kiambatisho cha ramani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana tarehe 28 Januari, 2010 mjini Dodoma. Katika kikao hicho Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji aliwasilisha Mkataba wenye nakala halisi ya ramani inayozingatiwa katika kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi. Kamati ilibaini kuwa suala la mpaka katika Ziwa Nyasa bado halikuwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Maji na Umwagiliaji alitoa ufafanuzi kuwa kwa utaratibu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(Southern African Development Community- SADC),* iwapo kuna utata wa mipaka baina ya nchi wanachama Mikataba yake hujiepusha na suala hilo. Ndio maana mpaka wa Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa haukuwekwa wazi, ila kilichoainishwa ni mipaka ya eneo zima litakalohusika na Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 2 Februari 2010, Kamati ilikutana tena na Waziri wa Maji na Umwagiliaji pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati ilipata maelezo kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu masuala ya kisheria katika Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa. Kwa mujibu wa maelezo yake, suala la utata wa mpaka katika ramani iliyoambatishwa na Mkataba halitaleta athari yoyote iwapo Bunge litaridhia. Isipokuwa kwamba tatizo la mpaka kati ya Tanzania na Malawi lishughulikiwe na Serikali kwa taratibu za kidiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kupata maelezo yote muhimu kuhusu suala la mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa, Kamati inakubaliana na hatua ya Serikali ya kuingia Mkataba wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi ambayo faida zake zimetajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati kwa ujumla. Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi ni mzuri na una manufaa makubwa kwa nchi yetu. Hata hivyo, ni imani ya Kamati kuwa Watanzania wanaamini kuwa mpaka wa Tanzania na Malawi unapita katikati ya Ziwa Nyasa. Aidha, suala la utata uliopo wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa linapaswa kutafutiwa jawabu la kudumu linalokubalika na nchi zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na maoni ya jumla kuhusu hoja hiyo, Kamati inatoa maoni mahsusi kama ifuatavyo:-

(i) Mkataba huu uwe kichocheo cha kuendeleza mazungumzo ya kidiplomasia kuhusu tatizo la mpaka wa Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa;

(ii) Serikali itumie fursa zinazotokana na matumizi ya maji ya Bonde la Mto Zambezi kutekeleza dhana ya Taifa ya Kilimo Kwanza katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji, uzalishaji umeme, uvuvi na shughuli nyingine nyingi ili kuinua uchumi wa nchi yetu;

(iii) Serikali iandae mipango mahsusi ya maendeleo itakayohusisha Mikoa iliyopo katika Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi, itakayowezesha kuinua uchumi wa mikoa hiyo na nchi kwa ujumla, kwa kutumia fursa zinazopatikana katika Mkataba huu;

(iv) Utekelezaji wa Mkataba huu ni mtambuka, Serikali ihakikishe kwamba Wizara zote zinazohusika na utekelezaji wa Mkataba huu zihusishwe kikamilifu bila kuiachia Wizara ya Maji na Umwagiliaji pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Napenda kuhitimisha kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati yangu. Aidha, namshukuru kwa dhati Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema; Naibu Waziri Mheshimiwa Christopher K. Chiza; Katibu Mkuu Eng. Christopher Sayi pamoja na wataalam wa Wizara kwa ufafanuzi wa kina wa hoja zilizojitokeza na hatimaye Kamati kukubali ombi la Serikali la kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nawashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini mkubwa na ushirikiano walioutoa katika kufanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo: Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti; Mheshimiwa Mussa A.Zungu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mjumbe; Mheshimiwa Col. Mstaafu Saleh A.Farrah, Mjumbe; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mjumbe; Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mjumbe; Mheshimiwa Hassan C. Kigwagilo, Mjumbe; Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mjumbe; Mheshimiwa William J. Kusila, Mjumbe; Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mjumbe; Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mjumbe; Mheshimiwa Dokta John S. Malecela, Mjumbe; Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mjumbe; Mheshimiwa Col. Mst. Feteh S. Mgeni, Mjumbe; Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Dokta. Ibrahim S. Msabaha, Mjumbe; Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mjumbe; Mheshimiwa Thomas A Mwang'onda, Mjumbe; Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mjumbe; Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mjumbe; Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Dokta Thomas D. Kashillilah, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge akiwemo Katibu wa Kamati hii Ndugu Stella Mlambo kwa kufanikisha shughuli za Kamati kwa wakati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba, Kamati yangu inaunga mkono Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa

Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(The Agreement on The Establishment of Zambezi Water Commission- ZAMCOM).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa heshima na taadhima, kuwasilisha maoni haya. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM -MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kuweza kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani ya kuridhiwa kwa Mkataba wa Kuanzishwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(The Agreement on The Establishment of Zambezi Water Commission- ZAMCOM).* Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni ya 86 (6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mkataba wa Uanziswaji wa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi *(The Agreement on The Establishment of Zambezi Water Commission- ZAMCOM),* Kambi ya Upinzani inaona kuwa jambo hili ni mwendelezo wa ushirikiano wa Kikanda kwa Nchi Wanachama wa *SADC* na hilo ni jambo la kupongezwa na kuharakishwa kwa kila kinachotakiwa. Kwani ukiangalia kwa makini moja kati ya vyanzo vikuu vya mto Zambezi ni Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, utunzaji endelevu wa Ziwa Nyasa, maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi oevu, ambayo ni chanzo kikuu cha maji cha ziwa hilo jambo ambalo utunzaji wa rasilimali asili ya vizazi vijavyo kwa ajili ya nchi zote zinazofaidika na uwepo wa ziwa hilo. Kambi ya Upinzani baada ya kuupitia Mkataba huu, inapenda kufahamu ni kwa nini nchi ya Zambia imeshindwa kusaini Mkataba huu wakati nchi hiyo inatumia maji ya Mto Zambezi kwa uzalishaji umeme katika maporomoko ya Kaborabasa na Ziwa Kariba. Aidha, katika Ibara ya 20, pale mwanachama anaposhindwa kutekeleza wajibu wake katika mambo yaliyokubaliwa, Mkataba hauoneshi nini kinafanyika kwa nchi husika. Hivyo basi, Mkataba ulitakiwa uweke wazi suala hili badala ya kusema Sekretarieti italifikisha suala hilo kwenye Baraza kwa maamuzi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kuwepo kwa utata wa mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika ziwa Nyasa na kutopatiwa ufumbuzi hadi leo. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, Rais wa Malawi ndio Mwenyekiti, wa *AU,* ni wakati muafaka sasa wa kurekebisha dosari hiyo kwa njia za kidiplomasia hasa ukizingatia rasilimali zinazopatikana ndani ya Ziwa hilo zikitumika vibaya na nchi mojawapo zinaweza kupelekea kutoelewana na hivyo kuwa chanzo cha machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo kama nchi ya Malawi itaingia Mkataba kwa kutoa leseni kwa meli ya kuvua kutoka nchi ya Malawi na meli hiyo ikavua hadi kandokando mwa nchi ya Tanzania, Tanzania ikiikamata meli hiyo na kuwafungulia mashtaka kama ilivyotokea hivi karibuni kwa meli iliyokamatwa katika bahari kuu, eneo la Tanzania, je, huo si ndio mwanzo wa kutoelewana baina yetu na Malawi? Ili kuondoa

uwezekano huo kutokea ndio sababu kubwa ya sisi Kambi ya Upinzani kutufanya tuzidi kuishauri Serikali juu ya uharakishaji wa suala hilo la mpaka kati ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona ili kuongeza umakini na uwajibikaji kwa nchi mwanachama, kulinda na kutekeleza yale yaliyokubaliwa ni bora adhabu kwa nchi husika ziwekwe wazi kwenye Mkataba. Kwani suala hili la maji na suala la mazingira kwa ujumla wake, kwa upana wake linahusu uhai wa wananchi wa nchi mwanachama kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi naomba nisimame kwa unyeyekevu nikimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili na mimi nichangie katika Azimio hili ambalo limeletwa kwetu na Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa 17 wa Bunge lako, Azimio hili lilikuja mbele yetu na mimi nilipata fursa ya kuchangia pia azimio hili. Bado sijaelewa kwamba sababu zilizofanya Azimio hilo lirudishwe, nilifikiri kwamba tungeelezwa ni kwanini lile Azimio baada ya kulichangia liliambiwa lirudi kwamba lilikuwa na matatizo. Nikiangalia nyaraka nilizonazo ndizo nyaraka zilezile ambazo tulizitumia wakati ule wakati wa kulijadili Azimio hili. Kulikuwa na nini wakati ule na sasa kuna nini? Kwa sababu sijaona badiliko lolote la nukta wala la ramani wala la kitu gani. Kulikuwa na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya tusije tukawa tunachangia mambo yetu binafsi, tunaacha mambo yanayogusa umma. Tuelezwe, kulikuwa na mkono wa mtu wa kushinikiza kwamba Azimio hilo lisipite? Kwa sababu sijaona mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee juu ya suala zima tunalozungumza. Tulikuwa tunazungumzia juu ya Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi, hatukuwa tunazungumza mpaka wa Tanzania na Malawi na bonde halina mipaka wala bonde halijui hii ni nchi gani, hii ni nchi gani, maudhui yote yalikuwa ni bonde la Mto Zambezi. Kwa nini tuliingiza habari za mpaka? Labda Serikali ingetwambia sasa ni kwa nini tuliingiza habari za mpaka. Katika ramani yangu inaonesha mpaka wa bonde la Zambezi ni upi, ndio tulichokuwa tunakijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayazungumza haya kwa sababu. Kwanza katika ile itifaki ya *SADC* kifungu cha 6, kinaonesha wazi kwamba katika maji shirikishi ni namna gani kama tutakuwa na migogoro tutayatatua kwa kupitia ile itifaki. Kwa hiyo, sioni hoja ya kusema tuna tatizo la mpaka wakati kifungu namba 6 cha protokali ya *SADC* kinaonesha wazi *lee way* ni ipi katika kutatua migogoro katika maji shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ikumbukwe wazi kwamba baada ya mwaka 2000, baada ya kuridhia na bahati nzuri Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyesaini yale makubaliano ya Kasane ya Botswana, alikuwa ni Mheshimiwa Diallo kwa niaba ya Waziri wa Maji

wakati huo, Ndugu Ngoyai Lowassa. Kwa hiyo nilitegemea kwa sababu ni mjumbe kwenye Kamati kule angekuwa ameisaidia Kamati kwamba ni kwa nini tulifikiri ni vema tukauridhia mapema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nieleweke wazi kwamba tunakuza baadhi ya mambo ambayo hayana msingi kwa kweli. Ilipaswa turidhie toka mwanzo kwa sababu sasa hivi kama tutaanza, nataka Serikali iniambie ni vijana wangapi wa Kitanzania watakuwa Botswana tayari kujiunga na Sekretarieti? Tutakuwa hatujachelewa? Nataka Serikali iniambie ni miradi mingapi ambayo sisi tutapata kama Watanzania? Sisi tunachangia 11.3% ya maji yote yanayokwenda kwenye bonde la Mto Zambezi. Sio hilo, tayari sisi tunafaidika na bonde la Mto Zambezi, tunapata umeme kutoka Zambia, maeneo yote ya Tunduma umeme wetu unatoka Zambia. Hivi faida hatukuziona hizi? Tumekazania kujadili mpaka wa Malawi na Tanzania ambao si mgogoro, labda sisi tunauanzisha sasa uwe mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Anglo-American Treaty* ya mwaka 1895 iko wazi na inaeleza mpaka huko wapi. Mwaka 1922 Donald Cameron, alifanya mazungumzo na nchi zote mbili baada ya Mjerumani kuondoka na kuhakikisha kwamba mpaka unakuwa kati kati ya maji na sheria za Kimataifa zinaonesha wazi kwamba mahali ambapo maji yako namna hiyo ni lazima mpaka utakuwa katikati. Lakini sisi tunasema kwa sababu Malawi wanasema ni Ziwa Malawi, ndio; Wanyasa Ziwa ni Nyasa, hawawezi wakaita Nyasa, Nyasa na ndio maana wanaita Ziwa Malawi, hawawezi kuita Nyasa, Nyasa. Nyasa maana yake ni Ziwa kwa Kinyasa. Halafu tunasema tunalalamikia ramani zinazotoka Malawi zinaonesha mpaka ni ng’ambo, Watanzania tutaacha lini kulialia? Sisi tumetengeneza ramani za kuonesha mpaka ni maji, tumezipeleka kule ili ku-*counter* ile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naona sisi tunaotoka maeneo yale hatuna mgogoro wa mpaka. Mgogoro katika matumizi ya maji sisi hatuna, tunaishi vizuri na ndugu zetu. Tuna matatizo ya Mto Songwe, tunakalishana na kutatua migogoro ile bila matatizo. Sasa kuchelewesha Azimio ambalo linataka kuwaajiri Watanzania, Azimio ambalo linataka kutuletea miradi, Azimio ambalo tunajua faida zake ni pamoja na umeme unaotoka Zambia, azimio ambalo tunataka tufaidike katika taaluma za ukusanyaji wa takwimu, tunachelewesha kwa sababu ya kusema tuna matatizo katika mpaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijafurahia sana lakini naunga mkono sana sana Azimio hili lipite ili tuanze kupata matunda. Nayasema haya kwa sababu, sisi tunaotoka upande wa Kusini Nyanda za Juu Magharibi, ndiko kuliko na vyanzo vingi vya mito inayokwenda kwenye Bonde la Mto Zambezi, kwa hiyo ni wadau sisi. Hatuwezi tukawa tunatunza vyanzo vya maji bila sisi kufaidika. Sasa kuridhia Azimio hili maana yake sasa Watanzania tuanze kufaidika. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri, vijana wetu ambao wako tayari, tunaporidhia kwamba tunakuwa nchi ya tano, basi tujue ni ajira ngapi tunazipata kule Botswana na tujue ni *component* zipi za miradi ambazo ziko tayari ili tuzichangamkie Watanzania na tuweze kujiunga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa, lakini naunga mkono Azimio hili la Mto Zambezi, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupewa nafasi hii na mimi nichangie machache. Kuhusu kuridhiwa kwa Mkataba huu wa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama ili kuunga mkono moja kwa moja Azimio hili la *ZAMCO.* Sisi tunaotoka mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya, ni wadau wakubwa sana wa Azimio na tunafaidika zaidi pamoja na Watanzania wenzetu wote katika nchi hii. Kwa hiyo, sina sababu ya kulipinga. Kwa kweli, limechelewa nafikiri Mheshimiwa Mpesya, amezungumza vya kutosha lakini vitu vyote ambavyo vina maslahi ya watu tusipende kuvicheleweshacheleweshakwa sababu havileti maslahi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi malengo yaliyoainishwa ya uanzishaji wa Kamisheni hii ni mazuri tena ni mazuri sana kwa maendeleo ya nchi yetu pamoja na nchi zetu zote nane. Kutokana na moja ya malengo kukusudia kuwa na ukusanyaji sahihi na takwimu sahihi zinazohusu rasilimali maji katika maeneo ya nchi hizi nane, nafikiri kwamba ndani yake tuna faidika sana. Tunafaidika kwa sababu hapo ndipo tunapoweza tukakaa chini sasa tukabuni mipango mizuri, tukabuni miradi mizuri ambayo ni endelevu kwa ajili ya nchi yetu. Kwa hiyo, naamini kabisa nchi zetu zote sasa baada ya kusikia kwamba Tanzania nayo imeridhia, sasa kutakuwa na kuchamka kwelikweli kuanzisha programu, kuanzisha miradi ya aina mbalimbali ili nao wahisani mbalimbali waingie katika kusaidia maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Kamisheni hii kutasaidia vilevile kutoa msukumo katika suala zima la utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika maeneo yote yanayozunguka Bonde la Mto Zambezi. Kwa upande wetu kama Tanzania na kama Azimio linavyosema, tunao mchango mzuri sana katika kuchangia maji yanayoingia katika bonde la Mto Zambezi kwa kupitia Ziwa Nyasa, ambako mimi natoka. Lile Ziwa ni kubwa na Ziwa ambalo linatoa mchango mzuri. Ni lazima, kama Watanzania na sisi tuwe *serious* katika ku-*play role* yetu katika hifadhi ya mazingira. Tunayo mito kama mitano ambayo inaingiza maji katika Ziwa Nyasa. Mito kama Ruhuhu kule mkoani Ruvuma, Mto Kiwira Mkoa wa Mbeya, Mto Songwe, Mto Rufiji na Mto Ruvuma, kule ambako Mwenyekiti unapigia kelele kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mito hii inatoa maji mengi kuingiza katika Ziwa Nyasa, lakini katika siku za hivi karibuni kumejitokeza hali ya kupungua kwa maji katika mito hii. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, kama tutaridhia Mkataba huu jambo ambalo nafikiri tutaridhia hivi karibuni maana yake tunawavutia na wadau mbalimbali, wahisani mbalimbali kuunga mkono miradi yote ya hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni zoezi kubwa sana ambalo unatakiwa mtu ulifanye, kwa hiyo kwa nguvu yetu sisi Watanzania peke yetu pengine inakuwa ni jambo gumu, lakini ikiwa tumejenga huu ushirikiano ambao tunautafuta hapa kwa kupitisha na kuazimia hili Azimio. Maana yake tunavutia na watu wengine wanajua kwamba aah

kumbe nao Watanzania wako *serious,* sasa tuwasaidie katika mipango yao. Kwa hiyo tunahitaji sana kuhifadhi vyanzo vya maji, tunahitaji sana kuhifadhi mito ambayo inaingiza maji yake ndani ya Ziwa Nyasa na baadaye kuelekea Mto Shire na baadaye kwenda bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeiomba Serikali hivi karibuni kwamba iweze kuchukua zile safu za milima ya Livingstone na kuiweka kama *nature reserve* unapokuwa na *nature reserve* unahitaji kuwa na misitu inayozunguka hiyo milima. Hivi karibuni kumejitokeza tabia mbaya sana, mbaya za kuchoma moto misitu yote inayozunguka *ranges* yaani safu za milima ya Livingstone na hili si jambo la kulivumilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya hivyo maana yake unaharibu vile vyanzo vya maji vyote ambavyo vinaanzia katika safu hizo, kwa hiyo naomba sana nayo Serikali iharakishe huo mpango wa kuwa *nature reserve* katika safu za milima livingstone kwa sababu wadau wengi wangependa kuingia na kushirikiana na Serikali na sasa kama wataona kwamba tunaridhia pia na Mkataba huu basi haitakuwa na sioni shaka yoyote kwamba wadau mbalimbali wahisani mbalimbali watatuunga mkono katika kuanzisha miradi mizuri na programu nzuri ili kuhifadhi mazingira ya milima hiyo pamoja na kuboresha Ziwa Nyasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *article* Na. 3 inasema kwamba Baraza la Mawaziri wa Nchi Wanachama watatoa maamuzi kuhusu wapi yawe makao makuu. Ningependa kuomba kwamba Serikali yetu hebu iombe, iombe *commission* hii ili makao makuu yawe Tanzania na hususan katika mikoa ile ya jirani kama Mbeya, kwa sababu eneo lile lina kila aina ya infrastructure ambayo inawezesha kila shirika, kila *commission* kila aina ya mradi kuweza kuwa na makao makuu katika mkoa wa Mbeya. Kwa hiyo, naamini kabisa Waziri anayehusika atajaribu kuanza kujenga hoja hiyo. Sisi tungependa kwa sababu ndio ajira zenyewe hizo tunazitafuta ziweze kuja hapa nchini na kutangaza nchi yetu na kutangaza mikoa ambayo sisi tunasema mikoa ya Kusini lakini na yenyewe iweze kuonekana kwamba inashika na kulea Makamishina makubwa kama haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya mafupi, naomba moja kwa moja niseme kwamba naunga mkono kwa asilimia mia uanzishaji wa Kamisheni hii na Azimio ambalo tunaliridhia hivi sasa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. RAYNALD A.MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kupata nafasi hii leo kuweza kuchangia juu ya Azimio hili la kuanzishia Kamisheni hii ya Maji ya Mto Zambezi pamoja na bonde lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natoa shukrani kubwa kwa Waziri wa Maji na wenzake kwa kuleta Azimio hili, kusema kweli ni kitu kimoja ambacho naona moja kwa moja kiungwe mkono na wengi wetu na hasa mimi binafsi naunga mkono hoja hii iweze kupita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyosemwa Tanzania inachangia karibu asilimia 11.3 hayo ni maji mengi sana sana na kwa hiyo ningependa kutoka mwanzo kusema

kwamba licha ya kwamba naunga mkono yale yaliyozungumzwa na Kamati mbalimbali na yale yaliyozungumzwa na wenzangu hapa, nasema kwamba tuwe na *master plan* ya namna ya kutumia vizuri bonde hili la Mto Zambezi na hasa katika eneo linalotuhusu ambalo ni Mto Ruvuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Ruvuma ni mto mkubwa na wa ajabu. Kwa bahati mbaya licha ya chanzo chake kuwa mahali pazuri lakini maji yake yote yanakwenda bahari ya Hindi. Ni kiasi kidogo sana tunakitumia kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na *master plan* nzuri ya kutumia bonde lile ili liweze kutunufaisha. Hivi karibuni sisi wengine tumeanza kutumia kidogo kidogo vyanzo vile kwa mfano katika Mto Lukuledi na hasa katika mto wa Ndanda, ambako natoka, tumeanzisha programu za umwagiliaji. Lakini programu hizi ni ndogo z Wizara inahitajika izibebe ili baadaye hata wenzetu wakija kuangalia waone kwamba kumbe kuna mambo mazuri, nao wanaweza wakaleta fedha zao ili kuweza kukuza ule umwagiliaji na ukatupatia manufaa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Wilaya yetu ya Masasi, nakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri naye alikuwepo katika safari ile, kulikuwa na ahadi iliyotolewa kwamba mradi wa Ndanda wa umwagiliaji Waziri Mkuu aliagiza kwamba Wizara ya Maji iharakishe kutoa kiasi cha shilingi milioni 250 ili tuweze kujenga wia na mifereji na kadhalika. Sasa toka pale tulipiga makofi tukaondoka, sasa mpaka leo Waziri yupo kimya. Namwomba Waziri wa Maji atekeleze ahadi hii. Nasihi Wizara ije na mpango endelevu wa kutumia vizuri Bonde hili na chanzo cha Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika Mto Ruvuma kuna samaki wazuri sana, kuna samaki aina ya Ningu, kuna samaki aina ya Kamchali, wapo makwalu na kuna hata aina fulani ya kamba wa maji baridi, wapo katika Mto Ruvuma. Watu wa kwetu kule wanajitahidi kujaribu kuvua, lakini vikwazo vinakuwa vingi mno wakivua kule Ruvuma kuleta Masasi wanakutana na vizuizi vya maliasili vingi. Vizuizi hivi vinawadai wavuvi walipie leseni nyingi na ruhusa za kila aina kiasi kwamba wavuvi wengi wanashindwa kupeleka samaki Masasi kwenda kuuza. Wavuvi wengi wanashindwa kwenda kuvua Mto Ruvuma kutokana na vikwazo vingi vinavyowekwa na idara ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mto Ruvuma cha ajabu ni kuwa, ule mto ametupatia Mwenyezi Mungu, samaki wapo, tuwaambie watu wetu wavue. Suala la kusema kwamba wanavua samaki wadogo siamini kwa sababu samaki niliowaona Masasi ni wazuri tu wanaotoka katika Mto Ruvuma. Kwa hiyo, naomba Wizara husika iwe na utaratibu mzuri wa kutokusumbua wananchi wale kuvua katika Mto Ruvuma. Ukienda Ziwa Nyasa kuna samaki watamu wanaitwa mbasa, sijaona samaki watamu kama hao. Aidha, unaweza kumpika kwa kumchemsha mtamu, kumkaanga ni mtamu, kumkausha ni mtamu. Lakini hakuna utaratibu wowote tuliojiwekea hapa nchini wa namna ya kuvua vizuri wala kumhifadhi ili aweze kutusaidia zaidi. Kwa hiyo, naomba tunapoanzisha Kamisheni za namna hii hebu tuangalie jinsi gani hivi vitu vingine vinavyoweza kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utalii nasema mpaka sasa hivi *hakuna master plan* ya utalii katika bonde hili la Ruvuma ingawaje tuna mapori makubwa mawili, kuna pori la Msanjesi na kuna pori la Lukwika. Siku moja nilipata bahati ya kutembelea Lukwika basi tulikuwa tunakunywa, hivi nikaona ndovu kama watano wanavuka mto Ruvuma, yaani Waingereza wanaita *majestically* yaani kwa kuringa kweli kweli na ndovu wale wana meno makubwa, sijawahi kuona meno makubwa namna ile, walikuwa watano wanakwenda upande wa Msumbiji. Hapo hapo kulikuwa na watatu na dume moja kubwa kweli linatoka Msumbiji linakuja huku. Mambo haya yalinistua kuona kuna mambo mazuri namna hii. Ndovu wanakwenda Msumbiji, wengine wanakuja Tanzania bila kipingamizi chochote bila kujali mipaka nikasema hivi Wizara yetu ya Maliasili ina habari ya mambo haya mazuri namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoomba tuwe na *master plan* ili kuweza kutumia rasilimali za namna hii na ndio maana nilisema Wizara ijitahidi kuanzisha hifadhi ya Taifa, *National Park* katika maeneo haya kuwe na hifadhi safi katika kutumia hili bonde vizuri. Kwa hiyo, ni juu yetu sisi wenyewe kuhakikisha kwamba vitu hivi tunavitumia vizuri na wenzetu tutakaokuwa nao kwenye kamisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nililotaka kuzungumzia katika hili ni kwamba wenzetu wanayatumia vizuri sana maji ya Mto Zambezi, wenzetu wa Zambia na Zimbabwe, wanayatumia kwa kuzalisha umeme na ule umeme wanatuuzia sisi huku. Maana yake ni kwamba wananufaika kupata fedha za kigeni toka kwetu kwa kulipia umeme. Lakini sisi hatupangi mipango ya kujipatia pesa katika maeneo yaliyo karibu na Mto Ruvuma, maji yanakwenda baharini. Sasa hivi karibuni kuna umeme wa gesi kutoka Mtwara kwenda Masasi, sioni kwa nini Wizara yetu ya Maji haiwezi kutumia umeme huu kuvuta maji ili kuyapeleka Masasi, Newala na katika maeneo yale yote, kwanini tuwe na kiu wakati maji mengi yanaporomoka kwenda baharini. Hili ni suala mipango tu, ingekuwa toka wakati wa uhuru tumepanga kwamba maji ya Mto Ruvuma wayatumie vizuri watu wa Masasi, Newala na kadhalika hii leo ingekuwa wote sisi tunafaidika na maji yale, lakini tumelala usingizi tu wakati rasilimali nzuri tunayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kusema tu kuna mambo mengi yanayoweza kutufaidia katika itifaki hii na hayo ni lazima yatokane na sisi wenyewe kwa kupanga mipango, halafu naamini wenzetu wakituunga mkono tutapata wawekezaji watakaohakikisha kwamba mipango hii inakamilika. Kwa hiyo, naunga mkono sana itifaki hii na naona kwa siku za usoni tutapata mafanikio na manufaa mengi zaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumebakiwa na muda wa kutosha kidogo, sasa msemaji ambaye nilimwita ambaye angefuata yeye amesema dakika hizi hazimtoshi, lakini yuko mchangiaji mwingine katika orodha yangu yeye anakubali dakika hizo zinamtosha kuleta ujumbe wake muhimu. Kwa hiyo, naomba nimwite Eng. Stella Manyanya ili kusudi baadaye tuwe tumebakia na wachangiaji wachache kwa kipindi cha jioni.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Azimio hili muhimu la uanzishwaji wa Kamisheni ya maji ya bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde la Mto Zambezi kama ilivyozungumzwa ni muhimu sana kwa Watanzania na nchi za Afrika kwa ujumla wake. Hivi karibuni nilikuwa nimetembelea nchi ya Zimbabwe na nikajionea utalii uliopo pale katika Victoria *falls* ambayo ni maajabu ya tatu ulimwenguni. Kwa hiyo ulinzi wa maji ya mto huu ni muhimu sana kwa sababu hata kama ule utalii unafaidisha Zimbabwe ina maana una *impact* kwa Afrika kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakumbuka pia Mto Zambezi una historia ya Wangoni walipotoka South Africa walivuka katika mto ule na hivyo una historia ya vita vya majimaji. Lakini pia ni mto muhimu ambao huwezi kuuacha unapozungumzia historia ya Wangoni. Hali kadhalika imeniwia vigumu kutosimama kuzungumzia Azimio hili kutokana na suala ambalo limezungumzwa la mipaka. Nitatofautiana kidogo na Mheshimiwa Mpesya kwa sababu nimewahi kushuhudia chokochoko zilizokuwepo wakati fulani katika miaka ya 70. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzuri kabisa ni kwamba, nchi hizi mbili Malawi na Tanzania tuna mahusiano mazuri na kwa kuwa tuna mahusiano mazuri hakuna haja ya kuwa na mambo ambayo yanaleta utata. Ni vema tukayamaliza na yakawa wazi, badala ya kusema kwamba tungoje tu kama ambavyo ilifanyika na huyo mkoloni au Mzungu wakati huo, lakini tunaona kabisa bado kuna dalili za kutokuelewana. Kwa bahati nzuri mimi ni mdau mkuu kwa sababu hata ardhi za baba zangu ziko mpaka katika maji ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoona kwamba sehemu kubwa ya mchango wa maji unatoka katika milima na bonde la Ziwa Nyasa lililoko Tanzania. Sasa kama hao watu hawatapewa motisha ya kufahamu fika kwamba lile ziwa kama ambavyo inaainishwa katika Mikataba ya Kimataifa, mpaka wake uko kati na hivi na wao ni sehemu ya kufaidika na lile ziwa. Hizi nguvu za kutunza misitu ile ili isiharibiwe itatoka wapi? Kwa hiyo, nafikiri kuna umuhimu kabisa wa nchi hizi mbili kukaa pamoja na kulimaliza tatizo hili. Kwa bahati nzuri ninavyomsikia na kumwelewa Mheshimiwa Rais wa Malawi, Mzee Bingo wa Mtalika ni mtu muungwana na mwenye upendo, hali kadhalika Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mtu mwanadiplomasia ya hali ya juu na muungwana, kwa hiyo, sioni kama watashindwa kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningezidi kuungana na wenzangu kwamba ni vema Serikali yetu isaidie na itoe msukumo wa haraka ili kuhakikisha kwamba wanamaliza hili tatizo. Lakini pia hii itatoa ujasiri au *confidence* kwa mwekezaji ambaye atakuja katika beach ziliko upande wa Tanzania. Kwa sababu wenzetu huwa wanasoma, wanafuatilia, akisikia kuna utata inamnyima nguvu ya kuja kuwekeza. Kwa hiyo, ni vema suala hili likakamilika ili kutoa hiyo fursa iliyoko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia katika siku za hivi karibuni Mkoa wa Ruvuma umekuwa ukipata matetemeko ya ardhi ya mara kwa mara, nahisi inawezekana kwamba historia au jiografia inazungumzia bonde la Ziwa Nyasa au milima ya Livingstone jinsi ilivyoumbwa. Kwa hiyo, napenda nifahamu je, kuna utafiti wowote uliofuatilia juu ya tetemeko hili na kuona kama kuna athari yoyote kubwa inayoweza kujitokeza ili kujua kwamba kama ni hatua zipi zichukuliwe kwa ajili ya kuwanusuru watu ambao wako katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie juu ya umuhimu wa barabara inayotoka Mbamba Bay mpaka Litui, Mheshimiwa Komba hayupo nina uhakika sasa hivi pia na yeye angelizungumza hilo mwenyewe. Ni kwamba barabara ile ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi wa Tanzania, naomba Serikali iongeze nguvu zake katika kuhakikisha barabara ile inakuwa nzuri na inapitika wakati wote ili kuona kwamba mipaka yetu inakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya niliyozungumza na kwa kuwa pia nimechangia kwa maandishi, nasema nashukuru sana na naliunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba nimshukuru Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, kwa kuweza kutusaidia kuutumia muda huu vizuri kama nilivyosema tumebakia na wachangiaji wawili katika hoja hii, mchangiaji wetu wa kwanza mchana atakuwa Mheshimiwa Prof. Mwalyosi na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Jenister Muhagama kama hatakuwa mezani. Baada ya hapo basi Mheshimiwa Waziri ataendelea kuhitimisha hoja yake na mwishoni tutaiamua kwa mujibu wa kanuni za Katiba yetu. Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni katika ukumbi huu.

*(Saa 6.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*(Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tulipoondoka asubuhi ni kwamba hili Azimio lilikuwa linachangiwa na hivi sasa ninao wachangiaji wa mwisho na nitaanza kumwita Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. Mheshimiwa Mwalyosi karibu.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba na mimi nichangie ingawaje kwa kiasi kidogo kwa sababu wenzetu waliotangulia wametufilisi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Mwandosya kwa kuwa king'anga'anizi na kuhakikisha kwamba hoja hii inawasilishwa hapa Bungeni na bila shaka kuidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze mapema kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa sababu kuu tatu. Kwanza ni kwamba, tunatakiwa kutekeleza itifaki ya maji shirikishi ya *SADC* ambayo ilishatiwa saini na Mheshimiwa Rais, lakini vile vile iliridhiwa na Bunge hili, tayari ni mchakato ambao tumeshaufikisha mahali, tutakuwa watu wa ajabu leo tukianza kukataa. Kwa hiyo, ni mtiririko tu wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili mimi ni mdau, Ludewa inashika sehemu kubwa sana katika mwambao wa Ziwa Nyasa, kwa hiyo faida ya kuridhia hii au hasara ya kutokufanya hivyo lazima wananchi wa Ludewa wataathirika kwa kiwango kikubwa, kwa hiyo naona ni lazima niridhie kwa vyovyote vile na kwa hiyo naunga mkono. Lakini kikubwa zaidi naelewa kinacholetwa mbele yangu na faida yake na naelewa ninachofanya ni kitu cha muhimu ndiyo maana nakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia labda nieleze kwa nini mimi nadhani ni vizuri ushirikiano unaopendekezwa kati ya nchi hizi nane, moja ambayo ni kubwa kuliko yote inasaidia kuhakikisha kwamba shughuli yoyote inayoweza kufanyika mahali popote katika Bonde hilo, shughuli yoyote ile inatakiwa isiathiri maendeleo au shughuli zinazoendelea katika maeneo mengine ya Bonde. Ni suala la mikakati jumuishi yaani *Strategic programmes* za kuhakikisha kwamba tunaliangalia bonde kwa upana na ukubwa wake ili kwamba kazi yote inayofanywa imezingatia kinachoweza kutokea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni muhimu kwa upande wetu, kwa mfano, katika Ziwa Nyasa wenzetu wa Malawi miaka ya huko nyuma waliwahi kuziba Mto Shlre ambao ndio unaotoa maji kutoka Ziwa Nyasa kuingia katika Mto Zambezi. Walipoziba pale maji yaliongezeka sana, matokeo yake ardhi kubwa sana iliyokuwa tambarare au ya chini upande wa Ludewa ilizama kutokana na kuziba Mto Shire, kwa hiyo ina maana kwamba hatuwi kwenye kundi hilo la kushirikiana na wenzetu na sisi tukawa nje, wanaweza wakafanya matendo ambayo hatutakuwa na mahali pa kulalamikia, kwa hiyo ni lazima tuwe ndani kwenye kundi hilo ili tuweze kulalamika endapo hilo litatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kunaweza kutokea uvuvi ambao si endelevu, niliwahi kuzungumza hapa Bungeni kwamba kuna wakati tulipata fununu au taarifa kwamba wenzetu wa Malawi walikuwa wanalisha samaki kule ziwani, walikuwa wanachukua boti kutoka Kaskazini wakiwa wanaendesha huku wanamwaga chakula cha samaki Ziwani. Sasa kwa kufanya hivyo unachangia uchafuzi wa maji kwenye ziwa lakini pia lengo ilikuwa kulazimisha samaki kula chakula kile halafu wakishiba wanakwenda kwenye sehemu ambayo maji ni ya joto ambayo siyo kina sana, kwetu kule

ni kina sana, lakini kwa wenzetu ni *shallow*, kwa hiyo samaki wakishiba wanakwenda kukaa kwenye maeneo ambayo ni ya joto joto zaidi. Kwa hiyo, samaki watavutiwa upande wa Malawi kuliko Tanzania, kwa hiyo inatuletea matatizo upande wa wavuvi wetu. Kwa hiyo, vitu hivi vinaweza kudhibitiwa kama tuko pamoja katika ushirikiano kwa sababu tunaweza kuzungumza nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna masuala ya umwagiliaji unaoweza kutokea na sisi kule Manda kwenye Mto Ruhuhu tunapanga kufanya umwagiliaji. Najua kuna shughuli kama hizo upande wa Kyela, nadhani hata upande wa Malawi lakini umwagiliaji mara nyingi ni kwenye maeneo oevu, ndiyo kawaida. Sasa tahadhari za kuchukua unapofanya umwagiliaji kwenye maeneo oevu ambako mara nyingi bioanuai ni kubwa na maeneo haya yanatakiwa kuangaliwa, kusimamiwa na pengine kuhifadhiwa inatulazimu kuwa waangalifu sana. Kwa hiyo, mtu yeyote au nchi yoyote inapofanya kazi ya umwagiliaji ni vema kuwasiliana na nchi nyingine ili tuhakikishe kwamba shughuli ya umwagiliaji haitaathiri wenzetu walio chini au maeneo ambayo maji yanaelekea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna mazao ya samaki, maeneo oevu hayo mara nyingi ndiyo mazalio ya samaki. Mara nyingi kuna samaki wanaopanda juu kwenda kuzalia huko, halafu watoto hao wakiteremka wanakuja kukulia Ziwani. Maeneo yote haya ni vema tuhakikishe kwamba yanahifadhiwa au yanatumiwa kwa umakini sana ili kutoleta athari ambazo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida ninazoziona ambazo ni nyingi tu lakini nataka kuzungumzia chache. Kikubwa ninachokiona ni kule kuongeza nguvu palipo na watu wengi kuna nguvu kubwa zaidi kuliko mojamoja kwani umoja ni nguvu. Taarifa tulizonazo kuhusu aina ya samaki katika Ziwa Nyasa lakini mazingira yanayozunguka kwenye bonde lile hatuna taarifa za kutosha na utafiti ni ghali sana. Kwa hiyo, tunapokutana nchi nyingi kwa pamoja watafiti wetu na wataalam wetu tunaweza kuwatumia hawa, tunaongeza nguvu ya kuweza kufanya kazi za utafiti na kutupa taarifa ambazo zinatumika kwa maendeleo na kwa namna hiyo tunaharakisha maendeleo ambayo ni endelevu kwa sababu tunakuwa na uhakika na kitu tunachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile katika Ziwa Nyasa tumepoteza samaki wengi sana ambao walikuwa ni watamu na waliokuwa wanapendwa sana na wananchi kutokana na uvuvi mbaya na nategemea kwamba, kupitia mpango huu sasa kati ya vitu ambavyo tunategemea watatusaidia katika kushirikiana na kuingiza katika umoja huu ni kuhakikisha kwamba utafiti wa uhakika unafanywa, tuangalie namna tunavyoweza kurejesha samaki wale ambao wameanza kupotea au wamepotea ili waweze kurudi tena kwenye ziwa lile kwa ajili ya kitoweo na vilevile kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza hapa asubuhi ndugu yangu mmoja habari ya matetemeko, ni kweli safari hii kumekuwa na matetemeko ya ardhi makubwa sana, najua yanatokea kwenye Bonde la Ufa kila mahali lakini matetemeko ya mwezi Desemba yalikuwa siyo ya kawaida kwani yalikuwa ni makubwa na yametokea kwa

*frequency* kubwa sana na watu waliogopa sana lakini tunachotaka kujua ni kwa nini yametokea wakati ule? Kulikoni? Kulitokea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui kama Serikali yetu ama labda Waziri atatwambia kama kuna vituo na unafanyika ufuatiliaji wa matetemko, kama kuna mitambo yoyote mahali popote ambayo inafuatilia matetemeko haya ili kuwa *–alert* wananchi wetu wajue kinachoendelea na kinachoweza kutokea ili kujiweka tayari yaani kujiandaa kwa lolote linaloweza kutokea. Nategemea kwamba tafiti kama hizo na ufuatiliaji kama huo utawezekana kwa kuingia kwenye ushirikiano na wenzetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ilivyo katika mabonde mengine bonde la Ziwa Victoria au Ziwa Tanganyika tumeshuhudia faida kubwa ambayo wenzetu wameweza kupata kutokana na mifuko ya fedha ambayo imetolewa na mashirika mbalimbali kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya mabonde hayo na sisi tunadhani kwamba tumechewa sana kwa sababu wenzetu wameanza muda mrefu na ndiyo maana nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kulileta hili sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine kwa sisi tulio katika bonde lile la Ziwa Nyasa tutaweza kufaidika kutokana na fedha itakayowekwa kwenye mifuko hiyo, itusaidie pengine kwenye miundombinu, uvuvi endelevu na kutusaidia wananchi kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kule Manda tunaweza tukapata fedha nyingi kutoka huko lakini barabara zinazoweza kuteremka kwenye Ziwa Nyasa kuteremka Mlima Livingstone, inawezekana zinahitaji fedha nyingi kwa hiyo pengine mifuko hii itatusaidia kuhakikisha kwamba tunapata miundombinu ya kuteremka kule ziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo mawili tu. Kwanza tumeambiwa kutakuwa na ofisi moja, nataka kuamini kwamba ofisi ya Botswana ni ya muda lakini itabidi tukubaliane ofisi itakuwa wapi. Nataka nikubaliane na Mheshimiwa Hilda Ngoye kwamba bonde lilivyokaa kwa vyovyote vile Ziwa Nyasa patakuwa ni katikati ya bonde, kwa hiyo kama ni makao makuu inatakiwa katikati na kwa vile tunazungumzia raslimali kuu hapa ni maji na maji mengi yapo hapo kwenye Ziwa Nyasa, kwa hiyo, nategemea ofisi iwe kwenye sehemu hiyo kwenye bonde la Ziwa Nyasa na miji mikubwa inayojulikana kandokando ni pamoja na maeneo kama Kyela. Kwa hiyo, nitashangaa mahali kama Kyela pakishindwa kufanyika kama Makao Makuu ya Ushirika huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa ninachotaka kusema ni kwamba bonde ni kubwa sana ku-*operate* au kutegemea kufanya kazi kutoka katika ofisi moja endapo itakuwa mbali sana tija haitakuwa rahisi kupatikana. Napendekeza basi kuwe na ofisi za kanda. Tuna bonde kubwa lakini likagawanywa katika kanda mbili au tatu, tukawa na

ofisi ndogondogo kwenye maeneo ya kanda ili kuwezesha mawasiliano ya haraka zaidi na kuongeza tija katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema naunga mkono kabisa, suala hili limechelewa kidogo lakini nadhani tutakimbia zaidi kuliko wenzetu, tutaungana na wenzetu wa Bonde la Ziwa Victoria na Tanganyika kuhakikisha kwamba fedha itakayotokana na kujiunga na wenzetu hawa inasaidia sana katika kuboresha maeneo ya pembezoni kama kule Ludewa ili nako tuweze kwenda sambamba na wenzetu katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi ambaye pia ni mwanamazingira na sasa nimwite mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Jenista J. Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, lakini niipongeze Serikali yetu kwa kuamua kukubali kuwa na mkakati huu maalum wa kuridhia Mkataba huu wa matumizi bora ya Bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwa namna moja au nyingine tunaweza tukasema kwamba azimio hili limechelewa kwa sababu za kimsingi lakini Wanaijeria wana methali moja inayosema unapokuwa na mke wako ndani ya nyumba na mmeanza kupigana ngumi, moto ukianza kuwaka mtaacha kwanza kupigana ngumi mkazima moto halafu hayo mambo ya ugomvi mtayatathmini baadaye. Hiyo ni methali nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengine hapa asubuhi wamezungumzia sana suala la mgogoro wa mpaka kati yetu na rafiki zetu wakubwa na jirani zetu nchi ya Malawi na huenda hiyo ilikuwa ni sababu moja ama nyingine ya kutufanya tuchelewe kuridhia Azimio hilo. Sasa kwa usemi huo wa methali ya Kinaijeria niliyoisema nadhani wenzetu wa Malawi wamesharidhia huu Mkataba sasa na sisi turidhie kwa methali kwamba sasa moto umewaka, tusiendele kutwangana ngumi tukasahau, tuzime moto ili tujiletee maendeleo, habari ya ngumi zetu tutazitafakari baadaye na kujua nani ni mkorofi na nani si mkorofi halafu tutayamaliza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nianze kwa kusema naunga mkono Azimio hili. Naunga mkono, nina sababu na niseme kwamba kwetu sisi wananchi wa Mikoa ya Kusini Ruvuma ikiwa mojawapo na unajua bonde linapita mpaka katika Mkoa wetu wa Ruvuma, mimi sina shaka naona huu ni ukombozi mkubwa sana huko Kusini ambako

tumekuwa kila siku tukilalamika kwamba maendeleo yetu yako nyuma. Sasa inapofikia mwanya wa namna hii naona ni ukombozi mkubwa sana na hata si kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini lakini pia kwa nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tumezungumzia mpango wa kiuchumi wa bajeti wa nchi yetu na mpango ule tumeona kwamba *agenda* yetu ya kwanza katika nchi yetu ni kilimo. Lakini Waziri wa Fedha wakati anatueleza mfuko wake unafikiri nini katika mipango ya maendeleo ndani ya nchi yetu, tuliona kabisa kwamba fedha yetu ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni chache sana, sasa hii miradi ndiyo itakayotusaidia kufidia pale ambapo sisi wenyewe tunashindwa na tumeona kwamba tumekuwa tukitegemea ufadhili kutoka nje ambao wakati mwingine unachelewa yaani hauji kwa wakati muafaka, sasa tukiingia kwenye Mkataba huu ina maana kwamba hata hii *agenda* yetu ya kilimo kwanza kwa namna moja ama nyingine itapewa nguvu na huu mpango mzuri kabisa wa matumizi ya Bonde la Zambezi ambao tunauridhia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, nianze na ushauri, naomba kushauri katika utekelezaji wa Azimio letu. Kwanza, tumesema kwamba tumeona hili Azimio tunaporidhia tutakuwa na miradi mikubwa tu, miradi ya kilimo cha umwagiliaji, miradi ya kiteknolojia, miradi ya kielimu na kadhalika. Sasa kama hii miradi yote imeainishwa katika Azimio na tunapoazimia ina maana tumeazimia kwamba na sisi tumekubali sasa kuipokea hiyo miradi, lakini naomba nishauri ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ile miradi ambayo sisi tunataka iweze kujengwa kwetu Tanzania kama ni miradi ya kiteknolojia tutafute teknolojia halisi tunazozihitaji kwa sasa kwa ajili ya kutukomboa katika dhana hii ya kilimo kwanza. Tutumie nafasi hii tujiulize teknolojia tunazozikosa katika nchi yetu zitakazotufanya kwenda mbele katika maendeleo yetu kwa kasi na kwa kutumika nafasi hii ya matumizi ya Bonde la Mto Zambezi ni teknolojia zipi tunazozihitaji kwa wakati wa sasa? Kwa hiyo, miradi ya kiteknolojia iendane na mahitaji yetu ya sasa katika nchi yetu ya Tanzania na kwa maeneo hayo yaliyojipambanua kwenye mradi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nashauri tuone Azimio linasema tutakuwa na suala zima la ajira ndani ya mradi wa bonde. Ilani yetu ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ilisema itajitahidi kuongeza ajira ndani ya nchi ya Tanzania na tumeshavuka lengo. Lakini huu ni mwanya mwingine unajileta, mara nyingi sisi katika nchi yetu nafasi hizi zinapotokea tusipofanya maandalizi tukaingia kupambana kwenye soko la nchi zilizomo ndani ya Bonde tunaweza kujikuta hatuna ajira za kutosha zitakazozalishwa kupitia nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe na mkakati hata kama kutakuwa na *sub-committees* ndani ya Kamisheni ya Bonde, siyo vibaya na sisi tukawa na ka-*sub-committee* ka ndani ya Wizara yetu katakakokuwa kanafanya hizo changamoto za kuhakikisha ajira hizo hatuzikosi. Wanafunzi wetu na vijana wetu wa Kitanzania

wamesoma na wana elimu nzuri, hii ni nafasi ya kuondokana na tatizo la ajira na kuwapatia ajira na tukiweza kuwapatia ajira tunaongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ni ushauri wangu mwingine, tusikae tu tunafurahia ajira, ajira, ajira, tumejiandaaje ili ajira hizo tuweze kuzikamata. Huo ni ushauri wangu wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina ushauri mwingine miradi hii ambayo itaanzishwa kwa ajili ya kuendeleza Bonde nadhani ni wakati wetu muafaka sasa kuangalia, hivi tunaoanishaje miradi ya Bonde na miradi yetu mikubwa ya Taifa kupitia Mpango wetu Mkakati wa Kilimo katika nchi yetu. Sasa ni nafasi nyingine nzuri ya kuona katika Mpango wetu wa Taifa, nini tunachokosa? Mradi gani mkubwa tungependa utekelezeke? Lakini kwa matatizo ama ya rasilimali fedha, watu tumeshindwa basi tutumie huu mwanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe mfano mmoja, sasa hivi nchi yetu ina upungufu wa sukari kwa takriban tani kama 80,000. Kwenye bonde hili la Zambezi na hasa kule Mkoa wa Ruvuma na Jimbo la Peramiho, kwa mfano, sisi tumeazimia sasa tuingie katika kilimo cha miwa ili tutengeneze sukari, tupunguze hili tatizo la sukari katika nchi yetu ya Tanzania. Sasa uone mianya ya matumizi ya Bonde kwa Kilimo cha namna hii yanaweza kuwa na tija kabisa katika mtazamo wa Kitaifa lakini katika mtazamo pia wa kuwainua wananchi wetu wakaondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani ni nafasi yetu nzuri sana kutumia Mkataba huu kuhakikisha, unaleta manufaa makubwa kwa wananchi wa Tanzania, lakini pia kwa nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mkataba unasema, una lengo la kuongeza kiwango cha elimu na ujuzi. Tunapozungumzia elimu katika suala la matumizi ya Bonde, hakuna mtu ambaye haelewi umuhimu wa elimu na ujuzi, kwa kuwa kwanza, bonde lenyewe litataka uhifadhi mkubwa. Bonde hili lina misitu, milima, vyanzo vya mito na unaona kabisa ni utajiri mkubwa wa uoto wa asili. Liko tatizo kubwa la kuhifadhi mazingira, ni tatizo la Kitaifa lakini ni tatizo la Kimataifa, basi tutumie nafasi hii kubadilishana ujuzi na uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi Waafrika lazima tubadilishane ujuzi na uzoefu kutoka nje, huko kwenye Mataifa ya Ulaya, lakini sasa naona hii ni nafasi yetu nzuri kujijengea uwezo ndani ya nchi zetu za Afrika, kuona tunaweza kutatuaje matatizo yetu wenyewe, kama hayo matatizo ya kimazingira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, kwa kuwa tunahitaji kuwa na vyuo vya utafiti wa mbegu bora, wa hali ya hewa, wa uoto wa asili na mambo mengine ya namna hii, hii ni nafasi nyingine nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa na Mheshimiwa Hilda Ngoye, wamezungumzia suala la ujenzi wa Makao Makuu kule Mbeya, naomba Mheshimiwa Waziri katika miradi mikubwa ya Bonde, hebu Mkoa wa Ruvuma ikiwezekana hata kule Jimbo la Peramiho tujenge chuo kimoja cha Utafiti katika kitengo hiki cha kuongeza ujuzi wa elimu na ujuzi wa teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukipata Makao Makuu Mbeya, tukajenga Chuo cha Utafiti, Mkoa wa Ruvuma kule Peramiho, nadhani Mheshimiwa Waziri haya mambo yatakuwa mazuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kwamba, Mheshimiwa Waziri kwa kweli sioni shaka na narejea kusema sioni shaka kwa nini tuendelee tu kugombana na kuwa na hofu kuhusu mipaka, ukiangalia haya niliyoyasema kama ushauri, ndiyo mambo ya msingi katika Azimio hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachewa wana methali isemayo: "Jani la mti likidondoka ni aibu ya mti." Sasa na sisi tusiporidhia Mkataba huu ni aibu ya nchi yetu. Tumepewa bure, tutumie. Kwa hiyo, tusipotumia ni aibu yetu, nasema wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanafurahia sana Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeridhia Azimio la Mashirikiano ya Mto Ruvuma na Msumbiji, nilikwambia hapa, Jimbo langu la Peramiho kule Namatui, tumepata fedha nyingi za umwagiliaji, sasa kwa nini nisifurahie hili Azimio ambalo litaenda kuwakomboa tena wananchi wa Jimbo langu la Peramiho na Mkoa mzima wa Ruvuma kwa ujumla wake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jani likidondoka ni aibu ya mti, tusiporidhia Mkataba huu ni aibu ya nchi yetu na ni aibu yetu sisi Wabunge, lakini ni aibu ya maendeleo ya nchi yetu. Nawashawishi wenzangu tuunge mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa mchango wako ambao bila shaka wengine wote pia wameufurahia. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba nimwite moja kwa moja Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji ili aanze kutoa majumuisho. Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Wamelipitia hili Azimio kwa undani sana na ni Kamati yenye watu wenye uzoefu mkubwa, watu wenye busara sana, uzoefu wao katika masuala ya Ulinzi, Usalama na Uhusiano wa Kimataifa ni mkubwa. Tulikuwa na vikao vinne, haijapata kutokea kwa Azimio moja tu. Binafsi wameniwezesha kuwa na ufahamu mkubwa, hasa kuhusu suala la mpaka kati ya Malawi na Tanzania, nawashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika wametimiza wajibu wao mliowapa ipasavyo kwani kupitia wao yaani Kamati, wameonesha kwamba, Bunge sio mhuri wa kuidhinisha mambo ya Serikali kila wakati, kwa hiyo nawashukuru sana, wamefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zetu za dhati kwa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Kamati yetu ya Kisekta haikuwa na ulazima kuliangalia hili Azimio, lakini kwa ombi letu walikutana ili tuweze kuwataarifu kuhusu Azimio ambalo linahusu maji shirikishi, ambalo ni eneo wanalolisimamia. Namshukuru sana Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, pamoja na Kamati nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada, naomba niwatambue waliochangia katika kulisemea au kwa kuandika kuhusu Azimio hili. Wale ambao wamesema hapa Bungeni ni pamoja na Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda, ambaye amesema kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi si haba ni wanne; Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba; nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafanya majumuisho kwa masuala ya kijumla ya msingi halafu nitamalizia kwa masuala mahususi ya Mkataba huu. Kuhusu masuala ya kijumla, nitaanza na suala la mpaka kati ya Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya bonde ni mipaka ya asili ya kijiografia na kihaidrolojia, hakika haina uhusiano wowote na mipaka ya kiutawala, mipaka ya kisiasa. Hata hivyo, kwa kuwa hili suala limezuka katika Kamati na vilevile baadhi ya wachangiaji wamelisemea, nitajaribu kuwa makini katika kutoa maelezo yangu, kwa sababu lolote nitakalosema linaweza kuchukuliwa kama ushahidi hapo baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kuna tafsiri mbili za mpaka kati yetu na Malawi; tafsiri ya kwanza ni kwamba, mpaka unapita katikati ya Ziwa na tafsiri ya pili ni kwamba, mpaka unapita ufukweni. Nyaraka mbalimbali za kihistoria na rekodi mbalimbali zinadhihirisha kuwepo kwa tafsiri hizi mbili. Serikali inakubaliana na ushauri wa Kamati na Wahesimiwa Wabunge kwamba, suala hili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi hakika utaimarisha ushirikiano na ujirani mwema na vilevile utafungua na kuongeza fursa nyingi za kuendeleza rasilimali za Bonde la Ziwa Nyasa na vilevile rasilimali zilizo katika Ziwa lenyewe na hivyo basi kuleta maendeleo ya Wananchi wa Tanzania na Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwishalitolea maelekezo kuhusu mchakato na ametoa maelekezo kwa Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu usimamizi, uratibu na ukamilishaji wa kazi ambazo Timu ya Serikali ya Wataalam imepewa ili hatimaye waishauri Serikali namna ya kuendelea. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maana hili amekwishalitolea maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bahati kama walivyosema wachangiaji waliotangulia, Rais wa Malawi, Mheshimiwa Bingu Wamutharika ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU) na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ni Mwenyekiti Mstaafu wa AU. Mimi ninasema ni fursa ya kipekee na ya kihistoria iliyojitokeza ya kupata ufumbuzi na maelewano kwa njia ya kidiplomasia na kindugu katika misingi ya ujirani mwema na maslahi ya pamoja ya Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mpesya na vilevile Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kutushauri kwamba, tuanze kwa kutambua kuwa Malawi na Tanzania ni marafiki, tusianze kwa kutambua au kuwa na hisia kwamba Malawi na Tanzania ni maadui. Tukianza hapo, nadhani tunaweza tukapata ufumbuzi wa tatizo la mpaka kati ya Tanzania na Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kijumla na la msingi ni lile linalohusu fursa za kiuchumi zinazotokana na utekelezaji wa Mkataba huu. Moja ya fursa zitakazojitokeza ni katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya Pamoja. Nina hakika kwamba, misaada itakayotolewa kupitia Programu hii au programu za pamoja na miradi ya pamoja, itakuwa mikubwa na mara nyingi Wahisani, Wafadhili na Washirika wetu wa Maendeleo, wanapenda sana kufadhili miradi ya namna hii, kwa sababu nao wanaona inatuunganisha pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri wa programu ndogo ambayo inatekelezwa katika Bonde hili ni programu inayotekelezwa na Malawi na Tanzania ya Mto Songwe, ambayo itahusu ujenzi wa Mabwawa makubwa na kutenga hekta takriban elfu sita za umwagiliaji kwa upande wa Malawi na Tanzania kwa ujumla na itahusu udhibiti wa mafuriko, umeme, uvuvi, utalii na ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni faida kubwa itakayotokana na utekelezaji wa programu ndogo katika programu kubwa ndani ya Bonde la Zambezi. Niseme tu,

tumekubaliana na Malawi kwamba, Makao Makuu ya Programu Ndogo ya Songwe yatakuwa Kyela na tumeanza kuyatayarisha. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwingine wa pamoja wa umwagiliaji ambao Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* imeonesha nia ya kusaidia; Mradi wa pamoja wa Zambezi Juu na Shire ambao unahusisha nchi za Msumbiji, Malawi na Tanzania.

Nadhani sasa tutakapokuwa ndani ya ZAMCOM inakuwa rahisi sana hata kujenga hoja ya kupata fedha kwa ajili ya Programu Ndogo ndani ya Programu Kubwa. Kwa kweli ni miradi mingi ambayo inatarajiwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa nyingine ambayo itatokana na utekelezaji wa Mkataba ni ajira na inakuja katika maeneo yafuatayo:-

Nina hakika kwamba, tutapata nafasi ya kuwa na Watanzania ambao watafanya kazi katika Makao Makuu ya ZAMCOM. Ni kweli kwamba, kutakuwa na ushindani, lakini vilevile katika SADC kuna suala zima la uwiano, haiwezekani nchi moja au mbili zikachukua nafasi zote. Kwa hiyo, nina hakika Tanzania itakuwa na nafasi yake ya kipekee katika Makao Makuu ya ZAMCOM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile limezungumzwa suala la uwezekano wa Tanzania kuwa Makao Makuu ya ZAMCOM; tutalifuatilia hili. Nimeongea na Mheshimiwa Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa amesema, atatumia nafasi yake tusaidiane katika kufanikisha hili na kuuridhia Mkataba huu. Linatupa nguvu sasa ya kuliweka suala hili katika ajenda yetu; tukiwa nje haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimependezwa na wazo lililokuja la uwezekano wa kuwa na Ofisi za Kanda, hili nalo tutalichukua kama moja ya ajenda yetu ndani ya ZAMCOM. Mwishoni hapa limekuja suala la uwezekano wa kuwa na Chuo cha Utafiti, sasa sijui kama kitakuwa Peramiho au sehemu nyingine, lakini ni wazo zuri ambalo nalo tunalichukua katika Ajenda ya Tanzania mara tutakapokuwa tumeridhia na kuwa Wajumbe kamili wa ZAMCOM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa nyingine za kiuchumi kwa kweli zinatokana na miradi inayoendelea hasa miradi ya umwagiliaji katika Bonde la Ziwa Nyasa, ambayo ni sehemu ya Bonde la Zambezi. Miradi hiyo ni Ngana, Kasiabone, Kisegese, Kifunda, Manda, Lifua, Mkiu na mingine mingi ambayo tunaanza kuitekeleza kwa maana ya kufanya utafiti na baadae kuiibua kama miradi mikubwa. Kwa hiyo ni kazi zinazoendelea katika Bonde la Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipango mahususi ya kuendeleza mikoa iliyo katika Bonde; naomba niseme tu kwamba, ndani ya Serikali katika Wizara yangu tuna Mpango wa Uwiano wa Mabonde yote Tisa ya Maji, tumeanzia na Bonde la Ruvu, Bonde la Ndani na Bonde la Kati. Mabonde mengine saba, ikiwa ni pamoja na Bonde la Ruvuma na Bonde la Nyasa, utekelezaji wake unaanza mwaka 2010/2011, unahusu

vyanzo vya maji, mizania ya maji, uendelezaji wa mabonde, kwa maana ya utalii, kilimo na mifugo, maji, miundombinu na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, nathibitisha hapa kwamba, uendelezaji wa Mabonde haya ni suala mtambuka, halihusu Wizara ya Maji na Umwagiliaji tu, linahusu wadau wengi ikiwa ni pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ujumla ambalo ni muhimu sana nalo ni; uhai wa Bonde unatokana na utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji. Ili maji yaendelee kuwepo na Bonde liendelee kuwepo, inabidi tutunze mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikakati iliyopo katika Mkakati Mkubwa wa Kitaifa wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, ambao ulitangazwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais na unasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ni suala zima la kuongeza maeneo ya hifadhi ili iwe sehemu ya Mkakati wa Kutunza Mazingira na Vyanzo vya Maji. Tulianza na Ihefu, ilikuwa kazi kubwa lakini matokeo yake sasa tumeanza kuyaona na ninaamini kabisa vizazi vinavyokuja, vitatushukuru kwa hatua hii ambayo tumeichukua; vinginevyo vingetulaani kama tusingefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Milima ya Livingstone, tunachukua pendekezo lililotolewa na Waheshimiwa hapa wakati wakichangia la kuongeza eneo la Hifadhi ya Kitulo ili lihusike vilevile na sehemu ya Milima ya Livingstone hasa maeneo ya miteremko, maeneo ambayo hayakaliwi na watu, lakini watu wanaendelea kulima na vilevile ni maeneo ambayo yanachomwa mioto kiholela na tatizo lake ni kwamba, hatimaye vyanzo vya maji vitakauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, itasaidia sana kutunza vyanzo vya maji, itapunguza uchomaji wa moto kiholela, itasaidia misitu kukua na itahifadhi bayoanuwai. Ninatoa wito kwa Halmashauri hasa zinazohusika na Safu za Milima ya Livingstone; Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Halmashauri ya Makete, Halmashauri ya Ludewa na Halmashauri ya Mbinga, wakutane na kuwa na Mkakati wa Kitaifa ndani ya Mkakati Mkuu kuhusu Utunzaji wa Mazingira na Vyanzo vya Maji katika Safu za Milima ya Livingstone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wadau wakubwa kwa maana ya Bonde, tutakuwepo katika kusaidia kufanikisha hilo ili wote twende pamoja, Halmashauri, Serikali, hasa sisi Wizara ya Maji na Umwagiliaji, pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa maana ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo mahususi liliulizwa suala kwa nini Zambia haijasaini mpaka sasa? Kama nilivyosema katika hotuba yangu kwamba, Zambia imeamua ambalo ni jambo zuri tu kwamba, ngoja kwanza iweke sawa mambo yake nyumbani, kwa maana ya Sera, Mikakati, Mipango, Sheria na Sheria za Rasilimali Maji. Sisi tuna imani kabisa kwamba, hatimaye itahusika. Kama wahenga wanavyosema, unaweza ukachagua rafiki, lakini huwezi ukachagua jirani, sisi ni majirani wa kudumu tu kwa hiyo tutaendelea kuishi na Zambia. Kwa hiyo, hawezi kutukimbia kwa maana ya

sisi Tanzania na majirani wengine katika Bonde la Zambezi; jiografia na haidrolojia inatuunganisha pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa vilevile kwa maana ya suala mahususi; nini kitatokea iwapo hakutakuwa na maridhiano au makubaliano katika utekelezaji wa Mkataba huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20 cha Mkataba kinahusu pale nchi inaposhindwa yenyewe kutekeleza Mkataba huu na inabidi itoe taarifa katika Sekretarieti ambayo itawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri ambao watatoa uamuzi. Vilevile ukiangalia kifungu cha 21 kitahusika na migogoro inayotokana kati ya nchi au baina ya nchi katika Bonde. Sasa hapa ni suala ambalo mfumo mzima wa SADC umejipanga sawasawa, kwa maana ya kwamba, suala la namna hiyo litapelekwa Mahakama ya SADC. Tukumbuke kwamba, mmoja wa Majaji wa Mahakama ya SADC si mwingine bali ni Mheshimiwa Frederick Mwita Werema kutoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna migogoro kati ya nchi zilizo katika Bonde na nchi nje ya SADC, basi taratibu za kimatifa zitafuatwa za kutatua migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine mahususi linahusu matetemeko. Matetemeko kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ni kitu cha kawaida sana katika Bonde la Ufa lakini tunafanya nini? Nina uhakika kwamba, wenzetu Wakala wa Jiolojia *(Geological Survey),* hili suala wanalishughulikia kama moja ya kazi zao na wanashirikiana na vituo vingine duniania. Vilevile ushirikiano huu unaratibiwa na Wizara ya Nishati na Madini na ninakumbuka kwamba, wenzetu wa hali ya hewa *(Tanzania Meteorological Agency*) nao hili suala wanalifuatilia kwa ushirikiano na Wakala wa Jiolojia *(Geological Survey)* na Wizara ya Nishati na Madini. Naamini wana mipango na mikakati ya kuweka vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu nakumbuka nilipoanza Ubunge, mimi na Profesa Mwakyusa, suala hili lilitukumba; yale matetemeko ya kila siku kwa muda wa miezi miwili, yaliyotokea katika Wilaya ya Rungwe na tulifuatilia kwa makini sana kuhakikisha kwamba, angalau Serikali inakumbuka kwamba, kuna suala zima muhimu la kuweka vituo na Idara ya Jiologia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni mmoja wa wadau katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, tunaendelea kusaidiana na tunaendelea kuwa pamoja. Ninadhani tutalifikisha hili Jahazi, pale ambapo aliyetuteua alitarajia tutalifikisha. Tunamuomba Mwenyezi Mungu, atusaidie katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru vilevile Katibu Mkuu, Ndugu Christopher Sai, yeye ni mzoefu wa siku nyingi, tumefanya kazi pamoja tangu miaka ya 1990s nikiwa Katibu Mkuu wake, sasa Katibu Mkuu wangu; kwa hiyo, nadhani timu hii imekamilika. *(Makofi)*

Ninawashukuru pia Watendaji; Mkurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, pamoja na wote ambao wamelishughulikia sana suala hili. Wakati mwingine walikuwa wanashangaa wanasema; itakuwaje Sheria mbili za Maji zilichukua siku mbili lakini Azimio moja la Zambezi limechukua siku nne; nikawaambia hii ndiyo demokrasia. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM), kwa kutimiza miaka 33 Tarehe 5 februari, mwaka 2010. Mwenyezi Mungu, atujalie ili miaka 33 inayokuja tuwepo, tusherehekee tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Uongozi na Wanachama wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rungwe kwa kufanikisha Sherehe za Miaka 33 ya CCM, Mkoa wa Mbeya wakiwa wenyeji. Nawashukuru sana Wananchi wa Rungwe Mashariki, imani yao kwangu ni kubwa wakati mwingine inanitetemesha. Ushirikiano wao ambao wanaendelea kunipa ni mkubwa, tuendeleze umoja wetu na ushirikiano ambao mpaka sasa umetuwezesha kufanya mambo makubwa katika kipindi cha miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, kwa heshima kubwa na unyenyekevu, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Maji ya Bonde la Mto Zambezi Liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Napenda nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuweza kuliwasilisha Azimio hili na hatimaye kuweza kulisimamia mpaka limeweza kupitishwa na Bunge; hongera sana Mheshimiwa Waziri. Sasa nichukue nafasi hii kumwita Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili naye sasa aje awasilishe Azimio lake la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za SADC *(The SADC Mutual Defence Pact).*

Karibu Mheshimiwa Waziri.

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za SADC *(The SADC Mutual Defence Pact)***

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele yenu. Nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge, kutoa rambirambi kwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Vita

Kawawa na kwa Watanzania wote, kwa kuondokewa na Mzee wetu, Hayati Rashid Mfaume Kawawa, Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; natoa shukurani zangu binafsi kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kuhusu Ulinzi wa Pamoja *(SADC Mutual Defence Pact)* ili Bunge lako liujadili na hatimaye kuuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya madhumuni ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* mwaka 1992 ni kudumisha amani na usalama baina ya nchi wanachama wake. Hivyo, ili kufanikisha azma hiyo, Nchi za SADC zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali, kwa mfano, katika mwaka 1996 zilianzisha chombo cha kushughulikia ushirikiano katika nyanja za Siasa, Ulinzi na Usalama *(SADC Organ on Politics, Defence and Security Co-operation – SADC Organ).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SADC – Organ* iliandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa Itifaki kuhusu maeneo inayoyashughulikia *(Strategic Indicative Plan for the Organ - SIPO*), ambao ulitiwa saini na Wakuu wa Nchi za *SADC* katika mkutano wao uliofanyika mwezi Agosti, 2001 Blantyre, Malawi na kupitishwa rasmi mwezi Aprili, 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mwongozo huo, upo Mkataba wa Pamoja wa Nchi za *SADC* kuhusu Ulinzi *(SADC Mutual Defence Pact)*, uliotiwa saini na Wakuu wa Nchi za *SADC* katika mkutano wao uliofanyika tarehe 26 Agosti, 2003 Dar es Salaam, Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Azimio hili ni kipengele cha 17 cha Mkataba huu, kinachohitaji nchi wanachama kuuridhia Mkataba huu kulingana na taratibu zao za kikatiba ili uanze kutekelezwa. Aidha, Wakuu wa Nchi za *SADC,* akiwemo Rais wetu, katika mkutano wao uliofanyika Maseru, Lesotho, tarehe 17 hadi 18 Agosti, 2006 walihimiza nchi ambazo bado hazijaridhia Mkataba huu, kutoa umuhimu wa pekee juu ya suala hili. Kwa mujibu wa mwongozo, utekelezaji wa Mkataba huu unatakiwa kuanza siku 30 baada ya theluthi mbili ya nchi wanachama kuuridhia.

Hadi kufikia Tarehe 17 Julai, 2008 nchi zilizoridhia Mkataba huu zilifikia 9 nazo ni Zimbabwe, Afrika Kusini, Namibia, Mauritius, Lesotho, Botswana, Msumbiji, Swaziland na Zambia. Nchi hizi ni kati ya nchi 12 zilizotia saini na kati ya nchi 14 Wanachama wa Jumuia ya *SADC;* hivyo, kwa idadi hii, theluthi mbili ilikuwa imefikiwa na hivyo Mkataba huu kuwa na nguvu kisheria kwa Wanachama wote wa *SADC*. Tanzania ni moja kati ya nchi wanachama 12 zilizosaini lakini bado haijaridhia Mkataba huu. Nchi nyingine zikiwa ni Malawi na DRC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba kwa kifupi niorodheshe vipengele kumi muhimu vya Mkataba huu vilivyoainishwa navyo ni kama ifutavyo:-

(i) Pale inapobidi, kwa pamoja kukabiliana na mashambulizi ya kijeshi dhidi ya nchi mwanachama.

(ii) Kukuza mahusiano na ushirikiano kati ya majeshi ya nchi wanachama katika mafunzo na mazoezi.

(iii) Kubadilishana taarifa za kiusalama na kushirikiana kufanya tafiti kuhusu uzalishaji wa vifaa na zana za kijeshi.

(iv) Kutohifadhi au kutounga mkono mtu au kikundi ambacho kinachangia kudhoofisha usalama wa nchi mwanachama, mipaka yake, hali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

(v) Kuheshimu uhuru, hadhi na mipaka ya nchi nyingine.

(vi) Kutokulea, kuhifadhi au kuunga mkono mambo yenye nia ya kuleta vurugu au kuhatarisha usalama wa kisiasa, kijeshi, uhuru na usalama wa nchi mwanachama.

(vii) Kujenga utayari wa kijeshi kwa nchi moja moja na nchi zote kwa pamoja ili kudumisha amani, utulivu na usalama.

(viii) Nchi mwanachama inaweza kujitoa baada ya kupita miezi kumi na mbili tangu kuwasilisha maombi kwa Mwenyekiti na itaacha kupata haki zote chini ya Mkataba huu.

(ix) Mkataba huo unaweza kufanyiwa marekebisho endapo nchi yoyote mwanachama itapendekeza kufanywa hivyo na kuungwa mkono na theluthi mbili za nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuorodhesha vipengele muhimu vya Mkataba wa Pamoja wa Ulinzi, naomba pia nitaje matokeo yatakayotokana na kuridhiwa kwa Mkataba huu. Kuridhiwa kwa Mkataba huu kutakuwa na matokeo yafuatayo:-

(i) Kupungua kwa uwezekano wa kuwepo misuguano na migogoro kati ya Tanzania na nchi jirani za *SADC*.

(ii) Kuwepo mbinu na nguvu zaidi za kijeshi katika kukabiliana na migogoro na ukanda wetu wa Afrika kuwa na amani na utulivu.

(iii) Majeshi ya Tanzania yatanufaika na mafunzo na kupata uzoefu kutoka majeshi ya nchi nyingine.

Mheshiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17 ya Mkataba wa Pamoja wa Nchi za *SADC* kuhusu Ulinzi inaainisha kwamba, hatua zichukuliwe na kila nchi mwanachama kuridhia Mkataba huu kwa kuzingatia taratibu zao za kikatiba. Kwa hiyo, Tanzania inahitaji kuuridhia Mkataba huu kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hakuna gharama inayoambatana na hatua ya kuridhia Mkataba huu, ukiacha malipo ya ada ya uanachama wa Tanzania katika *SADC,* ambayo hutengewa fedha katika Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi mbalimbali hususan Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Idara ya Usalama wa Taifa, wamekuwa wadau wakuu katika hatua zote za kuunda *SADC Organ,* kuandaa na kusaini Mkataba huu. Wote wanakubali kuwa upo umuhimu wa Tanzania kuridhia Mkataba huu. Aidha, Wizara ya Katiba na Sheria, ilishirikishwa kwa kutoa ushauri katika hatua zote za maandalizi ya Mkataba huu na kukubali Tanzania iweke saini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali, Mkataba huu ulipaswa kutekelezwa kisheria na nchi zote Wanachama wa *SADC* kuanzia tarehe 17 Julai, 2008 baada ya nchi 9 kati ya nchi 12 kuwa zimekwishauridhia. Hivyo, Tanzania kama mwanachama mwingine wa *SADC*, inawajibika kuutekeleza Mkataba huo kisheria, lakini ili uweze kutumika kwa mujibu wa sheria za nchi yetu ni lazima uhalalishwe Kisheria. Kutokana na hali hii, Mkataba huo unaletwa mbele ya Bunge lako Tukufu ili ujadiliwe na hatimaye kuridhiwa na Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za *SADC* (*SADC Mutual Defence Pact*) kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC);

NA KWA KUWA moja ya madhumuni ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ni kudumisha amani na usalama baina ya nchi wanachama;

NA KWA KUWA ili kufanikisha azma hiyo nchi wanachama zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali kama ile ya kuanzisha chombo cha kushughulikia ushirikiano katika nyanja za siasa na usalama;

NA KWA KUWA *SADC* iliandaa mwongozo wa utekelezaji wa Itifaki kuhusu maeneo unayoyashughulikia *(Strategic Indicative Plan for the Organ – SIPO)* na kutiwa saini na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Mwongozo huo vile vile upo Mkataba wa Pamoja wa Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika kuhusu Ulinzi *(SADC Mutual Defence Pact*) ambao Tanzania imesaini ili kushirikiana katika masuala yanayohusu Ulinzi;

NA KWA KUWA kwa kusaini Mkataba huo wa Ulinzi, nchi wanachama zitashirikiana katika kukabiliana na mashambulizi ya kijeshi dhidi ya nchi mwanachama, zitakuza uhusiano wa kijeshi kati ya nchi wanachama, zitabadilishana taarifa za kiusalama pamoja na kushirikiana kufanya utafiti kuhusu uzalishaji wa vifaa na zana za kijeshi na kuheshimu uhuru, hadhi na mipaka ya nchi nyingine.

HIVYO BASI, Bunge hili katika mkutano wake wa Kumi na Nane na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* kuhusu Ulinzi wa Pamoja *(SADC Mutual Defence Pact).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. FETEH SAAD MGENI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuja mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa Azimio kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) na Kanuni ya 114(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja na Nchi za *SADC* kuhusu Ulinzi *(SADC Mutual Defence Pact*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kutoa pole za dhati kwa Mjumbe mwenzetu wa Kamati, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Familia yake kwa ujumla, kwa kuondokewa na Mzee wetu, Hayati Rashid Mfaume Kawawa, tarehe 31 Disemba, 2009 na pia kuondokewa na mdogo wake, Ndugu Habiba Kawawa; Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pia natoa pole kwa Mbunge mwenzetu na Wananchi wa Wilaya ya Kilosa, kwa kukumbwa na janga la mafuriko; na mwisho kwa wale wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki katika ajali za barabarani zilizotokea hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 18 Januari, 2010 Kamati ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na kupata maelezo kuhusu Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa. Kamati ilielezwa madhumuni ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika *(SADC)* mwaka 1992 kuwa ni kudumisha amani na usalama baina ya nchi wanachama. Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa, iwapo Bunge litaridhia Mkataba huu, utekelezaji wa azma ya *SADC* katika nyanja ya ulinzi na usalama utaimarishwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe walijadili kwa kina na kutoa hoja mbalimbali ambazo zilitolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri. Hata hivyo, Kamati iliomba ufafanuzi zaidi kuhusu kipengele namba tano cha Mkataba kinachosisitiza juu ya kuheshimu uhuru, hadhi na mipaka ya nchi. Hoja ya msingi ya wajumbe iligusa utata wa mpaka baina ya Tanzaina na Malawi katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Januari, 2010 Kamati ilikutana tena Mjini Dodoma na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Husein Ali Mwinyi, kupata ufafanuzi kuhusu masuala yaliyojitokeza katika kikao cha kwanza cha kujadili Azimio husika. Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Kapteni John Z. Chiligati; Mawaziri wote wawili walieleza historia ya tatizo la mpaka baina ya Tanzania na Malawi na hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Tanzania katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya Mawaziri, Kamati ilishauri kuwa, Serikali ifanye juhudi za makusudi kupata jawabu la kudumu kuhusu tatizo hili la mpaka kati ya Tanzania na Malawi eneo la Ziwa Nyasa, ambalo limedumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha kama Mkataba unaokusudiwa kuridhiwa hauna vipengele vinavyopingana na Katiba na Sheria nyingine za nchi, Kamati ilikutana tena tarehe 0 Februari, 2010 ili kujiridhisha kabla ya kulishauri Bunge lako kuridhia Mkataba huu. Kikao hicho cha tarehe 2 Februari, 2010 kilihudhuriwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, baada ya ufafanuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilihakikishiwa kuwa Mkataba husika hauna kipengele chochote kinachopingana na Katiba wala Sheria za Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mapendekezo ya Serikali kuomba Bunge liridhie Mkataba huu. Nianze kwa kusema kuwa, kwa ujumla Kamati imeridhika kwamba, iwapo Bunge lako litaridhia Mkataba huu, yapo manufaa kwa nchi yetu katika Sekta ya Ulinzi na Amani ya Nchi. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa mkataba huu unaheshimu uhuru, hadhi na mipaka ya nchi, Kamati inashauri kuwa Serikali itumie fursa hii kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mpaka wa Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa;

(ii) Serikali itumie fursa inayopatikana kwa kuridhia Mkataba huu ili kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati ya majeshi ya nchi wanachama katika mafunzo na mazoezi ya kijeshi;

(iii) Utekelezaji wa Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa uende sambamba na kutumia vema taarifa zinazotokana na tafiti za pamoja za kijeshi miongoni mwa Nchi Wanachama wa *SADC;*

(iv) Mkataba huu utumike pia kuimarisha ulinzi katika Bahari ya Hindi miongoni mwa nchi wanachama ambazo zinapakana na bahari hiyo hasa kudhibiti uvuvi haramu na uharamia; na

(v) Serikali iendelee na uimarishaji ulinzi wa mipaka yake sambamba na kutekeleza masharti ya Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maoni haya, yapo mambo muhimu kwa ulinzi wa nchi yetu, ambayo Kamati imebaini ilipokuwa inashughulikia Azimio hili. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, taarifa mahususi kuhusu masuala hayo itawasilishwa ofisini kwako kwa hatua zinazofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kumshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Kapteni John Z. Chiligati na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema, kwa ushirikiano mkubwa na ufafanuzi wa kina walioupatia Kamati wakati ikishughulikia Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za *SADC* kuhusu Ulinzi *(SADC Mutual Defence Pact*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, napenda sasa kuwatambua Wajumbe wa Kamati walioshughulikia Azimio hili la Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwagilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Mst. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan

A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Ibrahim Muhamad Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Stella Mlambo, kwa kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, namwona Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama tena mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja kwa Nchi za *SADC (SADC Mutual Defence Pact*), kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nitoe salamu za mwaka mpya kwa wananchi wote na hasa wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtambile – Pemba. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wanaonipatia siku hadi siku, nitaendelea kuwa msikivu kwa yale yote mnayoona ninatakiwa kuyafikisha katika asasi zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwwenyekiti, Ibara ya (I) inayohusiana na tafsiri ya maneno; neno "*destabilize*" maana yake katika kifungu kidogo cha (c) inasema kuwa, naomba kunukuu: *"Any act or activity aimed at changing the constitutional order of a State Party through unconstitutional means."* Kambi ya Upinzani inaona tafsiri hii inaweza kuleta matatizo makubwa sana kwa nchi mwanachama kutokana na ukweli kwamba, Serikali nyingi zinazokuwa madarakani, kwa kutumia Katiba zao hukataa kuitisha chaguzi au kubadilisha Katiba ili kukidhi matakwa yao. Hivyo basi, ikitokea kundi ambalo linaungwa mkono na wananchi walio wengi likafanya mabadiliko ya uongozi; je, waliofanya mabadiliko hayo watachukuliwa vipi na Umoja huu wa SADC? Vile vile kama nchi imefanya uchaguzi wananchi wakashinda na Serikali iliyo madarakani haitaki kuondoka au kuachia madaraka, tukizingatia kuwa Tume za Uchaguzi zinateuliwa na Serikali iliyo madarakani na Tume ikishatangaza matokeo hayahojiwi na mamlaka yoyote; je, *SADC* inasimama wapi katika suala kama hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya (8) ya Mkataba inasema, nchi mwanachama haitakumbatia makundi ya watu au asasi ambazo nia yake ni ku-*destabilise the political, military, territorial and economic or social security of a state party*. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, japokuwa Mkataba huu ulisainiwa Dar es Salaam na nchi wanachama 12 kati ya nchi zote 14 hapo tarehe 26 Agosti 2003, lakini cha kushangaza ni kwamba, Tanzania ndiyo imekuwa ikikumbatia na kuvilea vitendo ambavyo vimefanyika vya

kutikisa uchumi wetu kwa kuruhusu yale yote yaliyofanyika katika Akaunti ya Malipo ya Madeni ya Nje *(EPA),* pamoja na uhawilishwaji wa fedha za iliyokuwa Kampuni ya Jeshi ya Uchimbaji wa Dhahabu MEREMETA na vitendo vingine ambavyo lengo lake lilikuwa ni kutikisa uchumi wa nchi, pamoja na ulinzi mzima wa jamii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya (11) ya Mkataba kuhusu utekelezaji wa Mkataba huu wa ulinzi wa pamoja; Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwatayarisha wananchi wa maeneo ambayo majeshi ya nchi mwanachama yatawafikia, kwa kuwapatia taarifa kuhusiana na uwepo wa majeshi hayo. Hivyo, hii ni muhimu kwani ni dhahiri kuwa, kila watu wanakuwa na mila na tamaduni zao; vivyo hivyo askari wanaotoka nchi mwanachama wanakuwa na tamaduni zao ambazo inawezekana kuwa tofauti na zetu. Tofauti na hivyo, inawezekana kabisa badala ya kutatua tatizo likatengenezwa tatizo jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, nina mchangiaji mmoja tu kwa Azimio hili, naye ni Mheshimiwa Athumani Janguo; naomba sasa nimpe nafasi hii ili naye aweze kuwasilisha mchango wake.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie katika Azimio hili na namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili linathibitisha ule msemo usemao "Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu." Kwa hiyo, katika masuala ya ulinzi ni vizuri nchi ambazo ni majirani wakaunganisha nguvu zao ili waweze kupambana na lolote ambalo linaweza kuja kutoka nje. Kwa hiyo, napenda niipongeze Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Wasaidizi wake, kwa kulileta Azimio hili ingawa limechelewa. *(Makofi)*

Kama Azimio linavyosema, Mkataba ulipitishwa miaka saba iliyopita na ulipitishiwa Dar es Salaam, lakini leo baada ya miaka saba ndio unaletwa. Tuna sababu nyingi za kuliunga mkono Azimio hili, mimi nitataja sababu tatu tu. Moja Azimio hili litaimarisha ulinzi wa nchi katika Jumuiya ya *SADC;* na pili, litapunguza uwezekano wa *conflicts* baina ya nchi kwa kuwa linazungumzia usuluhishi pale ambapo nchi wanachama huwa hazikuelewana kwa njia moja au nyingine. Mwisho, Azimio hili limepitishwa Dar es Salaam wenzetu katika *SADC* watatushangaa sana kuona kwamba, sisi hatuliungi mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni machache yafuatayo: Kwanza, Azimio hili halielezi waziwazi pale nchi wanachama wanapogombea mipaka kwa mfano Tanzania na Malawi leo hii ila linazungumziwa kutokuingiliwa tu kwenye mambo ya ndani. Pili, Ibara ya 5 inahusu mashauriano na katika kifungu cha (2) cha ibara hii kinampa madaraka Mwenyekiti wa *SADC* kuunda Tume ya Pamoja ya Usuluhishi inapotokea

kwamba, wanachama hawaelewani. Ibara ya 7(2) inasema, hapatachukuliwa hatua yoyote panapotokea kuingiliwa nchi na mwanachama iwapo nchi husika haitaomba msaada.

Sasa mimi ninachoshangaa ni kwamba, katika kipindi hiki cha miaka saba, pamoja na kwamba, bado zipo nchi ambazo hazijamaliza hatua ya pili ya Azimio hili, lakini sielewi kwa nini Tanzania na Malawi bado wameliacha suala hili la mpaka likae kwa muda huu wote. Sasa kwa kuwa nchi 9 kati ya nchi 14 tayari zimesharidhia Azimio hili; ni mategemeo yangu kwamba, Serikali yetu itakuwa ya kwanza kuchukua hatua za kujadiliana na Malawi, walimalize tatizo hili bila hata ya kwenda kupata usuluhishi wa *SADC* kama Azimio linavyosema ili ule urafiki wetu uendelee kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 15, inaelekeza nchi wanachama kufanya marekebisho kwenye mikataba yao na nchi nyingine au jumuiya nyingine pale ambapo mikataba hiyo itakuwa inapingana na Mkataba huu. Hili halitawezekana kufanywa na nchi wanachama kama hizo nchi nyingine hazitakubali kufanya marekebisho katika mikataba hiyo. Sasa hapa hatuelezwi; je, inapotokea hivyo mwanachama afanye nini?

Ninavyofahamu , nchi nyingi za Afrika zina mikataba ya ulinzi baina yao na mataifa mengine hasa ya nje. Unapokuwa una mkataba wa ulinzi, kuubadilisha hivi hivi tu kwa sababu wewe ni mwanachama wa Jumuiya nyingine siyo jambo rahisi. Kwa hiyo basi, sielewi ni namna gani hili linaweza likatekelezwa bila ya kuwepo na matatizo na ambapo wale wa nchi nyingine wakikataa kufanya marekebisho maana yake nchi mwanachama ya *SADC* kwa mujibu wa Azimio hili inaweza ikatatanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea hivyo, njia pekee aliyonayo mwanachama ni kurejea *SADC* na kutaka sasa kufanya marekebisho kama tunavyoelezwa na kifungu kidogo cha (3) cha Ibara ya 19 ili marekebisho haya yafanyike katika Mkataba huu. Lipo pia suala la kwamba, hayawezi kufanyika marekebisho hadi theluthi tatu ya wanachama ikubaliane nawe. Je, wasipokubali nchi mwanachama ina nafasi ipi ya kuweza kuendelea kuuheshimu Mkataba huu na pia bila ya kuvunja Mikataba yake na nchi nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pamoja na maoni yangu yote, Mkataba huu kama nilivyosema mwanzo, bado una manufaa makubwa sana kwa Wanachama wa *SADC*. Kwa maana hiyo basi, mimi sina tatizo la kuliunga mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono na nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Athumani Janguo. Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba, nilitangaza kuwa tuna mchangiaji mmoja tu, lakini kwa bahati nimepata maombi, kwa hiyo sasa nina wachangiaji watatu na hao ndio watakuwa wa mwisho. Nitaanza kwa kumwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, atafuatiwa na Mheshimiwa John Komba na baadaye tukamalizia na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha Azimio hili muhimu sana kwani sasa hivi ni wakati muafaka kabisa kwa nchi zetu za Kiafrika tukielekea katika kujenga Umoja wa Bara la Afrika basi hizi *Regional Blocks* nazo zijitahidi kujenga umoja katika Taasisi zake zote na moja ni hii ya mambo ya ulinzi. Kwa hiyo, naomba nitangulize tu kwamba, naliunga mkono Azimio na naipongeza sana Serikali kwa kuweza kulileta Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mambo mawili madogo, lakini nilifikiri labda Waziri atusaidie. Katika mambo haya, mara nyingi kunakuwa na *double standards.* Inawezekana kabisa nchi ndogo, haraka sana watu wakatoa maamuzi ya kuzipelekea ulinzi. Nchi kubwa kati yenu mkishindwa kufanya, kwa mfano ni rahisi sana kuamua sisi leo kwenda Comoro, lakini tukashindwa sana kwenda Zimbabwe. Sasa hizi *double standards* katika Jumuiya kama hizi ndizo zinadhoofisha hizi Jumuiya yenyewe inapoundwa. Sasa ni vizuri mikataba kama hii tunapoingia tuhakikishe kwamba, haki inatendeka kwa mkubwa na mdogo; vinginevyo, itakuwa umoja huu hauna maana yoyote na hiyo ndiyo *experience* ambayo imetokea katika mikataba ya aina hii. Zile nchi ndogo ndogo zinapoingia, huwa mara nyingi hazina *choice,* wakiamua wakubwa wanafanya, lakini zile nchi nyingine zilizomo ndani ya ule umoja madhali zina ubabe kidogo, zinaweza zikaonesha ubabe wake na zisifanyiwe chochote.

Kwa hiyo, kwa mkataba kama huu, pamoja na kwamba una uzuri wake na Azimio hili linasema ni vizuri hilo tukaliangalia katika hatua tunazokwenda mbele ya safari, lakini ili hatua hizo zifanyike vizuri, kuna suala zima la *harmonization* ya zile *system* zetu tunazozitumia za kiuchaguzi. Siyo tu kwamba, tumekubaliana mambo ya ulinzi na kadhalika, lakini ni vizuri *process* nzima mpaka mtu anapata madaraka basi angalau kuwe na uelewano. Ukiichukua katiba ya mwenzako kidogo ina *element* ya ki-*dictator* na katiba nyingine ina demokrasia kidogo ndani yake, hiyo kazi ya ulinzi yenyewe inaweza kuwa na matatizo. Kwa hiyo, nafikiri *exercise* nyingine ya kufanyika hapa na si kwa sababu ya *SADC* tu peke yake, tukiangalia *context* nyingine ya Bara la Afrika, tumefika mahali sasa tuangalie katiba zetu angalau zina uwiano wa aina fulani kwa wananchi kutoa madaraka yao ya Serikali kuingia kwenye madaraka. Kama hakuna hilo, tutakuwa na matatizo makubwa sana.

Kwa hiyo, tunaweza tukaunda Taasisi lakini zikagongana katika misingi ya kuwapata viongozi kuingia katika madaraka. Kwa kuanzia kwa upande wa *SADC,* tuangalie hizi katiba zetu kama zina uwiano wowote katika kuwapata viongozi wanaoingia kwenye madaraka. Hiyo itarahisisha sana kuweza kuzilinda nchi hizi, kwa sababu *system* zetu zinakwenda pamoja kwa Afrika Mashariki na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa katika chaguzi tu za Bunge la Afrika Mashariki, Tanzania tuna utaratibu tofauti, Kenya wana utaratibu tofauti, Rwanda wana utaratibu tofauti na kila Bunge lina utaratibu wake. Kwa hiyo, hakuna *harmonization*; mnafika mahali wenzenu wanakwenda Mahakamani wana-*block the all process* kwa sababu tu hakuna uwiano katika utaratibu mzima wa kupatikana Wabunge wake. Mimi nafikiri hili ni jambo ambalo ningetaka niseme kwamba ni muhimu sana likazingatiwa na likaheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niliona katika Azimio hili, sehemu nyingi linazungumzia "*may*", "*may*", hakuna *enforcement order* mahali popote. Inanipa mashaka kabisa, hii *organ* itakuwa na nguvu ya aina yoyote, inanipa mashaka kama hili Azimio linaweza kuwa *effective* katika utekelezaji wake, wakati hakuna mahali popote ambapo *enforcement order* inaweza ikatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema hayo na naunga mkono Azimio. *(Makofi)*

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja yenyewe, lakini kama mnavyokumbuka, tangu nimeingia Bungeni miaka minne iliyopita, nilikuwa nazungumzia sana Protokali ya Ziwa Nyasa. Jimbo lote la Mbinga Magharibi ni mwambao wa Ziwa Nyasa. Tatizo ambalo tunalipata sisi wananchi wa kule ni kunyanyaswa na wenzetu wa Malawi. Kila kukicha Majeshi ya Ulinzi ya Malawi ama *convoy* za ulinzi za Malawi zinakamata watu wetu wanaovua, wala hawafiki katikati ya Ziwa pengine wako ndani ya maji kidogo tu, wanakamatwa wanapelekwa kule wanapata adhabu kali kwa sababu tu kwamba wanadai mpaka wao uko kandokando ya Ziwa. Hii ni kero kubwa sana kwa wananchi wanaoishi kandokando pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi alikuja Mzungu mmoja kuwekeza hoteli kule akaniambia nimekuja lakini unihakikishie wewe Mbunge kama kweli eneo ninalotaka kuwekeza ni lenu, yaani ni eneo la Tanzania. Nikamchukua Mzungu yule mpaka Dar es Salaam kwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alimthibitishia kabisa kwamba, eneo hili ni letu. Akaenda kwao kuomba *funds* ajenge hoteli. Kwao akaambiwa nenda upande wa pili wa nchi nyingine inayodai kwamba eneo hili ni mali yake. Wale wakasema hapana eneo unalotaka kujenga ni mali yetu. Mzungu yule akaondoka na mali zake na fedha zake akaenda zake Ulaya tukakosa uwekezaji ule. Sasa kitu kama hicho, kinavunja moyo sana wananchi wanaokaa eneo hilo. Tunaomba sana kama kweli tuko *serious,* hizi Kamati za Ulinzi basi zikutane na wenzao kule. Marais wakutane waseme na watu wajue kuna nini kinaendelea katika mpaka kati ya Tanzania na Malawi.

Tunaomba wakikutana waeleze sisi Watanzania tuna haki gani katika Ziwa lile. Maziwa yetu yote; Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika na kandokando ya bahari, uwekezaji wa hoteli ni mkubwa sana. Inasikitisha sana, ukienda Ziwa Nyasa uwekezaji hakuna kabisa na kuna pwani nzuri, mchanga mweupe, maji meupe, samaki wenye rangi mbalimbali, lakini watu wanashindwa kwenda kule kwa sababu kuna utata juu ya mpaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopitisha jambo hili, tukumbuke kwamba tunawaumiza sana wananchi wa Jimbo langu. Basi tupitishe kwa jambo jema lakini tuwasaidie wananchi wale wajue kwamba lile Ziwa nao wana haki nalo *hundred percent.* Mchango wangu ni huo tu na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Azimio hili. Kwanza, napenda

kusema naunga mkono, lakini pili napenda kusema kwamba, Azimio limekuja katika kipindi ambacho tuna changamoto nyingi sana na hasa sisi kama Watanzania tunaunga Azimio la Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika *(SADC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baadhi ya wenzetu hawako katika mfumo huu. Nadhani ingeleta maana nzuri zaidi tunaporidhia Azimio kama hili, tuangalie changamoto gani ambazo tunazo kwa sasa. Sisi tunalilia ndiyo, lakini wenzetu tulionao ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wako nje ya Azimio hili. Tunahitaji kupata ulinzi na amani katika nchi yetu. Sasa ni vema Mheshimiwa Waziri angeweza kuliona hili na liwe sehemu mojawapo ya changamoto ili tuone kama Tanzania, kuridhia kwetu kuwe na tija ambayo italeta manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile utakuta kwamba, kuna Maazimio mengi tumeridhia. Kwa mfano, tuna Azimio la *International Conference for Great Lakes Regions,* ambayo Katibu Mtendaji wake ni Mtanzania, Balozi Mulamula, yuko kule Burundi. Unakuta sisi wenyewe kama Tanzania tunachelewa hata kutoa michango. Sasa ni kitu ambacho nakumbushia kwamba, Maazimio kama haya ambayo yanakuwa yanagusa nchi yetu na hasa katika anga za kimataifa, tuwe makini sana kuyaangalia, kwa sababu sisi kama Tanzania, nchi yetu ina historia ambayo ina msingi mkubwa sana. Tutaendelea kufanya hivi kama tunatekeleza wajibu wetu wa Kimataifa. Kwa hiyo ni muhimu tunaporidhia Azimio hili, twende sambamba na kutimiza wajibu wetu katika ngazi za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala zima la ku-*standardise*; ambalo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kalizungumzia. Ni kwamba, lazima tuwe na *uniformity* au *standards* ambazo kama wanachama sote tuwe pamoja. Isitokee maamuzi ambayo inapotokea kitu fulani tunachelea kutoa uamuzi, lakini inapotokea suala lingine tunatoa maamuzi ambayo hayaendani na *standard* za pamoja.

Kwa hiyo, nadhani ni muhimu sana Azimio kama hili lijikite kuona kwamba, Tanzania tunajaribu kutoa changamoto kwa wenzetu hata chaguzi zetu katika Umoja wetu huu ziwe na mfumo ambao unaendana ili baadae tunapopata matatizo ya kimfumo, tuweze kuyatatua kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili limekuja muda muafaka na napenda kusema kwamba, mchango wangu ulikuwa ni huo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao na ushauri wao walioutoa. Nataka niwahakikishe kwamba, yote yatazingatiwa. Naomba niwatambue wachangiaji. Wapo waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na wapo waliochangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kuzungumza, kwanza ni Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Masoud

Salum, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Capt. John Komba na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Stanley Kevela, Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Mheshimiwa Vuai Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe hoja hii kwa kujibu baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Napenda nianze na michango iliyotolewa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa ujumla, wamepongeza Azimio hili na wameunga mkono na ushauri wote walioutoa unaendana na Azimio lenyewe, isipokuwa tu hiyo sehemu moja waliyoisisitizia ya kupata muafaka kuhusu suala la mpaka wa Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa. Jambo ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi, lakini niseme kwamba, bahati nzuri jambo hili limeshatolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Mwandosya, aliyetangulia kusema hapa. Sina maneno zaidi ya yale ni kwamba, Serikali inalifanyia kazi, Waziri Mkuu amewaandikia wahusika ili waanze mazungumzo mara moja na taarifa nilizopewa leo ni kwamba, kikao cha kwanza kati ya nchi zetu mbili kitaanza tarehe 11 mwezi huu. Kwa hiyo, suala hili litashughulikiwa na Serikali kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maeneo matatu yaliyotoka kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Aliuliza endapo wananchi watafanya mabadiliko kuiondoa Serikali madarakani ambayo imekiuka Katiba ya *SADC* inawachukuliaje? Jibu ni kwamba, *SADC* inao utaratibu wa kuwafuatilia kwa karibu nyendo za chaguzi, siasa na demokrasia katika nchi wanachama. Kamwe haiungi mkono mabadiliko yasiyokuwa ya kidemokrasia na yanayovunja Katiba ya nchi wanachama.

Vilevile alitaka kujua umuhimu wa kutayarisha wananchi wa maeneo ambayo wanajeshi wa nchi wanachama yatawafikia kwa mujibu wa Ibara ya 11. Tunasema kwamba, hii ni hoja ya msingi na imepokelewa na huko nyuma tumekuwa tukifanya hivyo. Kila wanajeshi wa nchi rafiki wanapokuja kufanya mazoezi nchini mwetu, basi wananchi wa maeneo hayo wanatayarishwa kwa kuelekezwa yatakayotokea hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu hoja za Mheshimiwa Janguo kama ifuatavyo:-

Anasema Muswada haueleziwaziwazi pale nchi zinapogombea mipaka kufanywe kitu gani. Jibu ni kwamba, Ibara ya 5(1) inaeleza kuwa, kukiwa na matatizo ya mipaka, ile inchi inayoona imeonewa itafanya mashauriano kwanza na ile nchi nyingine na baada ya majadiliano suala hilo litapelekwa kwenye *organ*.

La pili, ni kwa nini Tanzania haijapeleka tatizo la mpaka baina yake na Malawi mbele ya Mwenyekiti wa *SADC* kwa mujibu wa Ibara ya 7(2)? Jibu ni kwamba, hii ni kwa sababu Tanzania hatujaridhia Mkataba huu, hivyo hatuwezi kutumia Ibara hiyo mpaka hapo tutakapokuwa tumeridhia Mkataba. Vilevile aliuliza kwamba, kunapokuwa na migongano ya mikataba ya ulinzi na huu wa *SADC* nchi husika ifanye marekebisho ya Mkataba uliopo. Je, nchi husika iliyoingia Mkataba na Mwanachama wa *SADC* isipokubali Mkataba huo ufanyiwe marekebisho; Mwanachama wa *SADC* afanyeje?

Jibu ni kwamba, hadi sasa Mikataba ya Ushirikiano wa nchi nyingine tuliyonayo, haigongani au kupingana na Mkataba huu. Baada ya kuridhia Mkataba huu, tutahakikisha kwamba, mikataba yote mingine inayofuata tutakayosaini inaoanishwa na huu ili isipingane. Aidha, alitaka kujua endapo marekebisho ya mkataba huu yaliyopendekezwa na mwanachama hayajapata kibali katika Ibara ya 19(3) basi nchi mwanachama afanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni kwamba, huu ni utaratibu wa Kisheria kwamba, marekebisho yoyote lazima yapitishwe na idadi fulani inayokubalika na wanachama. Hili limefanywa makusudi kwa sababu nchi za *SADC* ziko 14, leo kila mmoja akianza kuleta mabadiliko itakuwa kila siku Mkataba huu utabadilishwa. Ndiyo maana ukawekwa utaratibu kwamba, mabadiliko yoyote lazima yaungwe mkono na theluthi mbili ya wanachama na huu ni utaratibu wa Mikataba yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na hoja alizozitoa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba, kusiwe na *double standard* katika kutekeleza Mkataba huu. Mimi naamini kabisa kwamba, Mkataba huu unatoa nguvu za kisheria za nchi wanachama kukutana katika migogoro yoyote na kutoa maamuzi ya pamoja na ni imani yangu kwamba, kwa sababu nchi 14 au tuseme kwa sasa hivi nchi ambazo zimesharidhia zitakuwa na uwezo wa kutoa maamuzi ya pamoja juu ya matatizo au migogoro inayokabili nchi wanachama. Kwa hiyo, sidhani kama kutakuwa kuna *double standard*, kwa sababu hili sasa halitakuwa suala la nchi moja moja bali ni maamuzi ya pamoja. Vilevile alitaka kujua kama kutakuwa na *harmonisation* ya *system* ya uchaguzi. Mimi niseme tu kwamba, Mkataba huu unalenga katika suala zima la ulinzi. Ipo mikataba inayozungumzia masuala ya uchaguzi na kadhalika.

Kwa sababu kuna *organ* ya *SADC on politics, defence and security*. Sasa bila shaka kwenye upande ule wa *politics* yatakuwepo makubaliano kuhusu chaguzi na kadhalika. Huu ni mkataba unaohusu *defence,* lengo na madhumuni ni kuimarisha ulinzi wa pamoja kati ya nchi wanachama. Ameuliza vilevile kwamba, mkataba huu unatumia sana neno "*may*" hana uhakika kama utakuwa na nguvu za kufanya *enforcement.* Ninachosema ni kwamba, neno "*may*" limetumika kwa makusudi kabisa kwamba, maamuzi yatatokana na *consensus.* Kwa maana nyingine ni kwamba, kila penye mgogoro, nchi wanachama watakaa pamoja, kwanza mkataba huu unazitaka nchi na nchi wazungumze; endapo itashindikana kupata ufumbuzi, basi waende katika *SADC* na hatimaye upatikane ufumbuzi. Kwa hiyo, hili neno "*may*" limetumika kwa sababu kutakuwa kuna *option* zaidi ya moja.

Mheshimiwa Capt. John Komba amezungumzia suala la mpaka katika Ziwa Nyasa. Hili ni jambo ambalo limevuta hisia za watu wengi. Tunatambua fika, bila kupata ufumbuzi wa jambo hili, bado kutakwa kuna mgogoro kati ya nchi zetu mbili. Kama nilivyosema awali, kuna historia ndefu sana ya suala la mpaka katika Ziwa Nyasa na baada ya mazungumzo kuvunjika mara ya mwisho mwaka 1967, mazungumzo sasa yanaendelea na hivi karibuni kama nilivyosema awali, Mheshimiwa Waziri Mkuu,

amelivalia njuga suala hili na nimeambiwa vikao vitaanza tena tarehe 11 mwezi huu. Ni matumaini yangu kwamba, tutafika sehemu tatizo hili lipate ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa mwisho alikuwa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, ambaye alitaka kujua kwa nini wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wako nje ya Mkataba huu. Ni sahihi kwa sababu Mkataba huu unahusu Nchi Wanachama wa *SADC*; lakini nimueleze Mheshimiwa Chegeni kwamba, Tanzania kama nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tuna ushirikiano wa kiulizi na nchi hizi za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, bila shaka wasiwasi kuwa hakutakuwa na *coordination* na upande wa Afrika Mashariki haupo, kwa sababu tunavyo vikao vya pamoja, lengo na madhumuni ni kufikia kuunda Mikataba inayofanana na hii kwa upande wa Afrika Mashariki vilevile.

Kuhusu lile alilorudia kulikazia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed la *double standard,* kwa sababu sasa baada ya kupitisha Mkataba huu maamuzi yote yatakuwa ni *collective*, nchi zitakaa pamoja zitatoa maamuzi ya pamoja, kwa hiyo imani yangu ni kwamba, kwa kuwa nchi zote hizi ambazo zitakuwa zimeridhia zitakuwa pale; hakuna nchi moja inayoweza kuionea nyingine, isipokuwa maamuzi yatakuwa kwa pamoja kutegemea na hoja ya msingi itakayokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge na niseme tu kwamba, ushauri wao wote umezingatiwa na tutafanya kila njia tuweze kuhakikisha kwamba, baada ya kuridhia mkataba huu, basi ushirikiano wetu wa kiulinzi baina ya Nchi Wanachama wa *SADC* utaimarika na bila shaka kama tulivyosema awali, tutapata uzoefu mkubwa kupitia Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana, hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji napenda niwakumbushe Wabunge wa CCM kwamba, mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge kutakuwa na kikao cha *caucus*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa Nchi za SADC Liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli ambazo zimepangwa kwenye *Order Paper* kwa ajili ya siku ya leo zimekamilika, napenda kuchukua nafasi hii, kuliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.45 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 9 Februari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*